BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Tisa - Tarehe 20 Mei, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaletea salaam kutoka Bunge la Afrika Kusini, Cape Town nilipokwenda. Wale wenzetu wa Cape Town wanautaratibu wa mradi uliochangiwa na Benki ya Dunia kama mradi wetu wa *Legislative Support Programme.*

Kwa hiyo, wanafanya kila mwaka *consultative workshop* ya Maspika wa *Provinces* pale lakini Spika mwenyeji huwa anaalika Maspika wanne wa nchi za *SADC.* Kwa hiyo safari hii mimi nilialikwa na nilifurahi kwa sababu nimejifunza kwamba wenzetu wao wako mbali sana na *Budget Department* na *Budget Committee.*

Kwa hiyo, nimejifunza vizuri sana na nitatumia nafasi hiyo kuiimarisha Kamati yetu ya Bajeti na pengine kuangalia uwezekano wa kuwa na kitengo kizima cha Bajeti kinachoweza kufuatilia sio tu mipango ya Serikali lakini pia na matumizi ya Serikali katika kipindi ambacho tunakuwa nje ya Bajeti. Kwa hiyo tumejifunza sana na nilisikitika sikuweza kwenda na mmoja wa Wajumbe wa Bajeti. Lakini sikujua kama kuna utaalam mkubwa hivyo katika nchi zingine kuliko sisi. Tunaendelea Katibu!

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:-

Hotuba ya Bajeti ya Wizara Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:-

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. CECILIA D. PARESSO (K. n. y. MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO):-

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 233

Jimbo la Nzega Kugawanywa

MHE. JUMA S. NKAMIA (K.n.y. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA aliuliza:-

Jimbo la Nzega linakua kwa kasi na idadi ya watu inaongezeka kwa kasi na kwamba sasa Nzega ina Halmashauri mbili.

(a) Je, ni lini Serikali italigawa Jimbo hilo ili kupeleka uwakilishi karibu zaidi na wananchi?

(b) Je, ni lini Serikali itazigawa na kuzitambulisha Kata zinazotengeneza Halmashauri ya Mji?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 75 kimeipa Tume ya Uchaguzi Mamlaka ya kuchunguza na kugawa mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi kila baada ya miaka 10 au unapokaribia Uchaguzi Mkuu. Kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea maombi 47 ya kugawa Majimbo kutoka katika Halmashauri mbalimbali likiwemo Jimbo la Nzega.

Kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria, Tume iliweza kugawa majimbo sita ambayo ni Tunduru, Nkasi, Kasulu, Bukombe, Singida Kusini na Ukonga.

Aidha Jimbo la Nzega ni miongoni mwa Majimbo 41 ambayo hayakukidhi vigezo vya kugawanywa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakusudia kufanya uchunguzi wa mipaka na kugawa Majimbo kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao na kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Katiba, Jimbo la Nzega litagawanywa kwa kuzingatia vigezo na utaratibu uliowekwa na Sheria. Aidha Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndiyo yenye mamlaka kisheria ya kugawa eneo katika Majimbo ya Uchaguzi.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Nzega ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali *GN Na. 177* la tarehe 17/06/2011 na kubainisha jumla ya Kata 6 ambazo ni Nzega Magharibi, Nzega Mashariki, Kitangili, Uchama, Ijanja na Itilo. Kati ya Kata hizo Kata ambazo zina Madiwani ni tatu ambazo ni Nzega Mashariki, Uchama na Itilo. Kata za Nzega Magharibi, Kitangili na Ijanija ni mpya na hazina Madiwani. Kata hizi mpya zinatambulika na zimetolewa katika tangazo la Serikali.

Aidha, Halmashauri ya Mji wa Nzega itaanza rasmi baada ya uchaguzi wa Madiwani wa Kata hizo mpya kufanyika, zoezi ambalo litahusisha maeneo mengine yenye sura kama hiyo ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Tunduma.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa na swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna ongezeko la Kata tatu katika Halmashauri hii ya Nzega.

Je, Serikali haioni sasa upo umuhimu wa kugawa Wilaya ya Nzega kuwa Wilaya mbili iwe Wilaya ya Bukene anapotoka Mheshimiwa Zedi pamoja na Wilaya ya Nzega?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, haya majibu tuliyojibu hapa ni kwa mujibu wa yale maombi ambayo yalikuwa yameletwa. Kwa hiyo kama Mheshimiwa Nkamia anadhani kwamba sasa wanastahili hii iwe Wilaya kwa maana ya Bukene na Nzega ziwe Wilaya hilo ni jambo lingine kwa sababu sasa tulikuwa tunazungumzia habari ya Tume ya Uchaguzi ndiyo inayounda majimbo.

Sasa likija kwenye upande huo anaouzungumzia linamhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini hatimaye litakwenda kwa Mheshimiwa Rais ambaye ndiye mwenye Mamlaka na Madaraka ya kugawa nchi hii katika sehemu mbalimbali za utawala. Kwa hiyo likija sisi tutalipeleka katika utaratibu huu tuliouleza ili kutekeleza.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Natambua kwamba kuna vigezo ambavyo Serikali inazingatia kabla ya kugawa Jimbo au Wilaya. Je, vigezo hivi vina hadhi sawa au vinazidiana kwa hadhi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ni kweli ili kugawa Jimbo vigezo vinatofautiana. Kwa mfano katika Majimbo ya Mjini idadi ya watu inatakiwa iwe 237,000 na katika Majimbo ya Vijijini idadi ya watu ni 206,000. Lakini pamoja na hilo inaangaliwa uwezo wa mapato, hali ya umaskini, barabara, mawasiliano kama vile usikivu wa radio na vitu vingine, idadi ya mitandao na habari kama hizo. Kwa hiyo ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Telele yako mambo ambayo yanatofautiana na vigezo tofauti kati ya mijini na vijijini.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Wilaya ya Kilombero ina wakazi takribani 600,000 kabla ya Sensa na kwa kuwa Kata moja tu ya Ifakara ina wapigakura 33,000 na wameshaleta maombi ya kutaka kugawanywa kwa hilo Jimbo. Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa Kilombero yenye kata 23.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Naibu Waziri. Hilo ni swali lingine kabisa utatumia vigezo tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, nashukuru na takwimu ambazo Mheshimiwa Mbunge ambazo ametusaidia hapa. Procedure ni kwamba jambo hili linaanzia hukohuko Kilombero, wao watakaa kule watapita katika *District Consultative Committee,* watakwenda kwenye Baraza la Madiwani kule, halafu wakitoka kule watakwenda kwenye Halmashauri inaishauri Mkoa kwa maana ya *RCC, RCC* ni Bunge la Mkoa wanaingia mpaka Polisi na Uhamiaji wote wanaingia mle ndani. Likiletwa kwa utaratibu huo linakuja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, basi baada ya hapo sisi tunamshauri kwa kadiri tutakavyokuwa tumeona baada ya kwenda kucheki hivyo vigezo vyote tulivyoviona hapa. Kwa hiyo ni suala la kupitisha tu kwenye utaratibu.

Na. 234

Watendaji Waliohusika na Ubadhirifu Wizi na Ufisadi

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED (K.n.y. MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM) aliuliza:-

Kwa mujibu wa Taarifa za *LAAC, PAC, POAC na CAG* zilizowasilishwa Aprili, 2012 imebainika kwamba kuna wizi, ubadhirifu na ufisadi wa kiwango ca juu katika Halmashauri, Idara, Wizara a Mashariki ya Umma.

Je, ni watendaji wangapi waliobainika katika maeneo yaliyotajwa wameshachukuliwa hatua za kinidhamu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inapinga vitendo vyovyote vya wizi, ubadhirifu na ufisadi na imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kinidhamu dhidi ya watumishi wa Umma wanaobainika kuhusika na vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, hatua za nidhamu huchukuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 208 pamoja na Sheria nyingine zinazo tawala utumishi wa makundi mbalimbali ya utumishi wa umma. Sheria hizi, pamoja na mambo mengine, zimeainisha mamlaka za nidhamu kwa watumishi wa umma, makosa ya kinidhamu, taratibu za kinidhamu na adhabu zinazopaswa kutolewa kwa watumishi wanaopatikana na hatia hizo. Hivyo, mamlaka za nidhamu ndizo zenye wajibu wa kuchukulia hatua za kinidhamu watumishi walioko chini ya mamlaka husika wanaobainika kujihusisha na vitendo vya wizi, ubadhirifu na ufisadi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizowasilishwa katika ofisi yangu zimeoneshwa kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2013, Serikali ilikuwa imewachukulia hatua za kinidhamu watumishi 128 waliobainika kuhusika katika vitendo vya wizi na ubadhirifu na watumishi 41 waliohusika na ufisadi pamoja na rushwa. Hivyo ninapenda kutumia fursa hii kuzitaka mamlaka za nidhamu katika utumishi wa umma, kuendelea kutekeleza mamlaka hayo kwa kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wote wanaofanya vitendo vya utovu wa nidhamu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizipo na kuitaarifu Ofisi yangu ipasavyo ili hatimaye tuweze kukomesha kabisa vitendo hivi katika utumishi wa umma.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Waziri kakiri kwamba Serikali inapinga vitendo vyote vya wizi, ubadhirifu na ufisadi na bado taarifa za *CAG* zinaonyesha ukosefu wa nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali unaendelea. Hali ya kwamba si Kamati, si *CAG* ambaye anakuwa na meno katika kuwashughulikia watu hawa.

Je, Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari sasa hivi kuipatia Kamati kwa mfano ya *LAAC* inapokwenda katika ukaguzi vyombo vya dola ili pale ufisadi, ubadhilifu na wizi utakapoonekana waweze kuchukua hatua za haraka hapohapo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Inabidi u-*declare* kwamba wewe ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo kwanza. Usimame u-*declare interest* zako.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Spika, naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. *(LAAC).*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, hii haiwezi kufanyika kwa sababu Sheria inayomruhusu *CAG* kufanya ukaguzi inamruhusu pia kwa kushirikiana na vyombo vya upelelezi kuchukua hatua baada ya kufanya uchunguzi thabiti. Lakini ukifanya hivyo unavyofanya ni kama vile unamhukumu mtu bila kumsikiliza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Najua Serikali inajitahidi kwa kiasi chake kuwashughulikia watu ambao wanafanya ubadhirifu katika Serikali yetu. Lakini kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunge humu ndani; Serikali badala ya kuwashughulikia watendaji wa Halmashauri ambao wanafanya ubadhirifu katika Halmashauri zetu hususan kwenye miradi ya maendeleo; na naomba nitoe mfano malalamiko ambayo yaliyopo.

Moja ni Wilaya ya Arumeru na Mheshimiwa Medeye analijua, kuna mtumishi pale ameharibu katika masuala ya ardhi na Halmashauri ilienda kinyume na taratibu kwa kuingiza fedha kwenye akaunti binafsi takribani bilioni nane na hili Mheshimiwa Medeye analijua na amekuwa akilalamikia, badala ya kumshughulikia mtu anahamishwa kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Spika, sasa swali. Ni lini Serikali itawashughulikia watu kama hawa ambao wanafanya miradi ya maendeleo ishindwe kuendelea na mwisho Serikali kuonekana haina dhamira ya dhati kuondoa matatizo kwa Watanzania.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema yeye awali kwamba Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukomesha jambo hili; na hapa nina takwimu za hatua mbalimbali ambazo Serikali imechukua katika upande wa mishahara hewa, upande wa Maliasili, upande wa pembejeo na kadhalika. Kwa hiyo, Serikali inajitahidi kwa upande wake.

Kwa suala la kumtoa mtumishi kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine hili mimi napenda kuwaarifu Wabunge wenzangu kwamba mara nyingine *central* yaani TAMISEMI huwa hawana taarifa ya ubadhirifu katika Wilaya fulani.

Kwa hiyo, tunapohamisha sisi Utumishi tunakuwa hatuna taarifa. Tukiwa na taarifa mara nyingi tunambakisha mtumishi palepale ili aweze kujibu tuhuma zake. Naomba Waheshimiwa Wabunge kama Madiwani tushirikiane kwa sababu sisi ndiyo tunatakiwa kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi walioko katika Halmashauri zetu.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, jibu kuhusu hili alilolisema hili.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba nitoe ufafanuzi kuhusu suala la Halmashauri ya Wilaya ya Wilaya ya Arumeru. Mimi nimekwenda katika Halmashauri ile nimezungumza na Waheshimiwa Madiwani baada ya kuwa wameniita na kwa kuwa kulikuwa na uvutano mkubwa sana ambao ulikuwa unaendelea pale baina ya Halmashauri ile na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimeenda nikakaa nao tukalimaliza lakini hilo halikuingia miongoni mwa hoja, kilichotokea ple ni kwamba Halmashauri ilinunua shamba kutoka kwa mwekezaji kwa lengo la kutaka kugawa viwanja kwa ajili ya wananchi kukawa kidogo sijui niseme ni mgongano wa kimaslahi kwa maana ya Halmashauri bado ule mradi walikuwa wanaung'ang'ania kuwa ni mradi wao.

Ni halali kwa maana ya Baraza la Madiwani isipokuwa kwa upande mwingine kilichokuwa kinaombwa na kuwa lile shamba ambalo Halmashauri imelinunua lilitaka kuwa wagawiwe wananchi bure kwa maana kuwa walime badala ya kugawa viwanja.

Mheshimiwa Spika, lile suala nimelisimamia mimi mwenyewe suala la ubadhilifu linalozungumzwa halikuwepo isipokuwa alichoomba Mheshimiwa Midee ni kwamba tumuhamishe Mkurugenzi, tumhamishe Afisa Ardhi na tuwahamishe Maafisa kama saba kitu ambacho maombi ya Mheshimiwa ni kuhamisha.

Maombi hayo aliyapeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi nikapewa maelekezo na nikafanya kama nilivyoambiwa lakini kwamba kulikuwa na ubadhilifu kwa Afisa Ardhi hilo halipo lakini pia kufungua akaunti kwa ajili ya ule mradi kwasababu walichukua mkopo kutoka benki yalikuwa ni makubaliano ya Halmashauri na siyo uamuzi wa mtu mmoja.

SPIKA: Ninaomba tuendelee na swali linalofuata Ofisi ya Rais Waheshimiwa tunafanya *average,* ni dakika tano kila swali sasa ukienda zaidi yanazidi. Ofisi ya Rais Mheshimiwa David Silinde, ataulizwa swali hilo.

Na. 235

Watuhumiwa wa Ufisadi

MHE. DAVID E. SILINDE aliuliza:-

Kwa kipindi cha hivi karibuni Watanzania wengi wamekuwa wakituhumu Viongozi na Serikali, wanasiasa kuwa ni Mafisadi.

Je, ni lini Kauli ya Serikali juu ya Tuhuma hizo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa David Silinde, kwa niaba ya wadhamini wenzangu wa *Club* ya Yanga. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, jibu swali hakuna muda huo. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, nilichotaka kukisema wamekielewa tunawapongeza vijana wa Yanga kwa nzuri ya juzi. Baada ya bashrafu hiyo ningependa sasa kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, rafiki wa mwanangu Victor, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna takwimu kuonyesha kwamba Watanzania wengi kwa nambari wanawatuhumu viongozi wa Serikali na wanasiasa kuwa ni mafisadi. Ni kweli kuwa kuna tuhuma dhidi ya viongozi na wanasiasa ya ya kujihusisha na rushwa na matumizi mabaya ya Rasilamali za umma. Baadhi ya tuhuma hizo zilichunguzwa na kufikishwa mahamani kesi zinaendelea kwa tuhuma ambazo zilionekama kuna ushahidi na tuhuma zingine hazikuthibitishwa na washtakiwa waliachiliwa huru. Tuhuma ni hisia ambazo ni lazima zithibitishwe vinginevyo siyo haki kutuhumu kiongozi wa Serikali au kisiasa bila kutoa ushahidi wa kuthibitisha tuhuma hizo kwa kiwango kinachotakiwa kwa Sheria za nchi yetu, kiwango hicho ni kuthibitisha mashtaka bila kuacha mashaka yoyote ya maana. Serikali inatoa kauli gani kwanza ningependa kuwaasa viongozi wa Serikali, wa kisiasa na vyama vyote vya siasa kujiepusha na vitendo vya rushwa, kutumia rasilimali za Mamlaka kwa maslahi binafsi na kwamba wawe mfano bora wa uongozi.

Pili, wale wanaotoa tuhuma dhidi ya mtu yoyote watoe ushahidi kwa vyombo vya upelelezi ili viweze kuwashughulikia kwa mujibu wa Sheria tusitoe tuhuma kwa ajili ya kuwachafua watu wengine au Serikali iliyoko madarakani.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali kidogo yana walakini, lakini kwa kuwa Serikali imekiri wazi katika majibu yake kuwa kuna tuhuma kwa baadhi ya viongozi, wanasiasa kujihusisha na rushwa na matumizi mabaya ya rasilimali pamoja na ufisadi na kwa kuwa katika kipindi sasa karibu miaka saba mfululizo tangu mwaka 2005 kumekuwepo na tuhuma za baadhi ya makampuni kama vile meremeta, *Tan Gold, Deep Green, Richmond,* ununuzi

wa rada na kadhalika kwamba ametuhumiwa kuiba fedha.

Je, ni kiasi gani makapni haya yametuhumiwa kuiba fedha za walipa kodi wa Tanzania?

Lakini (b) Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Kikwete aliwahi kutamka hadharani kuwa wale wote walioiba fedha za madeni ya nje *EPA* warudishe fedha hizo na watasamehewa. Je, ni kiasi gani cha fedha kimerudishwa ambacho Mheshimiwa Rais aliwataka hao watu warudishe?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, swali la msingi limetaka kujua kiwano cha ufisadi katika jamii swali la msingi lingeelekezwa kwenye Meremeta, Rada na mambo mengine yote matayarisho ya hilo jibu yangeandaliwa, masuala ya Richmond tumeyazungumza hapa ndani likapita Azimio la Bunge masuala ya Meremeta Waziri Mkuu ameyatolea maelezo, masuala ya wizi wa fedha Uswis Serikali inayafanyia kazi ninachotaka kusema ni kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwa lile jambo ambalo angependa kupata undani na ukweli wake anione nimtafutie majibu kwa sababu hapa swali lake la kwanza ndani yake kuna maswali zaidi ya matano kwa hiyo nitashindwa kujibu moja baada ya lingine kwa maana ya kuwa swali lake la kwanza lilielekezwa *generally* katika suala la ufisadi, jinsi watu wanavyofisidi nchi yetu.

La pili, kiasi gani cha fedha hilo ni swali linalohusu takwimu mimi sikuja na takwimu hapa ningekuwa nimeulizwa nije kueleza kuwa ni kiasi gani cha fedha kimeokolewa hakuna shaka ningekuja na takwimu hiyo.

SPIKA: Ahsante ni jibu sahihi tu lilikuwa ni swali geni Mheshimiwa Mwaiposa swali la nyongeza.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imekuwa ni hali ya kawaida kabisa mtu mwenye gari zuri, mwenye nyumba nzuri au mtu aliye vaa nguo nzuri kuitwa fisadi katika hali ya kawaida na kwa kuwa jina hili au sifa hizi

zimekuwa zina waudhi sana walio wengi kwa sababu mali walizo nazo wamekuwa wamejipatia katika njia halali.

Je, Serikali hivi sasa iko tayari kutoa elimu ya maana halisi ya neno hili ufisadi ili wananchi waweze kulijua na kulitumia vizuri?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, naomba swali la nyongeza la Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya swali la msingi nilieleza kuwa Serikali haimchulii mtu hatua mpaka imepatikana ithibati kuwa anajihusisha na mambo ya ufisadi, Pili ninataka nieleze kuwa kwa taratibu za nchi yetu siyo dhambi mtu kumiliki mali ndiyo maana Serikali ya CCM inahimiza tupambane na umasikini, kinachogomba ndani ya Serikali ya CCM ni kujipatia mali zile kinyume cha utaratibu au kwa njia za kifisadi.

Kuhusu elimu aliyoisema kwa wananchi vyombo vipo, jeshi la polisi wana vipindi wanaelimisha jamii TAKUKURU wana vipindi na wana elimisha jamii na viko vyama vya hiari vina elimisha jamii kwa hiyo ninachotaka kusema kwa kifupi ni kwamba siyo dhambi mtu kumiliki mali ni dmabi mtu kumili mali uliyoipata kinyume cha Sheria, na ni dhambi kumiliki mali uliyopata kwa kufisidi.

Na. 236

Vifaa vya Uokoaji Wakati wa ajali

MHE. JUMA SURURU JUMA aliuliza:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa nchi yetu haina mpango madhubuti wala vifaa vya uhakika vya uokoaji wakati wa ajali za baharini au ziwani?

(b) Je, Serikali inawaambia nini Watanzania kuhusiana na hali hiyo ili kuwaondolea hofu.

WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bubu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mpango wa Taifa wa Utafutaji na Uokoaji katika usafiri na Majini (*National Aeronautical and Maritime Search and Rescue (AMSAR-Plan)* ambao uko katika hatua za mwisho kabla ya kuanza kutumika. Lengo kuu la mpango huu ni kutoa taratibu za kufuatwa katika utoaji wa huduma ya utafutaji na uokoaji pale inapotokea chombo cha anga au majini kupatwa na dharura, kupotea au ajali. Aidha, mpango umeainisha vifaa vinavyohitajika katika utafutaji na uokoaji.

(b) Mheshimiwa Spika, Ujumbe wa Serikali kwa Watanzania ni kuwa mpango wa utafutaji na uokoaji katika usafiri wa anga na majini umeandaliwa na pindi taratibu nyingine zitakapokamilika ikiwa ni pamoja na kupitishwa kwa Sheria husika mpango huu utaanza kutumika. Kwa sasa utaratibu uliopo ni kwamba kipindi cha dharura itokeapo mawasiliano hufanywa kupitia kituo cha uokoaji kilichopo Dar es salaam.

Kituo hiki huratibu uokoaji na utafutaji kwa kushirikisha Jeshi la Wananchi wa Tanznia *(Navy),* Kikosi maalum cha kuzuia majengo (KMKM), Kikosi cha Wanamaji cha Polisi na vyombo vya usafiri Majini vilivyo karibu na eneo la tukio ili kusaidia shughuli za uokoaji na utafutaji. Vikosi hivi vina vifaa vya uokoaji kama meli, boti wataalam wa kutafuta na kuokoa.

Aidha, meli na boti na wapiga mbizi binafsi hutumika. Kwa sasa Serikali haina chombo mahsusi kwa ajili ya utafutaji na uokoaji, hivyo utaratibu wa kutumia vyombo vilivyo karibu na tukio la ajali utaendelea hadi itakapopitishwa Sheria ya utafutaji na Uokoaji pamoja na Mpango wa Taifa wa utafutaji na Uokoaji ambapo utaratibu wa upatikanaji vifaa umeainishwa.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilitaka kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na mpango unaoandaliwa kwa ajili ya uokoaji ni lini mpango huu utakamilika ili upate kuletwa Bungeni?

La pili, amesema kuna vikosi vinasaidia kuokoa inapotokea maafa. Je, vikosi hivyo vimepewa mafunzo ya uokoaji?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa maandalizi haya siyo mepesi ni makubwa na ninaomba nimueleze kuwa Serikiali tayari ina kituo cha uratibu, utafutaji na uokoaji kilichopo Dar es salaam *Maritime, coordination Center* ambacho sasa hivi kina vifaa vya kisasa kabisa kama nchi nyingine zote zinazoendelea Duniani ambavyo vinaweza kuona kila chombo siyo katika bahari ya Hindi tu hata kwenye bahari zilizo mbali kabisa, tuna *automatic identification systems* na vilevile tuna *long range identification tracking of ships* na haya ndiyo maandalizi muhimu kabla hujaanza kutekeleza hiyo Sheria. Lakini ninaomba nimhakikishie kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha unaokuja 2013/2014 tutakuwa tayari tumeshaleta ndani ya Bunge hili hiyo Sheria.

Mbili, tumetaja hivi vikosi tumeeleza kama Navy, Polisi na KMKM hawa tayari vikosi vina ujuzi wa kutosha lakini suala la msingi hapa ilikuwa ni Sheria ambayo itafanya *coordination* ya uratibu pale linapotokea janga tuweze kupata chombo mahsusi cha kuweza kuhitikia haraka na kuweza kufanya wokozi, lakini suala la msingi la kuwa chombo cha *coordination* cha kuangalia kuona ni kitu gani kinatokea tumeshafanya kama Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari.

MHE.MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Spika, swali langu Mheshimiwa Waziri amelishalijibu wakati akijibu swali.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mangungu maana ni watu wa Rufiji.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, Chuo cha *Dar es salaam Marine Institute* walikuwa wameanzisha *program* ya kuwafundisha wavuvi wote katika Ukanda mzima wa Pwani kuanzia Mtwara hadi Tanga pamoja na Kilwa, *programme* ile imefikia wapi na kwa nini haiendelei ili kuwapa mbinu za uokoaji wakati majanga yanapotokea?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli Chuo cha *DMI* ni moja ya Vyuo vya mfano katika Bara la Afrika kinachotoa mafunzo kuhusu masuala yote ya bahari ninataka kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Chuo hicho hakijaacha *program* yake kinaendelea, hiki ni moja ya taasisi ambazo tunazifikiria kuwa central katika mpango mzima wa utafutaji na uokoaji.

SPIKA: Mheshimiwa Shah wa Baharini tena.

MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH: Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuwa na kituo maalum kama alivyotaja Mheshimiwa Waziri kipo pale Dar es salaam lakini kituo kile kimekuwa kinafanya kazi zaidi katika maeneo ya Ukanda wa Bahari ya Dar es salaam na Zanzibar pale inapotokea ajali.

Lakini kuna Ukanda huu wa Kusini kutokea Dar es salaam kwa maana ya bahari inayopakana na Wilaya ya Mkuranga, Rufiji, Mafia, Kilwa, Lindi na Mtwara kunakuwa na ajali za kila siku zinazotokea na watu wanapoteza maisha pamoja na mali zao. Lakini pale inapotolewa taarifa kwenda katika kile kituo huwa inatumia muda mrefu kuweza kufika.

Swali, ni kwa nini Serikali wakati tunasubiri mpango mzima huo aliouelezea Mheshimiwa Waziri kwa kutumia vikosi hivyohivyo vya ama jeshi la wana maji au Idara ya uokoaji na Zimamoto kuwa na kituo maalumu labda niseme tutafute eneo la kati kama Mafia au Kilwa ili linapotokea tatizo pale

baharini kuwe na wepesi wa kuwafikia wale waathirika kabla wengi hawajapoteza maisha yao.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Shah kama ifuatavyo:- Ninaomba nimhakikishie tena kuwa kituo tulichonacho Dar es salaam ni kituo cha kisasa chenye uwezo mkubwa kama vituo vingine vyote Duniani. Hakioni tu sehemu ya Dar es salaam tu, kinaona hata mbali kabisa hata *Red Sea* tunaweza kukuambia sasa hivi ni meli fulani sasa hivi inapita pale. Tuna mitambo ya kisasa kama nilivyosema *long range identification and tracking of ships system* iko pale ukitaka unaweza kwenda kuchungulia tumedhibiti bahari nzima. Tatizo letu sisi ni baada ya kudhibiti unatoa taarifa, una chombo gani cha kufika hapo kuweza kufanya uokoaji ndicho hicho ambacho tuna kihangaikia na Serikali.

Kwa hiyo, hatuwezi kufanya sasa hivi tunaenda kwa utaratibu kwa umakini na hiyo Sheria tutaileta hapa na Mheshimiwa Shah tutakupa uchangie kama Makao Maku yawe Mafia au yawe Pemba lakini tayari maeneo ya *Center* hii yanajulikana ni Dar es salaam na Zanzibar.

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linalofuata Mheshimi Capt. John Komba.

20 Mei, df 03

Na. 237

Elimu ya Hali ya Hewa

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA aliuliza:-

Elimu juu ya Hali ya Hewa ni muhimu sana kutolewa kwa wananchi wote ili waweze kujihami na hali mbaya ya hewa:-

(a) Je, kwa nini Mamlaka ya Hali ya Hewa hutangaza Hali ya Hewa ya Bahari na Ziwa moja tu la Victoria wakati kuna maziwa mengi nchini?

(b) Je, hii ina maana kuwa wananchi hawana umuhimu wa kujua hali ya hewa ya Maziwa mengine ya Nyasa, Tanganyika, Rukwa na kadhalika ili waweze kujihami?

WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, imekuwa ikitoa taarifa ya hali ya hewa kwa Ziwa Victoria kutokana na kuwa na mitambo yenye uwezo katika kituo cha hali ya hewa cha Mwanza. Aidha, katika vituo vya Dar es Salaam na Zanzibar mamlaka imefunga mitambo na vifaa vya hali ya hewa ambavyo vinaiwezesha mamlaka kutoa utabiri katika Bahari ya Hindi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwepo kwa taarifa za hali ya hewa katika Maziwa mengine, Serikali kwa kushirikiana na wafadhili mbalimbali imenunua mitambo na vifaa vya hali ya hewa ambavyo itawezesha mamlaka kutoa taarifa hizo.

Kwa sasa Mamlaka ya Hali ya Hewa ipo katika hatua za mwisho za kufunga mitambo na vifaa vya uchambuzi katika kituo cha Dar es Salaam. Kazi hiyo itakamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi ujao. Mtambo huo utaiwezesha *TMA* kutoa utabiri wa hali ya hewa katika maeneo ya Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Ziwa Rukwa. Aidha, *TMA* inahitaji shilingi bilioni 53.5 kwa ajili ya kutekeleza mpango wake wa miaka mitano ya uboreshaji wa huduma za hali ya hewa nchini. Kama fedha hizi zingekuwepo mara moja kwa kweli mamlaka ingeweza kuongeza vituo na vifaa na kuwa na uwezo wa kutoa kwa usahihi kabisa utabiri wa hali ya hewa nchi nzima.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, jibu hili bado sijaridhika nalo sana, kwa sababu maeneo hayo ambayo Maziwa yapo, Kwa mfano Nyasa, maeneo ya Songea, tunapata utabiri. Mvua itakuwaje kama kuna jua kali, ama mawingu. Sasa hivi vyombo vinatabiri nchi kavu ziwani ndiyo haviwezi kutabiri, au kuna tofauti gani kati ya vile vinavyotabiri ziwani na vile vinavyotabiri nchi kavu.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, tunachoongelea hapa ni taarifa zenye usahihi na siyo taarifa za ujumla. Ukitaka taarifa za ujumla tayari tunayo hiyo mitambo. Tunachosema ni kwamba tumenunua mitambo ya kisasa, ambayo itatoa utabiri wa uhakikika sasa ndani ya Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na hata ziwa Rukwa kwa usahihi kabisa na kuweza kuiruhusu sasa *TMA* kuingia mikataba na kampuni za simu *Vodacom* na *Tigo* kuweza kutoa utabiri huo uwafikie walengwa wakati huo huo.

MHE. ENG. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa swali la msingi linauliza elimu inayotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa ili kuweza kusaidia katika uokoaji janga linapotokea na majanga mengi yaliyotokea yanaonesha utabiri wa hali ya hewa hawakutoa taarifa zilizo sahihi kwa mfano *MV. Bukoba* tarehe 21 Mei, 1996 siku ya Jumanne.

Je, Serikali haioni ni busara kuweka kwenye mitaala kuelimisha Watanzania namna bora ya kupambana na majanga kwa sababu majanga mengi ni *no known risk,* zinafanywa kwa uzembe wa kibinadamu na wakati wakipelekwa mahakamani wanasema hapana walifanya kwa kutokukusudia?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nisahihishe kwamba ajali ya *MV. Bukoba* iliyotokea miaka 17 iliyopita haikutokana na kukosekana kwa utabiri wa hali ya hewa, kulikuwa na *factors* nyingi ambazo ziliainishwa katika taarifa, hizo *factors* ndiyo zilizotufanya Serikali tukae kwa muda wa zaidi ya miaka mitano kukaa chini kutengeneza sheria kali kabisa kuhusu usimamizi wa

vyombo vinavyokwenda majini. Ndiyo maana leo hii Tanzania hatuwezi kusajili chombo chochote kwa mara ya kwanza ambacho kina umri zaidi ya miaka 15 na kwa upande wa Bara tuna *Close Registry very restricted* ambayo bila Mtanzania kuwa na asilimia 51 ya hisa hatuwezi kusajili chombo hicho.

Kwa hiyo ninataka kumhakikishia tu kwamba kilichotokea *MV. Bukoba* haikuwa ni hali ya hewa. *TMA* ambayo imetambulika kimataifa kwamba ni taasisi ya Kitanzania inayofanyakazi yake vizuri sana, inatoa taarifa. Kinachotuletea matatizo hapa ni uwezo au chombo mahsusi cha Serikali ambacho kinaweza sasa kikatumia hizo taarifa na kufanya uokoaji.

Mheshimiwa Spika, huo utaratibu tumeshaanza kuufanyia kazi na tayari msingi wa kutosha tumeshauweka ambapo sasa hivi tuna chombo hicho cha Kimataifa cha ku-*identify* kuona meli gani inapita, chombo gani kimepata matatizo na kutoa taarifa. Tunachofanyia kazi sasa hivi baada ya taarifa je tutafikaje hapo kwenye tatizo. Hilo tutalileta ndani ya Bunge lako Tukufu na ninauhakika tutakuwa mahali pazuri tu. Ahsante sana.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na kujibu swali la nyongeza lililotangulia, ninapenda kujua Serikali ina mpango gani wa kuiopoa hiyo meli ya MV Bukoba?

SPIKA: Haya Waziri naomba majibu, miaka 17 iliyopita!

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, *priority* ya sasa kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaongeza meli mpya ndani ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na sasa hivi tupo kwenye mchakato wa kupata meli mbili mbili katika haya maziwa, vile vile kuweza kuimarisha uwezo wa Serikali katika uokoaji na utafutaji *research and rescue*, lakini kuwepo kwa ile meli ambayo ilishaharibika na ambayo ni kama kaburi lililozika Wtanzania wengi hapo chini na tulishalitamka namna hiyo, sioni udharura wake wa kuanza

kutumia mabilioni ya pesa kuanza kuiondoa, sasa tuipeleke wapi? Pengine Mbunge baadaye anishauri, tu tukishaitoa tuipeleke wapi.

SPIKA: Kama inaweza kutoka, tuende Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine.

Na. 238

Hali ya Gereza Wilayani Tarime

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE aliuliza:-

Gereza lililoko Wilayani Tarime lilijengwa enzi za ukoloni kwa lengo la kuhudumia watu wasiozidi mia moja (100) lakini sasa hivi idadi hiyo imeongezeka sana na kufanya hali ya gereza kuwa mbaya sana:-

(a) Je, ni lini Serikali italitatua tatizo hilo, ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za Watumishi?

(b) Je, ni lini Serikali itapanua gereza hilo pamoja na kununua gari la kuhudumia Mahabusu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kuboresha hali ya Magereza kwa awamu kwa kufanyia ukarabati, kujenga Magereza mapya na kukamilisha Magereza ambayo ujenzi wake haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kuboresha hali ya Magereza Nchini, Gereza la Tarime ni miongoni mwa Magereza yatakayofanyiwa ukarabati mwaka ujao wa fedha ambapo kukamilika kwakwe kutatoa pia nafasi ya ziada ya kulazwa wafungwa. Aidha, ujenzi wa nyumba za Askari pamoja na ukarabati wa nyumba zilizopo utaanza mwakani kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, hitaji la gari la kuhudumia mahabusu litatimizwa kwwenye Bajeti, kama Bajeti itakavyoruhusu.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika ahsante sana. Kusema ukweli sijaridhika na majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri, na kwa sababu Naibu Waziri alienda mpaka Tarime akaona hali halisi ilivyo, lile Gereza lina uwezo wa kuhudumia wafungwa wasiozidi mia mbili, lakini mpaka sasa hivi lina hudumia wafungwa mia tano mpaka mia sita. Naibu Waziri kwa kuwa ulifika, unawashauri nini?;

Swali la pili, naomba kauli ya Serikali kuhusu ujenzi wa gereza Wilayani Rorya kwa sababu kuna Wilaya mbili pale, Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Rorya. Wilaya ya Rorya haina gereza, wafungwa wote wanaotoka Rorya wanakuja Wilaya ya Tarime na wanajaza lile gereza la Tarime. Naomba kauli ya Serikali ni lini itajenga gereza Wilayani Rorya?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana nae kwamba kuna msongamano wa kutosha kwenye gereza hili na kama alivyosema inatokana pamoja na kuwa ni eneo lenye uhalifu mwingi Tarime pamoja na Rorya.

Lakini pia Rorya hakuna gereza mpaka leo, kwa hiyo kwa kuzingatia kwamba wahalifu lazima wahifadhiwe na bado hatuna mahali kule Rorya basi ni lazima kuwe na msongamano. Lakini Serikali inafanyia kazi ili kuhakikisha kwamba unapungua.

Swali la pili; aliuliza kwamba ni lini Rorya itapata Gereza, ninachoweza kumwambia ni kwamba Rorya haijapata Gereza na ni sehemu ambayo ina matatizo, ni moja kati ya Wilaya 43 ambazo bado hatujafanikiwa kujenga Gereza, jitihada tunazifanya kuhakikisha kwamba katika kipindi kifupi kiwezekanacho, kwa upendeleo wa Rorya kwa sababu maalum, basi magereza haya 43 pengine tutaanza na Rorya haraka iwezekanavyo.

SPIKA: Naomba tuendelee muda haunitoshi, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, atauliza swali hilo.

Na. 239

Mabadiliko ya Tabia Nchi na Mifugo

MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha jamii za Wafugaji zinapatiwa mifugo ambayo inahimili mabadiliko ya tabia nchi yanayosababisha hali ngumu ya hewa na magonjwa yanayoua mifugo.

NAIBU WAZIRI WA MENDELEO MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi Mbunge wa Maswa Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mabadiliko ya tabianchi yameleta changamoto nyingi zikiwemo mvua nyingi ama haba kuliko kawaida, ukame unaojirudia rudia na kusababisha vifo vya mifugo kama ule ulioua ng'ombe 250,900 mwaka 2006, na ule ulioua ng'ombe 403,849 mwaka 2009.

Aidha, madhara mengine ya mabadiliko ya tabianchi ni mvua inayoandamana na milipuko ya magonjwa kama vile homa ya Bonde la ufa ama *rift valley fever* iliyosababisha vifo vya ng'ombe 16,973, mbuzi 20,193 na kondoo 12,124 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, zaidi ya asilimia 98 ya mifugo yetu ni ya asili ikiwemo ng'ombe aina ya Tarime, Gogo, Singida, Iringa Pare, Sukuma, Fipa, Ankole, Chagga, Mbulu na Masai; mbuzi aina ya Ujiji, Gogo, Newala na Masai, na kondoo aina ya Masai red, Gogo na Tanzania *Black Head;* wenye uwezo wa kuhimili mazingira magumu yakiwemo ya upungufu wa malisho, magonjwa, ukame na uwezo wa kutembea umbali mrefu kufuata maji na malisho ikilinganishwa na mifugo ile ya kigeni.

Kinachotakiwa ni wafugaji kufuata kanuni za ufugaji bora, kuipatia mifugo yao maji na malisho ya kutosha, kuzalisha na kuhifadhi malisho, utunzaji na uendelezaji wa vyanzo vya maji, kujielimisha kuhusu mikakati ya kukabiliana na ukame huku wakidhibiti magonjwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuzalisha na kusambaza mifugo chotara kwa wananchi kwa lengo la kuboresha ng'ombe wa asili ili waweze kuzalisha wastani wa lita nane za maziwa, badala ya lita mbili kwa siku na kilo 500 za nyama kutoka kile 250.

Serikali inawashauri wafugaji kuendeleza mifugo yao ya asili kwa kutumia madume ya ng'ombe aina ya Mpwapwa na teknolojia ya uhamilishaji. Kwa kutumia madume bora na yenye sifa za kustahimili, wafugaji wataendeleza ufugaji wao huku wakimudu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa swali moja kwa Serikali.

Ili kuharakisha mikakati ya kukabiliana na tabianchi kwa wafugaji. Je, ni kwa nini Serikali isifanye utaratibu kama ule inaoufanya kwa Wakulima wa kutoa ruzuku kwa madume yaliyoboreshwa kama yale ya aina ya Mpwapwa?

NAIBU WAZIRI WA MENDELEO MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ushauri wake ni mzuri na mimi ninakubaliana naye kwamba kuna haja ya kufanya hivyo.

Tayari kumekuwepo na mapendekezo ya jambo hilo lifanyike maana ni moja kati ya mapendekezo na maombi tuliyoyapata kutoka kwa wadau wengi, mara tu Wizara ya Mifugo itakapokuwa imeingizwa katika vile vipaumbele vya *Big Results Now* bila shaka fedha zitapatikana za kutosha na hili litakuwa ni moja kati ya yale yatakayofanywa ili wafugaji waweze kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Wilaya ya Longido wameboresha mifugo kwa kuwa na mifugo bora zaidi aina ya Mpwapwa pamoja na *Ranch* aliyotaja Waziri. Je, Serikali haiwezi ikapeleka mbegu ya madume bora Shinyanga ili ng'ombe za Wasukuma nao wawe bora zaidi? (*Makofi*)

SPIKA: Haya, ili kusudi mfanane, Naibu Waziri majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MENDELEO MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na alichoshauri na kwamba Serikali inaweza na ina mikakati baada ya muda siyo mrefu sana madume aina ya Mpwapwa ama *Sahiwal* ambao wana uwezo wa ng'ombe kuwa na maziwa mengi na nyama ya kutosha kupeleka siyo usukumani tu lakini katika maeneo yote ya wafugaji, ili mifugo iweze kuwa bora izalishe nyama zaidi na izalishe maziwa zaidi. *(Makofi)*

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara inayofuata Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, atakayeuliza swali hilo ni Mheshimiwa Haji Khatib Kai, kwa niaba yake Mheshimiwa Kombo.

Na. 240

Ujenzi wa Bandari Micheweni

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO (K.n.y. MHE. HAJI KHATIB KAI) aliuliza:-

Jimbo la Micheweni ni moja ya maeneo yaliyopendekezwa kuwa na Bandari ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki:-

Je, ni lini Serikali zote mbili za Tanzania zitasimamia kuwepo kwa Bandari hiyo?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, kama lilivyoulizwa na Mheshimiwa Kombo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *program* na miradi inayotekelezwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki inazingatia viapumbele vya kikanda. Hivyo *program* au miradi husika hupitishwa na Jumuiya kwa kuzingatia vigezo vilivyokubaliwa pamoja na mchango wake katika Jumuiya na uwezekano wa kuchangiwa na Wabia wa Maendeleo na pia ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji huo.

Baada ya Nchi wanachama kuipitisha, mchakato wa kutafuta fedha za utekelezaji wa Miradi hiyo, miradi hiyo huanza.

Aidha, ulipaji wa gharama za utekelezaji wa miradi hiyo hufanywa na nchi mwanachama inayonufaika moja kwa moja kutokana na mradi huo.

Mheshimiwa Spika, miradi ya Zanzibar iliyopo katika vipaumbele vya Jumuiya hivi sasa ni ujenzi wa Bandari ya Maruhubi, ujenzi wa chelezo *(Dry Dock Construction)* na kivuko (*Roll on roll off-RORO)* kati ya Bandari ya Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba, Tanga na Mombasa.

Kulingana na vigezo vya Jumuiya, mradi wa Bandari ya Micheweni haumo katika orodha ya miradi ya kipaumbele. Ili mradi huu uweze kuingizwa katika orodha ya Miradi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, inabidi ufanyiwe upembuzi wa awali.

Kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Wizara ya Kisekta ya Serikali ya Mapinduzi ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu kufanyiwa upembuzi mradi huu ili kuona kama unakidhi vigezo vilivyowekwa na hivyo kuwezesha kuwasilishwa kwa mradi huu kwenye Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu itashirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuutetea Mradi huu mara baada ya kukamilisha maandalizi husika. *(Makofi)*

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, Ahsante sana. Baada ya majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa katika swali la msingi ni Micheweni kuwa na bandari, jambo ambalo liliamuliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Je, kwa nini lisipewe kipaumbele hasa ikizingatiwa kwamba, Micheweni ni mpakani baina ya Tanzania na Kenya na baadhi ya nchi nyingine?

Mheshimiwa Spika, la pili, je, upembuzi huo yakinifu utafanywa lini ili bandari hii iweze kujengwa?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi, kipengele cha mwisho kabisa, nilisema kwamba bandari ya Micheweni si miongoni mwa miradi ambayo imepewa kipaumbele katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Utaratibu wa bandari au mradi wowote kupewa kipaumbele katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni budi kwamba, mradi ule lazima upitishwe katika sehemu husika; wananchi wenyewe wanaidhinisha, unapelekwa katika Tume ya Mipango, halafu unathaminiwa pamoja katika vikao vya wataalam ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Tanzania kwa pamoja na baadaye ndiyo unapelekwa kwenye Sekretarieti ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nilipata bahati kwenda kule Zanzibar na nikakutana na Wizara ya Bandari na wakanidhihirishia kwamba, bandari ya Micheweni kwa hivi sasa siyo *priority* kwa ajili ya kupelekwa katika ule mradi wa Afrika Mashariki. *Priority* iliyopo ni bandari ya Chake Chake na Nimfumbuu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, upembuzi yakinifu ni jambo la lazima kufanywa na kwa tathmini ya mwanzo katika upembuzi yakinifu uliofanyika pale Micheweni, nilivyoambiwa na Wizara ya Bandari, ni kwamba, jiografia ya pale hairuhusu kujenga bandari, lakini kwa kutengeneza gati hilo linawezekana.

SPIKA: Tunaendelea, angalieni saa.

Na. 241

Utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa *MCC*

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA aliuliza:-

Utekelezaji wa mradi wa umeme wa *MCC* katika mikoa sita ukiwemo na Geita hasa katika Jimbo la Busanda umeanza muda mrefu na sasa ni mwaka wa pili tangu waanze kusimika nguzo:-

Je, ni lini sasa umeme utawaka?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GRORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi ya *MCC* katika Mkoa wa Geita inajumuisha Vijiji vya Buselesele, Katoro, Rwamugasa, Nyarugusu, Ikina, Bukoli, Bukondo, Nyang'hwale na Msalala. Kazi za mradi zinajumuisha ujenzi wa njia za umeme za misongo mbalimbali zenye urefu wa kilomita 338.97. Utekelezaji wa mradi katika maeneo haya, unaendelea na hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa njia za umeme zenye urefu wa kilomita 211.43 na ujenzi wa njia za umeme zenye urefu wa kilomita 127.54 unaendelea.

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme chini ya ufadhili wa *MCC* katika Mkoa wa Geita, hasa katika Jimbo la Busanda unatarajiwa kukamilika wakati wowote mwaka huu wa fedha na umeme kuwaka kipindi hicho.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika jibu la msingi, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, umeme utawaka wakati wowote katika mwaka huu wa fedha. Lakini

wananchi wangependa kujua mwaka huu ni lini? Kwa sababu tayari sasa hivi ni mwezi Mei na mwaka karibu unakwisha mwezi Juni umekaribia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika utekelezaji wa miradi hii ya *MCC* kuna huduma muhimu sana ambazo, umeme unapita yaani nguzo zinapita juu, lakini nguzo za kupeleka kwenye huduma hizi muhimu kama shule za sekondari, vituo vya afya na zahanati umeme haufiki. Ningependa kupata kauli ya Serikali, mnajipanga vipi kuhakikisha kwamba, vituo vya afya kama vile Bukoli, halafu pia shule za sekondari kama Chibunga na nyinginezo zinapata huduma hii ya umeme? *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu jibu la nyongeza na majibu yote yanayohusu miradi ya *MCC* kama ifuatavyo:-

MCC ilitupatia fedha karibu milioni 700 Dola za Marekani, ni 698.2 milioni, *MCC one.* Kwa ajili ya utendaji mzuri, walivyokwenda kufanya *evaluation,* maana yake zilikuwa nchi zaidi ya kumi, Tanzania na Morocco peke yake ndiyo tumebaki. Hii inamaanisha kwamba, mbali ya matatizo kwamba, kuna miradi inasuasua, lakini tumeweza kuridhisha Serikali ya Marekani na imeweza kutupatia mradi wa *MCC Compact Two.* Tumebaki wawili tu Tanzania na Morocco.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusoma hili swali leo asubuhi na vile vile huko nyuma nimeongea na Serikali ya Marekani na leo asubuhi nilikuwa naongea na Balozi wa Marekani. Amenithibitishia kwamba, miradi yote *MCC* inapaswa kuwa imekwisha Septemba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anayeuliza tarehe ya umeme kupatikana kufuatana na Serikali ya Marekani na sisi Wizara tunavyofuatilia ni Septemba mwaka huu na *MMC Compact Two* ambayo tumeipata kutokana na kwamba utendaji wetu umekuwa ni mzuri, maana yake huko nyuma ilichukua miezi kati ya 18 na miezi 24 kabla mradi haujaanza.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu sisi ni watendaji wazuri na tumedhihirisha hivyo, tunaongea na Serikali ya Marekani kwamba *MCC* ya pili ambayo ni umeme vijijini. Naomba nisisitize hili miradi yote *MCC,* lengo letu ni kupeleka umeme vijijini. Tutataka ianze haraka iwezekanavyo badala ya miezi 14, sasa tutapunguza na wiki ijayo, nitakaa na *MCC* ule uongozi umekuja kutoka Marekani, tuangalie namna ya *MCC* kuanza halafu na hii ya Septemba iishe haraka inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, majibu ya *MCC* na ucheleweshwaji ni hayo hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante kwa taarifa nzuri, tuendelee na swali linalofuata. Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa kwa niaba yake Mheshimiwa Jafo.

Na. 242

Mkakati wa Kupeleka Umeme Nyamisati

MHE. SELEMANI S. JAFO (K.n.y. ABDUL J. MAROMBWA) aliuliza:-

Mchakato wa kupeleka umeme Nyamisati umepitia katika ngazi zote hadi kumpata Mkandarasi:-

Je, utekelezaji wa mchakato huo utaanza lini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme Nyamisati unahusisha ujenzi wa njia kuu ya umeme umbali wa kilomita 40 kutoka Kijiji cha Bungu. Mkandarasi, *Ms Intercity*

Builders ndiye alishinda zabuni ya ufungaji umeme kutoka Bungu hadi Nyamisati. Mradi huu unagharimu jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 2.4.

Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo ni Mkandarasi kukamilisha upimaji wa njia ya umeme *(Line survey)* na kuwasilisha michoro *TANESCO* kwa ajili ya uhakiki. *TANESCO* imekwishawasiliana na uongozi wa Halmashauri ya Rufiji na tayari Mthamini Mali wa Serikali kwenye eneo itakapopita njia ya umeme amekwishapatikana. Hivi sasa malipo kwa ajili ya kazi hii yanafanyiwa kazi ili Mthamini aweze kulipwa na kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, kazi za kuchimba mashimo na kusimika nguzo zitaanza mara tu baada ya tathmini ya mali kwa maeneo yatakayoathirika wakati wa zoezi la kujenga njia ya umeme kukamilika. Aidha, *REA* na Mkandarasi wameshasaini *Letter of Credit* kwa ajili ya uingizaji wa vifaa mbalimbali vya mradi.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa mradi huu umelenga sana kuwasaidia wananchi walio kati ya Nyamisati na Bungu na kwa kuwa sehemu hiyo ina taasisi muhimu sana ikiwepo kama ile shule ya *WAMA* iliyojengwa na Taasisi ya *WAMA* ambayo ni muhimu sana kuwasaidia wasichana. Je, naomba nijue hasa ni lini *time frame* mradi huu hasa utaanza rasmi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nipende kuishukuru Wizara kwa kufanya mchakato mkubwa sana wa mradi wa umeme katika Jimbo la Kisarawe kutoka Mlandizi mpaka Mzenga na kutoka Kisarawe mjini kwenda Maneromango. Lakini hivi sasa Mkandarasi wa *Symbion* speed imekuwa ndogo na haturidhiki nayo. Nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha mradi huu unakwisha haraka iwezekanavyo ili mradi wananchi waweze kupata manufaa na kulinda miundombinu ile ya umeme iliyokuwepo pale Kisarawe?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, anauliza ni lini mradi ule wa *REA* utakamilika kutoka Nyamisati kwenda Bungu. Kilichotokea pale ni kwamba, fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi ule zilikuwa tayari na Mkandarasi alikuwa tayari, lakini wananchi wa maeneo yale ndiyo wanaokataa kupisha mradi, wakidai malipo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kusema mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, kusema kweli utekelezaji wa miradi kwa fedha za ndani hizi zinazopatikana kwa kodi za wananchi wetu, kubwa hapa iwe ni nia na dhamira ya Serikali katika kuwapatia wananchi umeme. Kama maeneo ambayo umeme unapita, wananchi wakiweka mgomo kwamba mpaka walipwe fidia, kwa hakika utekelezaji wa miradi hiyo utakuwa mgumu sana.

Mheshimiwa Spika, hapa nimpongeze sana Mheshimiwa Jafo. Yeye alifanikiwa kuwashawishi wananchi wa Kisarawe wakapisha mradi, ukatekelezwa na taratibu nyingine za fidia zinaendelea kuangaliwa. Nichukue nafasi hii kuwaomba wananchi wa Nyamisati na Bungu kwamba wangepisha mradi utekelezwe, kwa sababu fedha ipo halafu taratibu nyingine ziendelee.

Mheshimiwa Spika, ingawa fedha kwa kweli kama za kulipa fidia kwa miradi yote tunayosema nchi nzima, ambayo tunataka kutekeleza miradi ya bilioni kama 881, kwa *batch* hii ya *REA* inayokuja, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge sijui kama tutaweza. Lakini niseme tu kwamba, kwa wale wananchi au maeneo ambayo wataona watoe ushirikiano kwa Serikali kupisha miradi hii itekelezwe, wakifanya hivyo, watakuwa wameisaidia sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, ni suala la miradi inayotekelezwa na Kampuni ya *Symbion* hii ya *REA*. Ni kweli kumetokea ucheleweshaji, lakini tumejaribu kuongea nao, wamesema hadi ifikapo mwezi Juni, miradi hii itakuwa imekamilika.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumekula muda ambao siyo wa maswali. Kwa hiyo, naomba nitangaze matangazo ya kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie kwa Wajumbe wa Kamati yake kwamba, watakuwa na kikao leo saa saba na robo katika Ukumbi namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba na robo watakuwa na kikao katika Ukumbi namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba na robo watakuwa na kikao katika ukumbi wa Msekwa.

Pia tumepata taarifa kwamba Mheshimiwa David Kafulila, amefiwa na dada yake. Kwa hiyo, hatunaye hapa amekwenda kufanya maandalizi ya mazishi. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe mahali pema Peponi marehemu Salome. Ahsante. Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 – Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja ya kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Asasi zake katika mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mnaonipa unaoniwezesha kutekeleza kikamilifu majukumu niliyokabidhiwa ya kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Wajumbe wa Tume ya Katiba kwa kazi kubwa wanayoendelea kufanya ya kuratibu maoni ya wananchi kwa ajili ya kuunda Katiba Mpya. Aidha, naipongeza Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS)* kwa kuratibu kwa ufanisi mkubwa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2012 na hatimaye kuweza kupata idadi kamili ya watu katika nchi yetu. Naipongeza pia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuanza kutoa vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda Mbunge, kwa hotuba yake fasaha yenye maelezo ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 na mwelekeo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Saidi Mtanda. Pia nawapongeza wajumbe walioteuliwa kujiunga na Kamati hiyo. Ushauri wao ndio umefanikisha maandalizi ya hotuba hii. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwao.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki, hususan wananchi wa Jimbo la Chambani kwa kuondokewa na Mbunge wao Mheshimiwa

Salim Hemed Khamis *(CUF)* aliyefariki ghafla tarehe 27 Machi, 2013 alipokuwa anatekeleza majukumu ya uwakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutoa pole kwa Watanzania wenzangu waliopoteza ndugu zao kutokana na majanga na maradhi mbalimbali yakiwemo kuporomoka kwa jengo la ghorofa 16 Jijini Dar es Salaam, tukio la bomu na machimbo ya changarawe Mkoani Arusha, bila kumsahau mpendwa wetu msanii maarufu, marehemu Fatuma Binti Baraka (Bi Kidude) aliyefariki dunia tarehe 17 Aprili, 2013. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu matano, kama ifuatavyo:-

Eneo la kwanza, ni Utangulizi;

Eneo la pili, ni Majukumu ya Wizara;

SPIKA: Wale wanaotoka watoke kwa staha ndiyo Kanuni inavyotaka.

WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Eneo la nne, ni Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014; na

Eneo la tano, ni Hitimisho; lenye kujumuisha makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na maombi rasmi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera za Sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo;

(ii) Kuratibu na kusimamia masuala ya maendeleo ya vijana ili kuwawezesha kujiajiri, kuajirika na kujitegemea;

(iii) Kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali na kusimamia vyombo vya habari nchini;

(iv) Kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni nchini;

(v) Kuratibu na kusimamia maendeleo ya michezo nchini;

(vi) Kusimamia utendaji kazi wa Asasi, miradi na programu zilizo chini ya Wizara; na

(vii) Kuendeleza, kuwezesha na kuratibu masuala ya kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Kuhusu Mapato na Matumizi; katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya Sh. 714,209,000 kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Februari, 2013 jumla ya Sh. 655,447,097 zilikuwa zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 92 ya lengo la makusanyo ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, kadhalika Wizara ilitengewa jumla ya Sh. 16,210,999,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizo zilijumuisha mishahara ya Wizara Sh. 2,410,358,000 na ya Asasi Sh. 7,761,301,000, Matumizi Mengineyo *(OC)* ya Wizara Sh. 4,635,340,000 na ya Asasi Sh. 1,404,000,000. Hadi mwezi Februari, 2013 jumla ya Sh. 10,264,994,921 zilipokelewa na kutumika, kati ya fedha hizo Matumizi Mengineyo ni Sh. 3,947,748,471 na Mishahara ni Sh. 6,317,246,450.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo; katika

kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, Wizara ilitengewa jumla ya Sh. 3,096,600,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2013 Sh. 2,030,000,000 zilikuwa zimepokelewa na kutumika, sawa na asilimia 66.

Mheshimiwa Spika, Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na kuboresha uwanja wa Uhuru kwa kuujenga kwa umbo la *'U'* na hatimaye kuwezesha watazamaji 20,000 kukaa wawapo uwanjani hapo, Mradi wa Upanuzi na Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)*, kulipa sehemu ya deni la ununuzi wa majengo ya ofisi za Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na kuendelea kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa wazi unaojengwa na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Aidha, ukarabati wa nyumba za watumishi katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Sekta ya Habari ilikabiliana na changamoto mbalimbali katika mwaka wa fedha 2012/2013. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na baadhi ya vyombo vya habari kukiuka na kutozingatia maadili ya taaluma ya habari, kurusha matangazo ambayo yanakwenda kinyume na Sera, Sheria na Kanuni za Utangazaji.

Mheshimiwa Spika, changamoto zingine ni ufinyu wa fursa za masomo ya juu ya taaluma ya habari nchini na mazingira duni ya kazi kwa baadhi ya wafanyakazi katika tasnia ya habari. Aidha, pamoja na changamoto hizo Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiambia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu ilikuwa imewasilisha kwenye Baraza la Mawaziri, mapendekezo ya kutunga Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari nchini. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali tayari imeridhia kutungwa kwa sheria hiyo ya kusimamia vyombo vya habari. Kufuatia uamuzi huo wa Serikali Muswada wa kutunga sheria hiyo utawasilishwa hapa Bungeni baadaye mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Sheria ya Kusimamia Vyombo vya Habari kupitishwa na Bunge lako Tukufu, Wizara itaanza kuandaa waraka wa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Haki ya Kupata Habari. Kwa sasa Serikali inaendelea na utafiti ili kupata uzoefu kutoka nchi mbalimbali zenye sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kutungwa kwa sheria ya kusimamia vyombo vya habari kutasaidia sana katika kuimarisha tasnia ya habari hapa nchini na kupunguza kwa kiasi kikubwa baadhi ya changamoto nilizozieleza hapo juu ikiwemo suala la mafunzo kwa waandishi wa habari na mazingira duni ya kazi. Hivyo, ni matarajio yangu kuwa Muswada wa sheria hiyo utakapowasilishwa hapa Bungeni sote tutauunga mkono.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuratibu shughuli za Vitengo vya Habari kama ilivyoahidi katika bajeti iliyopita. Katika kuratibu shughuli hizo Wizara iliandaa kikao kazi cha mwaka cha Maafisa Mawasiliano wa Serikali kilichofanyika mjini Dodoma tarehe 4-9 Februari, 2013. Kikao hicho kilihudhuriwa na Maafisa Mawasiliano 139 wa Serikali kutoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kipindi hicho Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kupitia Ubalozi wake hapa nchini iliandaa mafunzo kwa Maafisa Mawasiliano wa Serikali kutoka Wizara, Taasisi za Umma, Wilaya na Mikoa. Mafunzo hayo yalilenga katika kuwajengea uwezo wa kutumia mitandao ya kijamii na mawasiliano kwa umma ambayo ndiyo mifumo ya mawasiliano inayotumika sana duniani kote hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Tovuti ya Wananchi iliendelea kufanya kazi ya kupokea maoni ya wananchi na kufuatilia majibu. Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi 2013, jumla ya hoja 15,875 zilipokelewa. Hoja 13,756 zilishughulikiwa kwa kupelekwa katika Wizara na Taasisi husika ili kupatiwa majibu na ufumbuzi. Hoja nyingi zilihusu fidia ya ardhi, mabadiliko ya

Katiba, kuhama kutoka mfumo wa utangazaji wa analoji kwenda dijiti na ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maudhui ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 12 ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanzishwa kwa sheria hiyo inayoifanya *TCRA* na Kamati ya Maudhui kuwajibika katika Wizara mbili tofauti, tumebaini kuna changamoto chache ambazo Wizara yangu na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia tunazifanyia kazi ili kurahisisha na kuimarisha usimamizi wa tasnia ya Utangazaji hapa nchini ambayo inazidi kukua siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/ 2013, Wizara kupitia Kamati ya Maudhui imeendelea kushughulikia malalamiko yanayowasilishwa na wananchi mbalimbali nchini kuhusu vituo vya utangazaji kukiuka kanuni za utangazaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kulialifu Bunge lako Tukufu kuwa mnamo tarehe 26 Februari, 2013, Kamati ya Maudhui ilivifungia kurusha matangazo kwa kipindi cha miezi sita kwa kosa la kutangaza habari za kichochezi, vituo vya redio Kwa Neema *FM* cha Mwanza na Imaan *FM* cha Morogoro. Vituo hivyo vilitakiwa pia kuithibitishia Kamati ya Maudhui kwa maandishi kuwa havitarudia tena kutenda kosa la aina hiyo na kama vitarudia, adhabu kali ya kuvifutia leseni za utangazaji itatolewa.

Mheshimiwa Spika, katika tarehe hiyo hiyo ya 26 Februari, 2013, Kamati ya Maudhui pia ilitoa onyo kali kwa kituo cha redio cha *Clouds FM* cha Jijini Dar es Salaam na kukitoza faini ya shilingi milioni tano kwa kukiuka kanuni za utangazaji. Serikali ililazimika kuchukua hatua hizi ili kudhibiti hali iliyoanza kujitokeza ya baadhi ya vyombo vya habari kutumika katika kuchochea udini na mfarakano ndani ya jamii yetu na hivyo kuhatarisha amani na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Uhamaji wa kutoka mfumo wa Analoji kwenda Dijiti. Mwitikio wa uhamaji wa kutoka katika mfumo wa utangazaji wa analoji kwenda dijiti umeonesha mafanikio makubwa kuanzia kipindi cha mpito mwaka 2010 mpaka Desemba, 2012. Aidha, zoezi la uzimaji wa mitambo ya televisheni ya analoji lililofanyika nchini mnamo tarehe 31 Desemba, 2012 lilifanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya Desemba 31, jumla ya Miji saba ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Moshi, Tanga, Mbeya na Dodoma ilikuwa inafikiwa na matangazo kwa njia ya mifumo ya aina zote mbili, yaani analoji na dijiti. Kwa sasa Miji saba ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Tanga, Arusha, Dodoma, Moshi na Mbeya tayari mfumo wa utangazaji wa analoji umeshazimwa na wananchi wanapokea matangazo kwa njia ya mfumo mpya wa dijiti.

Mheshimiwa Spika, aidha, zoezi la uzimaji huu wa mfumo wa utangazaji wa analoji utaendelea kwa awamu mpaka hapo maeneo yanayopata matangazo ya analoji nchi nzima yatakapokuwa yamefikiwa na matangazo kwa njia ya dijiti.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)*. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* liliendelea kuimarisha usikivu wa Redio na Televisheni ya Taifa ambapo, upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa kuhamishia mitambo ya Redio ya *FM* sehemu zenye miinuko katika vituo vya Songea na Morogoro ulifanyika. Mradi huo sasa upo kwenye hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, wananchi hivi sasa wanafuatilia shughuli za Bunge kutokana na Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* kurusha matangazo hayo moja kwa moja kutoka hapa Bungeni kupitia vituo vyake vya *Radio* na Televisheni licha ya changamoto mbalimbali zinazolikabili Shirika hilo. Huduma hii muhimu imewawezesha wananchi kujua kile wanachokisema wawakilishi wao Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kupitia fursa hii nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutumia chombo hiki kuwasiliana na wananchi wakiwa hapa Bungeni kwa lugha fasaha na sanifu.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuiongezea uwezo *TBC*, Wizara imekuwa na mazungumzo na nchi rafiki kuhusu uwezekano wa kusaidia jitihada za Serikali za kuimarisha *TBC*. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tkufu kuwa, Serikali ya Watu wa China imekubali kuipatia *TBC* gari la kurushia matangazo ya nje *(OB-van)*, msaada ambao utaiongezea uwezo wa kurusha matangazo yanayohusu matukio mbalimbali ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Uturuki nayo imekubali kuipatia *TBC* msaada wa vifaa mbalimbali zikiwemo kamera na kompyuta za kuhariri vipindi vya Televisheni. Aidha, Serikali ya Japan, kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa *(JICA)* imekubali kuipatia *TBC* wataalam wa masuala ya ufundi wa kujitolea ili kuwajengea uwezo mafundi wa *TBC*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Televisheni ya Taifa lililoko Mikocheni, Dar es Salaam ili liweze kutumika. Aidha, katika kuongeza ufanisi, Serikali imeridhia miundo mipya ya Utumishi ya *TBC* ambayo imeanza kutumika mwezi Julai, 2012, hatua ambayo imewaongezea ari ya kazi watumishi wa Shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya habari na mawasiliano, *TBC* imeingia makubaliano na Kampuni ya China, iitwayo *Star Communication Network Technology* na kuanzisha kampuni ya ubia iitwayo *Starmedia (T) Limited*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ubia huo matangazo ya TBC_1 yanapatikana kwa mfumo wa dijiti katika maeneo ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Mjini Magharibi, Morogoro, Mwanza, Pwani, Tanga, Kilimanjaro na Mbeya. Mpango wa kampuni hiyo ni kuongeza

mitambo ya dijiti katika mikoa mingine minane ndani ya mwaka wa fedha wa 2013/2014. Mikoa hiyo ni Iringa, Mara, Kagera, Lindi, Tabora, Singida, Ruvuma na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN)* imefikia makubaliano ya awali na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* ya kuendeleza kwa ubia kiwanja kilichopo Kitalu Na. 27, katika eneo la *Central Business Park* Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kuanza utekelezaji wa mradi huu yapo katika hatua za mwisho. Aidha, Kampuni imekamilisha andiko la mradi wa kutafuta fedha kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanda chake cha Uchapaji Magazeti ili kukiwezesha kuchapa kazi nyingi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta masoko mapya ya ndani ya nchi na Afrika Mashariki, *TSN* imeanza kufanya mazungumzo na mashirika mbalimbali ya ndege pamoja na kampuni za usafirishaji wa barabara ambapo magazeti ya kampuni yatasambazwa na kufika mapema katika mikoa na nchi jirani ambako kampuni hizo zinatoa huduma zake. Hii itawezesha magazeti yanayozalishwa na kampuni kuwafikia wasomaji na wananchi kwa ujumla mapema zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 ndio mwongozo pekee unaotakiwa kufuatwa na vyombo vya utangazaji nchini. Suala la matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili kwenye vituo vya televisheni na redio lina umuhimu mkubwa kwa vile ndiyo lugha ya Taifa inayotumika kwa Watanzania wengi. Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kusisitiza umuhimu wa vituo vyote vya utangazaji nchini kutumia Kiswahili sanifu kama Sera ya Habari na Utangazaji inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Sekta ya Maendeleo ya Vijana ina jukumu kuu la kuweka mazingira mazuri yanayowezesha kujenga uwezo wa vijana ili waweze

kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya Taifa kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kimsingi tunawatayarisha vijana, kwa kuwapatia stadi za maisha na stadi za kazi ili waweze kujitambua, kujitegemea, kujiajiri, kuajiri wengine na kuweza kuajirika. Hili tunalifanya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo Wizara na Idara za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Sekta hii ya Maendeleo ya Vijana, kwa kipindi cha mwaka 2012/2013, ilikumbana na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni upungufu wa Maafisa Vijana katika ngazi za Mikoa na Halmashauri za Wilaya; upungufu wa vyombo vya usafiri, maeneo ya vijana ya kufanyia kazi na kukosa maarifa ya biashara na ujasiriamali kwa wengi wa vijana ikiwa ni pamoja na wanaomaliza vyuo vikuu. Changamoto kubwa imekuwa ni kukosa fedha za mitaji na mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hii imetokana na kutokuwa na fedha za kutosha katika Mfuko wa Vijana za kuweza kutoa mikopo na mafunzo kwa vijana zaidi ya milioni kumi na sita nchini. Ukosefu wa maarifa ya biashara na ujasiriamali umesababisha vijana wengi kutokuwa na ubunifu na moyo wa kujituma.

Mheshimiwa Spika, katika hili Wizara imeendelea kufanya kazi kwa karibu kwa kushirikiana na TAMISEMI, Mikoa yote imeelekezwa kuajiri Maafisa Vijana. Mpaka sasa Mikoa 14 na Halmashauri 30 zimeajiri Maafisa Vijana. Mikoa hiyo ni Mwanza, Geita, Shinyanga, Mtwara, Dodoma, Kagera, Iringa, Manyara, Singida, Mbeya, Kigoma, Tabora, Rukwa na Dar es Salaam. Naipongeza Mikoa hiyo kwa dhati. Natoa wito kwa Mikoa na Halmashauri ambazo hazijaajiri Maafisa Vijana kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha vijana nchini wanapata maeneo kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi, Wizara yangu imewasiliana na wakuu wa mikoa yote kwa ajili ya kutenga maeneo hayo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, tayari mikoa minne imewasilisha Wizarani kwangu taarifa za kutenga maeneo hayo; Mikoa hiyo ni

Pwani, Dar es Salaam, Mbeya, Kagera, Katavi, Rukwa na Kilimanjaro. Natoa wito kwa mikoa ambayo haijatenga maeneo kufanya hivyo kwa manufaa ya maendeleo ya vijana wetu kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuwajengea vijana utaalam wa kijasiriamali, Wizara yangu inashirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* katika kutayarisha awamu ya pili ya Programu ya Kazi Nje Nje (KNN). Programu hii itahusisha Wilaya tatu katika kila Mkoa (Tanzania Bara na Zanzibar). Vijana wapatao 1,500,000 wanategemewa kufikiwa, kati ya hao vijana 45,000 wanatarajiwa kuanzisha miradi mipya ya biashara; kupitia mpango huu vijana wataweza kujiajiri na kuajiri wengine.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imefanya majadiliano ya kina na asasi mbalimbali za kifedha ili kuwawezesha vijana kupata mikopo rafiki. Kutokana na majadiliano hayo tumebaini fursa anuai kwa vijana za kuwawezesha kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzijengea uwezo *SACCOS* ambazo zilikopeshwa fedha kutoka katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa ajili ya kuwakopesha vijana katika Halmashauri zao. Wizara imetembelea *SACCOS* na vikundi vya vijana vilivyonufaika na mikopo hiyo katika Mikoa mbalimbali. Zoezi hili bado linaendelea na lengo ni kuhakikisha Mikoa yote inafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Sehemu ya Uhamasishaji na Uwezeshaji kwa vijana ikishirikiana na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini; imeendelea kuratibu na kufikia vikundi vya vijana na vijana mbalimbali kwa malengo ya kuwapatia stadi za maisha na kazi hasa maarifa ya ujasiriamali na biashara. Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2012 hadi Februari 2013, jumla ya vijana 8,743 wamepata mafunzo kutoka mikoa 23 na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa wanajishughulisha

katika uzalishaji na huduma kama vile kilimo, misitu, ufugaji, uvuvi, uchimbaji madini, elimu, afya na usafirishaji. Upatikanaji wa vijana wa kupatiwa mafunzo ni kwa kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa. Wizara inaendelea kushirikiana na *ILO* katika upatikanaji wa vijana hao. Mpango huu ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kutekeleza shughuli za maendeleo ya vijana hapa nchini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Taasisi ya *FORUM SYD*, Wizara ilitoa mafunzo ya ujasiriamali, ubunifu na uanzishaji wa miradi yenye tija, uongozi, uwajibikaji na stadi za maisha kwa vijana katika Wilaya za Magu, Ukerewe, Karagwe, Ilemela, Nyamagana, Kinondoni, Temeke na Ilala. Mafunzo yalitolewa pia kwa Watendaji kutoka Wilaya hizo juu ya majukumu na programu mbalimbali za maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Makete pamoja na taasisi ya *BALTON (TZ) Limited*, Wizara ilihamasisha na kuendesha mafunzo ya kilimo cha umwagiliaji kwa vikundi vya vijana wanaoshiriki katika miradi ya kilimo ili kuwapatia ujuzi wa kilimo cha kisasa kwa njia ya matone. Teknolojia hii itasambazwa kwa Mikoa mingine ili kuongeza fursa za ajira kwa vijana na uhakika wa chakula kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani *(UNFPA)*, Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Mafunzo ya Stadi za Maisha kwa Vijana Walio Nje ya Shule yenye lengo la kuwawezesha vijana kumudu changamoto mbalimbali za maisha kama vile maambukizi ya VVU na UKIMWI, mimba za utotoni, matumizi ya dawa za kulevya na ukosefu wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kupitia programu hii Wizara imekwishaandaa mwongozo sanifu wa kufundishia elimu ya stadi za maisha. Wizara imejipanga kutoa elimu hii kwa vijana

nchi nzima kwa njia ya elimu rika. Ili kutimiza azma hii mwezi Septemba, 2012, Wizara ilitangaza nafasi za waelimishaji wa Kitaifa wa stadi za maisha kupitia kwenye vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini. Wizara imepokea maombi 369 kutoka sehemu zote za Tanzania na taratibu za kuwapata waelimishaji wa stadi za maisha zinakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana; ili kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika shughuli za maendeleo yao, Wizara imeendelea na hatua mbalimbali za kuunda Baraza la Vijana Tanzania. Rasimu ya Waraka wa uundwaji wa Baraza la Vijana hivi sasa ipo katika ngazi za juu za maamuzi Serikalini. Rasimu hii imejadiliwa na kufanyiwa marekebisho mbalimbali katika ngazi ya vikao vya Makatibu Wakuu *(IMTC)*.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kuwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu, Muswada wa Sheria ya kuunda Baraza hilo baada ya Baraza la Mawaziri kupitisha Waraka huu. Mchakato wa kuunda Baraza la Vijana la Tanzania umechukua muda mrefu kutokana na umuhimu wa kuwashirikisha vijana na wadau wengine kutoa maoni na mawazo yao ili Baraza litakapoundwa likidhi matakwa ya vijana na jamii ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Vijana; Wizara pia imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Vijana. Nyaraka za maombi ya kuwasilisha andiko la mapendekezo ya kiufundi na fedha zimetolewa kwa wazabuni tisa walioonesha nia ya kutekeleza kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mbio za Mwenge wa Uhuru; Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ambao umekuwa ni kichocheo kikubwa cha shughuli za maendeleo, umoja, mshikamano na amani kwa Taifa letu. Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2012 zilizinduliwa katika Jiji la Mbeya, tarehe 11 Mei, 2012 ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, mbio hizi ziliambatana na ujumbe uliotumika kuwahamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika zoezi la sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, chini ya kaulimbiu isemayo: “Sensa ni msingi wa mipango ya maendeleo yetu; shiriki kuhesabiwa tarehe 26 Agosti, 2012”.

Mheshimiwa Spika, kupitia mbio hizo, wananchi na hasa vijana walihimizwa pia kushiriki katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kupambana na maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI, kuepuka matumizi ya dawa za kulevya na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, sherehe za kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru zilifanyika mjini Shinyanga tarehe 14 Oktoba, 2012 ambapo Mgeni Rasmi katika sherehe hizo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2012, jumla ya miradi ya maendeleo 289 yenye thamani ya sh. 158,837,117,855 ilizinduliwa na kuwekewa mawe ya msingi.

Mheshimiwa Spika, wiki ya vijana; sambamba na kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru, Wizara iliratibu maadhimisho ya Wiki ya Vijana kitaifa ambayo hufanyika kila mwaka kuanzia tarehe 8 – 14, Oktoba. Lengo la maadhimisho haya ni kuwapa vijana fursa ya kuonesha vipaji vyao, kazi za ubunifu pamoja na kujenga mtandao wa mahusiano.

Mheshimiwa Spika, vile vile ni kipindi ambacho Vijana hupata nafasi ili umma utambue na kuthamini michango mbalimbali inayotolewa na vijana katika shughuli za maendeleo katika ngazi ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika maadhimisho hayo vijana wajasiriamali 992 kutoka Mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Visiwani walishiriki katika maonesho ya kazi za ubunifu. Aidha, taasisi 59 zinazotoa huduma kwa vijana zilishiriki.

Mheshimiwa Spika, vile vile vijana walishiriki katika

midahalo ambapo walijadili mambo mbalimbali yanayogusa maisha yao ikiwemo vita dhidi ya rushwa, dawa za kulevya, tatizo la ajira, ujasiriamali, maambukizi ya VVU na UKIMWI, utawala bora, udumishaji wa amani nchini na jinsia. Washiriki wa Wiki ya Vijana walipata ushauri nasaha na kupima afya zao kwa hiari, ambapo watu 2,363 walipima na kati yao wanaume walikuwa 1,403 na wanawake walikuwa 960. Waliokutwa na maambukizi ya VVU walikuwa 40; kati ya hao wanawake ni 23 na wanaume ni 17.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni, ilikabiliana na changamoto kubwa ya kuendelea kumomonyoka kwa maadili, hasa miongoni mwa vijana kutokana na athari za utandawazi. Aidha, katika zoezi la kurasimisha tasnia za filamu na muziki, baadhi ya wadau hawakuwa na uelewa kamili wa sheria na kanuni za tasnia hizi na hivyo, kushindwa kutoa ushirikiano mzuri wakati wa mchakato wa kurasimisha tasnia za filamu na muziki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizi, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo katika mwaka wa fedha wa 2012/2013:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO),* Ofisi ya Kanda ya Dar es Salaam, iliendelea kutoa mafunzo kwa wadau ya kuwawezesha kuandaa mapendekezo ya elementi za urithi usioshikika kwa ajili ya kuorodheshwa kwenye urithi wa utamaduni wa Kimataifa unaotambuliwa na *UNESCO.* Maandalizi ya mapendekezo hayo yanafanyika sasa.

Mheshimiwa Spika, Vazi la Taifa; mintarafu Vazi la Taifa, Wizara imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri unaozingatia mapendekezo ya muonekano wa vitambaa vya kushonwa Vazi la Taifa yaliyokusanywa na Kamati ya Vazi la Taifa Kikanda kwa kuhusisha Mikoa yote na makundi maalum, wakiwemo wasanii, waandishi wa habari, vijana na wanawake. Waraka huu tayari umewasilishwa kwenye ngazi za juu za maamuzi Serikalini kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuleta mshikamano miongoni mwa watendaji wa Sekta ya Utamaduni, Wizara imekuwa ikiandaa, kusimamia na kuendesha Mikutano Mikuu ya Sekta ya Utamaduni kila mwaka kwa kuwashirikisha wadau na watendaji wa sekta hii, lengo likiwa ni kupokea, kujadili mustakabali wa utamaduni hapa nchini na kupitisha maazimio kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Katika mwaka huu wa fedha Mkutano Mkuu huo ulifanyika Jijini Dar-es-Salaam tarehe 19-22 Novemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikihimiza kuenzi na kutukuza utamaduni wetu kupitia fani mbalimbali za sanaa na lugha. Katika kutekeleza hilo, Wizara iliratibu na kusimamia vikundi vitatu vya ngoma za asili vya ndani na kimoja kutoka Rwanda, kushiriki katika maadhimisho ya miaka 51 ya Uhuru wa Tanzania Bara kwa ufanisi na ubora uliotukuka mnamo tarehe 9 Desemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara iliratibu na kusimamia ushiriki wa vikundi vya sanaa na wajasiriamali wa bidhaa za sanaa katika Tamasha la kwanza la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika Kigali, Rwanda, tarehe 11-16 Februari, 2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imefungua Ofisi ya muda ya Tawi la Tanzania la Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na imeendelea kukusanya kumbukumbu za mapambano ya kupigania uhuru nchini kutoka kwenye Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji kupitia Maofisa Utamaduni wa ngazi hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) lilitekeleza kazi muhimu zifuatazo:-

(i) Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya ‘Lugha ya Taifa’ kupitia *TBC* Taifa, vipindi 52 vya ‘Kumepambazuka’ kupitia *Radio One* na vipindi 52 vya ‘Ulimwengu wa Kiswahili’ kupitia Televisheni ya TBC_1;

(ii) Kupitia na kusoma jumla ya Miswada 24 ya vitabu na kuipatia ithibati ya lugha;

(iii) Kutoa huduma za tafsiri kwa asasi za Serikali, Mashirika ya Umma na ya Binafsi pamoja na kwa watu binafsi. Aidha, Baraza lilitoa huduma ya ukalimani kwenye Mkutano wa Mapinduzi ya Kijani katika Afrika Mjini Arusha mwezi Septemba, 2012, Mkutano wa Bunge la Afrika nchini Afrika Kusini mwezi Oktoba, 2012 na Januari, 2013 na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika nchini Ethiopia mwezi Julai, 2012;

(iv) Kufuatilia matumizi ya Kiswahili na kutoa ushauri kuhusu makosa mbalimbali yaliyofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine wa Kiswahili. Jumla ya makosa 90 yalishughulikiwa;

(v) Kufanya uchunguzi wa msamiati wa lahaja za Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu ambapo jumla ya maneno 650 yalikusanywa kwa ajili ya kuingizwa kwenye Kamusi Kuu ya Kiswahili sanifu; na

(vi) Katika kujiimarisha na kujitanua kiutendaji, Baraza limekarabati baadhi ya majengo yake kwa ajili ya kutumika kufundishia Kiswahili kwa wageni na maktaba ya Baraza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) lilitekeleza kazi zifuatazo:-

(1) Kuendesha midahalo 52 ya Jukwaa la Sanaa ambapo baadhi yake ilirushwa hewani kupitia Televisheni za *TBC$_1$*, *Star TV,* Mlimani *TV, Clouds TV* na *Radio* ya Wapo *FM*. Wadau wapatao 3,616 walihudhuria na kushiriki katika midahalo hiyo;

(2) Kukusanya taarifa 1,500 za wasanii na wadau wanaojishughulisha na sanaa ili kuziweka kwenye Tovuti ya BASATA *(www.basata.or.tz);*

(3) Kuendesha mafunzo ya utengenezaji wa batiki na uchapaji kwa wakufunzi katika Mkoa wa Singida na mafunzo ya uongozi katika sekta ya sanaa kwa viongozi 20 wa mashirikisho ya sanaa; na

(4) Kuendelea kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa wazi wa sanaa.

Mheshimiwa Spika, urasimishaji wa kazi za wasanii; katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuratibu na kusimamia urasimishaji wa tasnia za filamu na muziki kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Chama cha Hakimiliki na Hakishiriki Tanzania *(COSOTA)* na BASATA. Urasimishaji huo umeanza rasmi mwezi Januari, 2013. Aidha, katika kuhakikisha kwamba, suala hili linaeleweka vema na kuwanufaisha wadau na wananchi kwa jumla, Bodi imeendelea kutoa elimu kupitia vikao na wadau, vyombo vya habari, mabango makubwa na kwa kutumia madokezo madogo madogo redioni na katika televisheni. Ili kuhakikisha kwamba tasnia hizo zinaanza kuchangia pato la Taifa, utengenezaji wa stempu 5,000 za kodi za mwanzo za kubandika kwenye bidhaa za filamu na muziki umekamilika.

Maombi ya mahitaji ya stempu yamepokelewa na stempu zimeanza kutolewa. Asasi zinazosimamia mchakato huu, ambazo ni Bodi ya Filamu, *TRA, COSOTA* na BASATA, tayari zimeshaunganishwa kielektroniki ili kurahisisha na kuchapusha utendaji kazi wake;

(ii) Kupitia Miswada 124 ya filamu na kuipatia vibali. Aidha, jumla ya filamu 152 zilikaguliwa;

(iii) Kusimamia na kuratibu masuala ya filamu na michezo ya kuigiza kwa kushirikiana na Bodi za Mikoa na Wilaya, ikiwa ni pamoja na utoaji wa mafunzo ya kuboresha tasnia ya filamu kwa waongozaji wa filamu;

(iv) Kuendesha mafunzo kuhusu weledi katika tasnia ya filamu ambapo chama cha waongozaji wa filamu walipewa semina ya siku 10 kwa kushirikiana na wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(v) Bodi imeendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi na mafunzo kwa watumishi; na

(vi) Kushughulikia kutoa vibali 153 kati ya lengo la vibali 105 vinavyohusu maombi ya utengenezaji filamu. Kiwango hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 46 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kutoa mafunzo kwa wanachuo 161 waliohitimu na kutunukiwa stashahada na wanachuo 110 walipata mafunzo ya kozi fupi;

(b) Kudahili wanafunzi 14 na kutoa mafunzo ya cheti cha *National Technical Award (NTA);* na

(c) Kusimamia na kuendesha Tamasha la 31 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania ambapo vikundi 38 toka nchini na vikundi vinne toka nje ya nchi vilishiriki.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maendeleo ya michezo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa mara nyingine Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye ni mwanamichezo namba moja hapa nchini, amekubali kumlipia mshahara kocha wa kigeni wa mpira wa kikapu atakayefundisha timu ya Taifa ya mchezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Chama cha Mpira wa Kikapu nchini kinakamilisha taratibu za kuingia mkataba na kocha huyo. Uamuzi huu wa Mheshimiwa Rais unastahili

kupongezwa na kila mmoja wetu. Aidha, unaonesha dhahiri nia yake na nia ya Serikali anayoiongoza ya kuimarisha michezo yote hapa nchini kwa faida ya wananchi wetu wote.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ilikabiliana na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na upungufu wa wataalam katika fani mbalimbali za michezo; uwezo mdogo wa kumudu mahitaji ya sasa ya uongozi wa Vyama vya Michezo na ushirikishwaji na ushiriki mdogo wa jamii katika maendeleo ya michezo.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na changamoto hizo, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa mafunzo kwa wanachuo 38 katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya ambao wamehitimu mwezi Februari, 2013.

Mheshimiwa Spika, aidha, wadau wapatao 200 walishirikishwa katika kutoa maoni ya mifumo mbalimbali ya kuendeleza michezo kwa jamii kupitia mikutano iliyofanyika katika Vituo vya Michezo vya Arusha na Songea. Pia, mafunzo ya uongozi kwa vijana kupitia michezo yalitolewa kwa wanamichezo vijana 100.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia iliwezesha wataalam watano kuhudhuria mafunzo ya michezo kwa jamii huko India kama sehemu ya kujenga uwezo wa wataalam wa michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kukabiliana na changamoto za uendeshaji na usimamizi wa michezo nchini, Wizara yangu iliandaa na kuratibu vikao vya wadau mbalimbali wa michezo ili kukamilisha rasimu ya marekebisho ya Sera ya Maendeleo ya Michezo. Rasimu hiyo imewasilishwa ngazi za juu Serikalini kwa maamuzi baadaye mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, tumeamua kufanya marekebisho ya Sera hii kutokana na mabadiliko yaliyojitokeza katika tasnia ya michezo nchini na duniani katika miaka ya hivi karibuni. Lengo ni kuiwezesha tasnia ya michezo kuchangia pato la Taifa na kuongeza tija kwa wanamichezo.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeandaa rasimu ya waraka wa kuridhia Mkataba wa Udhibiti wa Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu za Kuongeza Nguvu katika Michezo. Serikali itawasilisha Azimio linalohusu Mkataba huu kwenye Bunge lako Tukufu baadaye mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliwezesha timu za Taifa za Michezo ya Riadha, Ngumi, Kuogelea na Paralimpiki kushiriki katika Michezo ya Olimpiki na Paralimpiki iliyofanyika Jijini *London* kati ya mwezi Julai hadi Septemba, 2012. Jumla ya wachezaji saba walishiriki michezo ya Olimpiki na mchezaji mmoja alishiriki michezo ya Paralimpiki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na michezo hiyo, Wizara iliratibu na kuwezesha mashindano ya Kanda ya Tano kwa mchezo wa mpira wa kikapu ambapo nchi saba za Afrika zilishiriki mashindano hayo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara iliratibu michezo ya Afrika Mashariki ijulikanayo kama *East Africa Cup* ambayo huwakutanisha vijana wapatao 3,000 kutoka nchi za Kenya, Zimbabwe, Malawi, Zambia, Sudan Kusini na nchi zote za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutafuta wafadhili wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuchangia na kusaidia maendeleo ya michezo nchini. Kwa sasa mazungumzo yanaendelea kati ya Wizara yangu na Chuo Kikuu cha *Clemson* cha Marekani na Chuo Kikuu kishiriki cha

Newmans cha Uingereza kwa ajili ya miradi ya pamoja katika maendeleo ya michezo, hususan katika kukiendeleza Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Malya na taaluma ya michezo kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia iliendelea kusajili Vyama na Vilabu vya Michezo hapa nchini. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, jumla ya Vilabu vya Michezo 60 na Vyama vya Michezo 45 vilisajiliwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, Baraza la Michezo la Taifa *(BMT)* lilitekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuendesha mafunzo ya utawala bora kwa viongozi wa Vyama na Mashirikisho ya Michezo ya Taifa kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika sekta ya michezo. Mafunzo haya yalitolewa kwa Mashirikisho na Vyama saba vya Michezo mbalimbali;

- Kuandaa mfumo rasmi wa wanawake kushiriki katika shughuli za michezo kama sehemu ya kuimarisha ushiriki wa wanawake katika michezo na uongozi kupitia michezo kwa kushirikiana na Baraza la Michezo la Uingereza *(UK Sport International)*. Jumla ya wanawake 18, wanashiriki mpango huu kwa ufadhili wa *Anita White Foundation* ya Uingereza;

- Kuandaa mifumo rasmi ya elimu na ithibati ya ufundishaji wa michezo, michezo shirikishi kwa jamii, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya michezo nchini na mfumo rasmi wa utambuzi na ukuzaji wa vipaji vya vijana katika michezo kwa kushirikiana na *UK Sport International* kupitia mradi wa kuhamasisha vijana kushiriki katika michezo kwa lengo la kuboresha maisha yao, ujulikanao kama *International Inspiration*; na

- Kuitisha na kuendesha mkutano wa siku mbili kwa Wenyeviti na Makatibu wa Kamati za Michezo za Mikoa yote Tanzania Bara kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika kuhamasisha Wananchi kushiriki kwenye shughuli za michezo katika maeneo wanayoyasimamia.

Mheshimiwa Spika, Utawala na Rasilimali Watu: Katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2012/2013, watumishi 37 wamehudhuria mafunzo katika taaluma mbalimbali. Kati ya watumishi hao, 28 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi na watumishi saba wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Vilevile, watumishi wawili wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imepangiwa watumishi wapya 33 kutoka Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ili kujaza nafasi wazi zilizokuwa na kibali. Hadi sasa, watumishi 26 wameripoti kazini na kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Idara ya Habari imekusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kuwa Msemaji Mkuu wa Serikali katika masuala ya kisera kama ilivyoainishwa katika Kanuni C 16 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009;

- Kuimarisha utendaji kazi wa Tovuti ya Wananchi na kupokea maoni ya Wananchi na kufuatilia maoni hayo;

- Kuratibu shughuli za Vitengo vya Habari vilivyomo katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi, Mamlaka na Wakala wa Serikali; na

- Kukusanya, kuandika na kuchapisha habari mbalimbali za kiserikali na maendeleo ya Wananchi likiwemo Gazeti la Nchi Yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* linakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kuandaa na kurusha vipindi bora na sahihi vya redio na televisheni kwa Wananchi;

- Kuhakikisha matangazo ya redio na televisheni yanaendelea kuwa hewani kila siku; na

- Kuimarisha usikivu kwa kufanya matengenezo ya mitambo ya redio na televisheni inapoharibika.

Mheshimiwa Spika katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN)* inakusudia kufanya yafuatayo:-

- Kuendelea na juhudi za kutafuta fedha za mradi wa upanuzi wa kiwanda cha uchapaji kwa kuendeleza mazungumzo yaliyofikiwa na Benki ya Rasilimali Tanzania;

- Kuendelea na juhudi za kukamilisha mkakati wa ubia wa kuendeleza viwanja vyake vilivyopo Dodoma na Dar es Salaam kwa kuendeleza makubaliano yaliyofikiwa na *TCRA* na *PPF*; na

- Kuendelea na juhudi za kuinua ubora wa magazeti yake na kuimarisha usambazaji hasa mikoani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara kupitia Sekta ya Maendeleo ya Vijana, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Vijana ya Taifa pamoja na kuboresha huduma ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuweza kutoa huduma ya mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana pamoja na kuendelea kuzijengea uwezo *SACCOS* zinazotoa huduma kwa vijana;

- Kuratibu na kusimamia shughuli za Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa lengo la kuhimiza umoja, amani, mshikamano na maendeleo miongoni mwa wananchi;

- Kukamilisha mchakato wa uanzishwaji wa Baraza la Vijana Tanzania;

- Kuendelea kutekeleza programu ya elimu ya stadi za maisha kwa vijana walio nje ya shule ili waweze kujitambua na kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali za maisha zinazowakabili; na

- Kushirikiana na Wadau wa Maendeleo na Halmashauri za Wilaya kutoa mafunzo kwa vijana kwa lengo la kuwajengea uwezo katika masuala ya ujasiriamali, kuanzisha miradi yenye tija, uongozi, uzalendo na matumizi bora ya Teknolojia ya Mawasiliano *(ICT).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2013/14, Wizara kupitia Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni itatekeleza yafuatayo:-

- Kufanya utafiti wa lugha za jamii kumi katika Mikoa ya Kagera na Manyara kwa lengo la kukuza na kuhifadhi sarufi na misamiati yake vikiwa ni vyanzo muhimu vya kupanua msamiati na istilahi za Lugha ya Taifa, yaani Kiswahili;

- Kusimamia Kamati Maalum ya Wadau wa Kiswahili inayoratibu na kuendesha mkakati wa kutumia fursa za ajira kwa Watanzania zitokanazo na kuundwa kwa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki itakayokuwa na Makao Makuu huko Zanzibar;

- Kuratibu uendeshaji wa Kituo cha Kufundisha Kiswahili cha Addis Ababa, Ethiopia;

- Kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuwa na Vazi la Taifa na matumizi yake; na

- Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Jumba la Utamaduni na Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2013/14, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuandaa na kurusha vipindi 52 vya Lugha ya Taifa kupitia Redio ya *TBC* Taifa, vipindi 52 vya Kumepambazuka kupitia *Radio One* na vipindi 52 vya Ulimwengu wa Kiswahili kupitia Televisheni ya TBC_1 ili kuimarisha matumizi ya Kiswahili sanifu nchini;

- Kuendelea kusoma Miswada ya vitabu vya taaluma na kuipatia ithibati ya lugha;

- Kuratibu na kutoa huduma za tafsiri na ukalimani katika Mikutano ya Kitaifa na Kimataifa, shughuli za mashirika, makampuni na watu binafsi;

- Kuendelea kuchunguza makosa ya Kiswahili yanayofanywa na vyombo vya habari na watumiaji wengine na kusambaza masahihisho yake;

- Kutunga Kamusi Kuu ya Kiswahili Sanifu ambayo itajumuisha msamiati wa kawaida pamoja na istilahi za maarifa ya nyanja mbalimbali; na

- Kuanzisha kozi fupi za ukalimani na tafsiri kwa ajili ya wahitaji maalumu pamoja na kozi za kuongeza maarifa kwa walimu wa kiswahili.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha

2013/14, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuendesha mafunzo ya utambaji wa hadithi na uchezaji ngoma za asili kwa watoto wa Mkoa wa Dar es Salaam;

- Kuendesha mafunzo maalumu kwa wasanii waongozaji, waandishi wa miswada ya tamthiliya, wataalamu wa urembo na mapambo, wabunifu wa maleba na wasanii waigizaji katika Mkoa wa Dar es Salaam;

- Kuendelea kuimarisha urasimishaji wa tasnia ya muziki;

- Kufanya utafiti kuhusu wasanii mahiri wa Kitanzania na kuweka taarifa zao katika kanzi data ya Baraza; na

- Kuendesha midahalo 52 ya sanaa kwa wasanii, waandishi wa habari na wadau wa sanaa 4,000.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/14, Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kukamilisha na kuendelea kuimarisha urasimishaji wa tasnia ya filamu na bidhaa zake;

- Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu urasimishaji wa tasnia za Filamu na Muziki kwa kutumia vikao, vyombo mbalimbali vya habari na fursa za Maadhimisho ya Kitaifa;

- Kupitia miswada 240 ya filamu, kukagua filamu 240 na kuziweka katika madaraja kwa kuzingatia maadili ya nchi yetu;

- Kutoa vibali 170 vya utengenezaji wa filamu kwa wadau wa ndani na nje ya nchi, kutoa leseni 10 za

uendeshaji wa kumbi za sinema, leseni za wasambazaji na watengenezaji wa filamu;

- Kukusanya takwimu za tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza;

- Kusimamia na kuratibu masuala ya filamu na michezo ya kuigiza;

- Kuendesha operesheni ya kukamata na kuteketeza filamu zisizokaguliwa na zisizowekewa stempu;

- Kufanya operesheni ya kuwabaini na kuwachukulia hatua wasambazaji, watengenezaji na wauzaji wa filamu wasiowasilisha filamu kwa ukaguzi na kuwekewa madaraja pamoja na kuyabaini na kuyadhibiti maeneo yanayoonesha filamu bila kufuata taratibu. Operesheni hii pia itahusu filamu zisizo na vibali na stampu;

- Kuratibu matamasha ya filamu yakiwemo Tamasha la Filamu za Bara la Asia na Ulaya;

- Kubuni mfumo wa kuziweka filamu katika viwango vya ubora ili kila filamu iweze kuingia sokoni na kutambulika kulingana na ubora wake. Aidha kupokea maoni ya wadau kuhusu kuwa na bei elekezi katika filamu ili kuondokana na unyonyaji unaowakumba wasanii; na

- Kuendelea kujengea uwezo vyama na vyombo vilivyoundwa na wadau wa filamu pamoja na kuendesha mafunzo kwa watengeneza filamu ili kuboresha mazao ya kazi za filamu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuendesha mafunzo ya stashahada kwa washiriki 200 na mafunzo ya muda mfupi kwa wasanii walio kazini 200;

- Kukamilisha mitaala ya shahada ya kwanza ya sanaa za maonesho na sanaa za ufundi na kuiwasilisha *NACTE* kwa madhumuni ya kupatiwa ithibati; na

- Kusimamia na kuendesha Tamasha la 32 la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maendeleo ya Michezo: Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali za michezo kwa walimu wa shule za msingi, sekondari, viongozi wa michezo na makocha 400 katika Vituo vya Michezo Kanda ya Kaskazini (Arusha) na Kanda ya Kusini (Songea);

- Kuendelea kutafuta maeneo mapya na kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya ushirikiano kati ya nchi marafiki na Tanzania katika Sekta ya Michezo.

- Kuendesha mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ufundishaji michezo na Stashahada ya Uongozi na Utawala wa Michezo kwa wanachuo 60 wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya;

- Kuwezesha Timu za Taifa kushiriki Michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika Glasgow, Scotland mwezi Agosti, 2014;

- Kuendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili ya Mradi wa Eneo Changamani la Michezo la Uwanja wa Taifa lililoko Jijini Dar es Salaam; na

- Kutoa huduma na mafunzo ya Kinga na Tiba kwa Viongozi wa Vilabu na Vyama vya Michezo, wanamichezo na wahudhuriaji kwenye viwanja vya michezo na Kufanya upimaji na kutoa elimu kwa wanamichezo kuhusu madhara ya matumizi ya dawa na mbinu haramu za kuongeza nguvu katika michezo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2013/14, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) litatekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuendelea kukamilisha mifumo rasmi ya elimu na ithibati ya ufundishaji wa michezo nchini, michezo shirikishi kwa jamii, ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya michezo nchini, pamoja na mfumo wa utambuzi na ukuzaji wa vipaji vya michezo miongoni mwa vijana kwa kushirikiana na wadau kupitia Mradi wa kuhamasisha vijana kushiriki katika michezo kwa lengo la kuboresha maisha yao, uitwao *International Inspiration*;

- Kuendelea kutoa mafunzo ya Utawala Bora katika Sekta ya Michezo kwa Vyama vya Michezo vya Taifa;

- Kuendelea kuimarisha ushirikiano na Serikali za Mitaa katika juhudi za kuleta maendeleo ya michezo kuanzia ngazi ya Vijiji kwa kutoa mafunzo ya awali ya ufundishwaji wa michezo kupitia mpango wa michezo kwa jamii; na

- Kuratibu chaguzi za Vyama vya Michezo ambavyo vitafanya uchaguzi wa Viongozi wao kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/14.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuwajengea uwezo watumishi wake 25 katika mafunzo mbalimbali. Aidha, ili kuendelea kupiga vita rushwa na kupunguza mmomonyoko wa maadili katika utumishi wa umma, Wizara itatoa mafunzo kwa watumishi 60 kuhusu namna ya kupambana na kuzuia rushwa pamoja na kujenga maadili mema;

- Kuendelea kutoa msaada wa chakula na lishe kwa watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI ambao wamejitokeza. Aidha, mafunzo kuhusu kujikinga na VVU na

UKIMWI yatatolewa sambamba na kuendesha Kampeni ya Ushauri Nasaha na Kupima VVU na UKIMWI kwa hiari;

- Kuimarisha Utawala Bora na ushirikishwaji watumishi sehemu za kazi kwa kuendesha Vikao vya Baraza la Wafanyakazi pamoja na vikao vingine vya kiutawala ili kuimarisha utendaji kazi; na

- Kuwapandisha vyeo watumishi wanaostahili kwa kuzingatia miundo ya kada zao, Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, toleo la mwaka 1999 na 2008 pamoja na Taarifa za Upimaji wa Wazi wa Utendaji Kazi (*OPRAS*).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendeleza mafanikio yaliyopatikana katika Sekta inazozisimamia ili ziweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. Hii ni pamoja na kuongeza ajira, kipato, kulinda mazingira, kuleta amani na furaha katika jamii. Pamoja na kutumia fursa hizo, bado kuna changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji zipatiwe ufumbuzi ili fursa hizo ziweze kutumika ipasavyo katika kuleta maendeleo ya nchi. Matarajio yangu ni kwamba, changamoto zilizopo zitaendelea kupatiwa ufumbuzi hatua kwa hatua hasa kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, naomba kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 katika kutimiza malengo yetu.

Mafanikio ya utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yamewezekana kutokana na ushirikiano uliopo miongoni mwa Viongozi na Watumishi wa Wizara na wadau wengine walio nje ya Wizara.

Shukrani zangu za pekee ziende kwa Mheshimiwa Amos Makalla, (Mb), Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ambaye amekuwa msaada mkubwa kwangu, Bw. Sethi Kamuhanda, Katibu Mkuu na

Bibi Sihaba Nkinga, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi, Wataalamu na Watumishi wote wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na Asasi zilizo chini ya Wizara kwa juhudi walizofanya kuhakikisha kwamba wanatimiza ipasavyo majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, nitumie fursa hii tena kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo ambao wametuunga mkono wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Shukrani hizi ziwaendee wahisani waliotusaidia nikitarajia kuwa wataendelea na moyo huo. Siyo rahisi kuwataja wote, lakini nitaje wachache ambao ni Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Finland, Uingereza, Denmark, Japan, Sweden, Norway, Iran, Cuba, Korea ya Kusini, Marekani na Ujerumani pamoja na Mashirika ya Kimataifa ya *UNESCO*, *UNICEF*, *UNFPA*, *IYF, UNDP, ILO, SYD, JAICA, RALEIGH INTERNATIONAL, VSO, AMREF na BRITISH COUNCIL.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuvishukuru vyombo vyote vya habari nchini ambavyo vimefanya kazi nzuri ya kuitangaza nchi yetu. Ninaamini kuwa, vyombo hivyo vitaendelea na kazi ya kuhabarisha, kuburudisha na kuelimisha umma kwa kuzingatia maadili na weledi. Aidha, ninamshukuru sana Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati, bila kuvisahau Vituo vya Televisheni ambavyo kwa namna ya pekee vinarusha hotuba hii hewani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 882,203,000 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara imetengewa bajeti ya Shilingi 20,728,045,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Matumizi Mengineyo na Mishahara), fedha hizo zinajumuisha:-

Mishahara ya Wizara - Shilingi 2,617,598,000; Mishahara ya Asasi - Shilingi 6,639,527,0000; Matumizi Mengineyo ya Wizara - Shilingi 8,041,920,000; na Matumizi Mengineyo ya Asasi - Shilingi 3,429,000,000.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara imetengewa jumla ya Shilingi 600,000,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 21,328,045,000; ambapo kati ya hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 20,728,045,000 na fedha za Miradi ya Maendeleo ni shilingi 600,000,000.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe tena shukurani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.hum.go.tz, www.mwananchi.go.tz* na *www.tanzaniangovernment.blogspot.com.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante. Hoja hii imeungwa mkono, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hiyo au mwakilishi wake. Naona amekuja Makamu, Mheshimiwa Said Mtanda!

MHE. SAIDI M. MTANDA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, nachukua fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge

ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2013/2014 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ilikutana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Jijini Dar es Salaam tarehe 26 Machi, 2013. Katika vikao hivyo, Kamati ilipokea na kujadili kwa kina Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ushauri wa Kamati umezingatiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ilipangiwa bajeti ya shilingi 19,307,599,000; kati ya fedha hizo, shilingi 10,171,659,000 inajumuisha mishahara na shilingi 6,039,340,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Shilingi 3,096,600,000 kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya Maendeleo.

Kati ya fedha hizo, shilingi 2,740,000,000 zilikuwa fedha za ndani na shilingi 356,600,000 zilikuwa ni fedha za nje. Hadi Kamati ilipokutana na Wizara mwezi Machi, 2013, fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi 11,758,067,082 ya fedha za ndani, sawa na asilimia 73 na shilingi 2,030,000,000 ya fedha za nje, sawa na asilimia 66.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali ikamilishe utoaji wa fedha hizi kwa kipindi kilichosalia ili Wizara iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 21,328,045,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya Fedha hizo, shilingi 9,257,125,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na shilingi 11,470,920,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC).*

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara imetengewa shilingi 600,000,000, zote zikiwa ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, pamoja na maombi ya fedha yanayojumuisha Makadilio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2013/2014, Kamati inatoa maoni na Ushauri ufuatao:-

Bajeti Ndogo inayotengwa kwa ajili ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Ukichukua taarifa za Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii, utaona kwamba, kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo, Kamati imekuwa ikiitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Wizara hii.

Pamoja na kwamba kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 bajeti iliyotengwa imeongezeka kutoka shilingi bilioni 19.3 hadi shilingi bilioni 21.3, bado kiasi hiki hakitoshi kutekeleza changamoto za kukabiliana tatizo kubwa la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kuwa, kila mwaka zaidi ya wahitimu 1,200,000 kutoka kwenye ngazi mbalimbali za taaluma wanaingia kwenye soko la ajira. Soko ambalo lina uwezo wa kuhudumia wahitimu 200,000 pekee. Kutokana na hali hiyo, vijana wanaomaliza elimu ya juu kutoka vyuo mbalimbali hapa nchini wamekuwa wakiaswa kuacha kutegemea ajira kutoka Serikalini na Mashirika mbalimbali na badala yake wajiajiri wenyewe na hatimaye wasababishe ajira kwa wengine ili kutendea kazi dhana ya kukuza ajira na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ndiyo yenye jukumu la kuandaa mazingira wezeshi ya kuwasaidia vijana kuweza kujiajiri wenyewe. Kiasi hiki kidogo kinachotengwa, hakitoshelezi mahitaji halisi yaliyopo. Pamoja na Serikali kutenga bajeti kidogo, Kamati inaitaka Wizara kuandaa mpango maalum wa makusudi wa kupunguza tatizo la ajira kwa vijana nchini. Kamati inaamini kuwepo kwa mpango wa makusudi wa kupunguza tatizo la vijana nchini kutapelekea Sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo itachochea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* ni Chombo cha Habari cha Umma kinachomiliki mitambo ya Redio na Televisioni iliyoko maeneo mbalimbali ya nchi. Moja ya majukumu ya kuanzishwa kwa Shirika hili ni kuhakikisha kuwa, matangazo ya Redio na Televisioni yanasikika nchi nzima na yanakuwa hewani kwa saa 24. Ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu yake, Shirika la Utangazaji Tanzania linahitaji kiasi cha shilingi bilioni 11.15.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha hizo kikipatikana, Shirika hili litaweza kuimarisha mitambo yake ya *studio*, *satellite, transmitters* na ya mtandao wa kompyuta, ambayo kwa sasa imechakaa na kusababisha usikivu wa matangazo kupungua na kushindwa kurusha *live* baadhi ya matukio ya kitaifa, picha za *video* kunata kwenye runinga na sauti kukwama mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeelezwa kuwa, matangazo ya Redio na *Television* yanayorushwa na *TBC* yanaweza kukatwa na kuzima muda wowote nchi nzima kutokana na Shirika kushindwa kulipia huduma ya kukodi mitambo ya *satellite segment* inayotolewa na Kampuni ya Marekani ya *INTELSAT* kupitia Shirika la Simu Tanzania *(TTCL).*

Mheshimiwa Spika, mbali na Shirika kushindwa kulipia huduma ya kukodi mitambo ya *satellite segment*, *TBC* pia inadaiwa na watoa huduma mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kiasi cha takribani shilingi bilioni tano.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, mapato ya Shirika yamekuwa yakishuka siku hadi siku, kwa sababu *TBC* inashindwa kujiendesha vizuri na hivyo kushindwa kuandaa vipindi vingi vinavyovutia wafanyabiashara kupeleka matangazo yao.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha na kushangaza kuwa, pamoja na Serikali kutambua matatizo yanayolikabili Shirika hili, hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendelao.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, kuna baadhi ya Wizara, Taasisi, Wakala na Idara za Serikali, ambazo zimekuwa zikihudumiwa na *TBC* kwa kurusha vipindi vyao kwenye Redio na Televisheni bila kulipia huduma hiyo. Kamati inawataka wadaiwa sugu wa *TBC* kuhakikisha wanalipa madeni yote wanayodaiwa na Shirika hili katika Mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA),* ambacho ni Chombo cha Serikali, umeonesha kwamba hakuna Shirika la Utangazaji la Umma Ulimwenguni linalojiendesha lenyewe bila kupata ruzuku kutoka Serikalini. Kamati inaitaka Serikali kutambua umuhimu wa shughuli zinazofanywa na *TBC* na kuendelea kuipa *TBC* ruzuku ya kutosha. Vilevile, Kamati inaitaka Serikali itakapokuwa inahitimisha hotuba ya bajeti ya Wizara hii, iliarifu Bunge lako Tukufu kiasi cha fedha za Miradi ya Maendeleo kilichotengwa kwa ajili ya Shirika la Utangazaji Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba, iwapo Serikali itaitengea *TBC* bajeti ya kutosha, Shirika hili litaweza kujitegemea kwani hadhira itaongezeka na *TBC* itaaminika na hatimaye kuboresha matangazo na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, lugha ni sehemu ya Utamaduni wa Taifa na hivyo ni kiungo muhimu katika kuwaunganisha watu wa taifa moja. Katika kutambua hilo, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliundwa kwa Sheria ya Bunge Namba 27 ya

1967, ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 1984. Lengo la Baraza hili ni kukuza na kuendeleza Lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Sheria iliyoanzisha BAKITA, pamoja na mafanikio iliyoyapata bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zifuatazo:-

- Sheria hii haielezi bayana maeneo ya usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Lugha Kiswahili;

- Sheria haiipi BAKITA mamlaka ya kusajili na kutoza ada vyama na vyombo mbalimbali vya kuendeleza Kiswahili; na

- BAKITA haina mamlaka ya kutoa adhabu yoyote kwa ukiukwaji wa matumizi mabaya ya Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa marekebisho ya Sera ya Utamaduni ili marekebisho hayo yafanyike sambamba na Sheria iliyoanzisha Baraza la Kiswahili Tanzania. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha itakayosaidia pamoja na majukumu mengine, BAKITA kuweza kutekeleza Maazimio yaliyomo kwenye Kamisheni ya Kiswahili kwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo Tanzania imeridhia.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ni Shirika la Umma lililoundwa kwa Sheria ya Bunge Namba 23 ya mwaka 1984. Baraza ni Chombo cha Serikali cha dhima ya kuhuisha, kukuza na kuendeleza sanaa. Moja ya majukumu ya Baraza la Sanaa la Taifa ni kuhuisha na kuhimiza maendeleo ya uzalishaji wa kazi za wasanii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba, jukumu hilo la BASATA likitekelezwa kikamilifu, litasidia tasnia ya sanaa kuvutia vijana wengi na kuwapatia ajira kupitia kazi za sanaa na hivyo kukuza pato la mtu mmoja mmoja na Taifa na hatimaye kuimarika kwa uchumi. Hata hivyo, kutokana na

usimamizi hafifu wa kazi za sanaa ya muziki, mapato yanayopatikana ni asilimia 12 tu ya kiwango ambacho kingepaswa kukusanywa kutoka katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, usimamizi huu hafifu wa kazi za Wasanii na mapato yake hauko katika tasnia ya Muziki pekee, unajitokeza pia katika maeneo mengine kama vile sanaa za michezo ya kuigiza, filamu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa, udhaifu huo umetoa mwanya kwa maharamia wa kazi za wasanii kuendelea kujinufaisha isivyo halali, unachangiwa na upungufu uliomo kwenye Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuitikia wito uliotolewa na Kamati wa kutaka Sheria hiyo ifanyiwe marekebisho. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, Serikali iharakishe ukamilishwaji wa mchakato huo ili kuwakomboa Wasanii dhidi ya uharamia unaofanywa na watu wanaotaka kutajirika kupitia kazi zinazofanywa na Wasanii.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inatambua na kupongeza hatua ambazo zimechukuliwa hadi sasa na Serikali katika kulinda Hakimili na Hakishiriki za kazi za Wasanii. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na Mpango wa kuanzisha mtandao wa kielektroniki *(Electronic Network System)* ambao utaunganisha Wadau, Wizara na Taasisi zote zinazosimamia tasnia za filamu na muziki unaendela kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ndicho chombo chenye dhamana kisheria kuhamasisha Wananchi wa ngazi zote wapende na kujihusisha na michezo. Chombo hiki pia kinapaswa kuendeleza na kusimamia vyama vya aina zote za michezo ya ridhaa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu hayo, Chombo hiki kimekuwa kikitengewa bajeti finyu ambayo inapelekea kiendelee kukabiliwa na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:-

- Ukosefu wa ofisi zenye ubora unaolingana na hadhi ya Chombo hiki. Kwa sasa Ofisi za Baraza zipo katika majengo ya zamani ambayo ni mabovu; na

- Ukosefu wa fedha kwa ajili ya maandalizi ya timu zinazopata fursa ya kuiwakilisha nchi katika Mashindano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Baraza la Michezo Tanzania kukabiliana na changamoto hizi, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

- Serikali itenge bajeti ya kutosha itakayowezesha BMT kukamilisha ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo, ambalo litakapokamilika litaiwezesha Baraza la Michezo kupata ofisi za kisasa.

- Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuhudumia Timu za Taifa za michezo mbalimbali zinapopata fursa ya kuiwakilisha nchi katika Michezo ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Tanzania ulianzishwa mwaka 1993 kwa lengo la kutoa mikopo midogo yenye gharama nafuu, itakayowawezesha vijana kujiajiri wenyewe. Suala la kuwawezesha vijana kujiajiri kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni changamoto kubwa inayolikabili Taifa kwa sasa na hii ni kutokana na ukweli kwamba, Vijana ndiyo nguzo na nguvu kazi ya Taifa na ukweli kwamba, vijana ndiyo kundi kubwa katika jamii. Tatizo kubwa katika kuwawezesha vijana ni ukosefu wa rasilimali fedha ambayo ingetumika kutoa mikopo, mafunzo ya ujasiriamali na ufuatiliaji wa shughuli za vijana nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuwaendeleza vijana, kwani Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Serikali imetenga shilingi 3,100,000,000, zitawawezesha vijana wengi kujiajiri kwa kubuni na kuanzisha miradi ya uzalishaji mali. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaamini fedha hizi ni kidogo ukilinganisha na idadi kubwa ya vijana ambao hawana ajira. Kamati inaishauri

Serikali kuona uwezekano wa kuongeza fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira kwa vijana ni suala mtambuka ambalo linahitaji kuhusisha wadau wengine hususan sekta binafsi. Serikali imekuwa ikishirikiana na Benki za *CRDB* na *NMB* katika kushughulikia tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Benki ya *CRDB* imeanzisha Mpango unaolenga kuwakopesha Vijana waliomaliza Vyuo Vikuu na kwa kuanza Benki hii imeanza kushirikisha Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA)* hususan kwa Vijana waliomaliza Elimu ya Chuo kwa wahitimu wa fani ya Sayansi kwa dhamana ya cheti. Katika mkakati huu, Benki ya *CRDB* inatambua kuwa ili vijana waweze kuajirika na kutengeneza ajira nchini ni vyema wapatiwe elimu ya stadi ya ujasiriamali itakayowasaidia vijana kufahamu namna bora ya kuendesha biashara zao.

Kamati inaipongeza Benki ya *CRDB* kwa kuanzisha utaratibu wa kuwakopesha wahitimu wa Vyuo Vikuu ambao baada ya kukopeshwa hurudi vijijini ili kuendeleza shughuli za kilimo na ufugaji.

Kamati inaamini hatua itasaidia kupunguza tatizo la ajira na hasa kwa vijana wanaokimbilia mijini kutafuta kazi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali ishirikiane na Benki ya *CRDB* kwa kuongeza huduma hii kwa Vyuo vingine hasa Vyuo vya Elimu ya Ufundi Stadi *(VETA),* ambavyo hufundisha asilimia kubwa ya vijana wanaohitimu Elimu ya Msingi na Sekondari. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuingiza elimu ya ujasiriamali katika mitaala ya elimu ya sekondari na vyuo vya ualimu, kwa lengo la kuwawezesha vijana kuhitimu wakiwa na elimu hiyo, jambo ambalo litawasaidia kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Benki ya *NMB* imekuwa ikishiriki pia kusaidia kuondoa tatizo la ajira kwa vijana hapa nchini. Benki ya *NMB* imeanzisha Mfumo wa *"Chap Chap,"* ambao unalenga kuwasaidia vijana wanaotaka kukopeshwa "Bajaji" kwa kuchangia asilimia 30. Baada ya kuchangia kiasi hicho,

benki hutoa mkopo wenye thamani ya bajaji ambapo mkopaji atalazimika kurejesha mkopo huo ndani ya miezi ishirini na nne, yaani miaka miwili. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuandaa mazingira wezeshi yatakayosaidia vijana wengi kupata mkopo kutoka Benki ya *NMB* kwa kuboresha mfumo huu ili Benki ya *NMB* iweze kuwafikia vijana wengi zaidi hata ambao hawajishughulishi na shughuli za kuendesha bajaji. Hatua hii itasaidia vijana waliokopa katika mikoa mbalimbali kuweza kuanzisha miradi mingine kama ufugaji, kilimo, ushonaji na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kutumia hati za kimila ambazo zitawawezesha vijana kutumia hati hizo kama dhamana ya kupata mikopo kwenye benki mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kwa mara nyingine tena, kukupongeza kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa jinsi wanavyokusaidia kuendesha Vikao vya Bunge. Kwa niaba ya Kamati, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha Maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara (Mb) - Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Naibu Waziri - Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla (Mb); Katibu Mkuu - Ndugu Sethi Kamuhanda; Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Sihaba Nkinga na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa waliotuonesha wakati tunatekeleza shughuli za Kamati. Ninawashukuru na kuwatakia mafanikio zaidi katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Naomba *Hansard* inukuu Orodha ya majina ya Wajumbe wa Kamati hii wakiongozwa na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Kiongozi mahiri wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii ni wafuatao:-

Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama - Mwenyekiti, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Capt. John Damian Komba, Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omary, Mheshimiwa Salvatory Naluyanga Machemli, Mheshimiwa Jaddy Simai Daddy, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo na Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, akisaidiwa na Katibu wa Kamati, Ndugu Happiness Ndalu, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, naomba nitambue uwepo Bungeni wa Wasanii Maarufu, akiwemo dada yangu *Lady JD, Prof. J*, Mkoloni na kundi lote la Vinega; karibuni sana. *(Makofi)*

Pili, nitaomba Hotuba yangu iingie yote kwenye

Hansard kama ilivyo kwenye kitabu, kwa sababu hapa ninasoma *extract* tu.

KUHUSU UTARATIBU

SPIKA: Mheshimiwa Sugu, naomba ukae kidogo, sijui Sugu sijui nani. Mheshimiwa Mbilinyi. *(Kicheko)*

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, ninatumia Kifungu cha 68(1) kuhusu utaratibu, lakini nakwenda kwenye Kanuni ya 64(a) inayosema; Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Spika, msomaji anayeendelea katika taarifa yake, ukitoka ukurasa wa kwanza ule mpaka wa 14, mambo yanayozungumzwa ni ya uchochezi mkubwa kweli kweli. Ukurasa wa pili, kuhakikisha kwamba ni ya uchochezi, anasema; Tanzania imegeuka chini ya usimamizi wa Wizara na Serikali hii ya CCM kuwa Taifa linaloteka nyara wanahabari, kuwatesa kwa kuwang'oa kucha na meno, kuwatoboa macho na kuwamwagia tindikali na hata kuwaua.

Mheshimiwa Spika, hii ni kauli nzito sana kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ambayo hakuna mtu anayeweza akainyamazia aone Mbunge anaendelea kusoma taarifa na Watanzania wanasikiliza. Atueleze wapi ambapo Serikali ya Chama cha Mapinduzi kimewang'oa kucha waandishi wa habari, kimewatoboa macho, kimewamwagia tindikali na kuwaua?

Mheshimiwa Spika, taarifa kama hizi tusiruhusu zije ndani ya Bunge, ambapo tunawapotosha Watanzania kuwaaminisha kwamba, Serikali hii inafanya jambo baya.

Mheshimiwa Spika, ninashauri na ninaomba nitoe hoja, taarifa hii ukurasa wa kwanza mpaka wa 14 isitishwe ili ikaandikwe upya isomwe kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Naomba mkae wote.

Juzi, sisi wenyewe ndani ya Bunge hili, tumepitisha Azimio la kutokuhusisha uchochezi ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasitisha Kikao cha Bunge, mpaka saa 11.00 jioni, Kamati ya Kanuni ikakae na ipitie Hotuba hii. *(Makofi)*

Nasitisha Kikao cha Bunge, Kamati ya Kanuni tukutane kule. *(Makofi)*

(Saa 5.35 asubuhi Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kuwa, nilipositisha Shughuli za Bunge kabla ya saa saba mchana, nilifanya hivyo baada ya Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashairiki, kusimama na kuomba kuhusu utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1) na Kanuni ya

64(1)(a), ambapo alitilia shaka lugha iliyotumika kuanzia ukurasa wa kwanza hadi ukurasa wa 14 wa Hotuba ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa madhumuni ya kuheshimu uendeshaji bora wa shughuli za Bunge na kuzingatia vyema misingi ya Kanuni za Bunge, niilitisha Kikao cha Kamati ya Kanuni za Bunge na kufanya majadiliano kuhusu jambo hili.

Kamati hiyo ilipitia kwa kina maelezo yaliyopo katika kurasa hizo na kuzingatia mambo ya msingi kama vile dhana ya kutokuingiliana baina ya Mhimili wa Bunge na Mahakama. Pamoja na umuhimu wa kuepuka lugha za uchochezi. Aidha, Kamati ilizingatia umuhimu wa kutojadili jambo bila kuwa na ushahidi wa kutosha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 72, ni Mamlaka ya Spika, kusimamia utaratibu wa majadiliano. Vilevile, Kanuni zetu zimetoa mwongozo juu ya mambo yasiyoruhusiwa Bungeni.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(c), nimeelekeza kuwa maneno yote katika Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, yanayozungumzia mauwaji ya David Mwangosi, yaondolewe kwa sababu yanahusu suala ambalo liko Mahakamani.

Vilevile, kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(g), nimeelekeza kuwa maneno yote yaliyosemwa katika ukurasa wa kwanza mpaka wa 14 yaondolewe, kwa sababu yanaudhi, yanawadhalilisha watu wengine, waliotajwa katika hotuba hiyo. Aidha, nimeelekeza maneno yote yenye maudhi kama hayo katika hotuba hiyo yaondolewe. *(Makofi)*

Jambo kubwa hapa, nataka tuelewe kwamba, Bunge siyo sehemu ya kugombanisha Wananchi na Serikali

yao, bali ni Taasisi inayosimamia Serikali na hivyo hivyo ni wajibu wa Bunge kuhakikisha kwamba, amani ya nchi inalindwa na ni vizuri ukawa ni mwanzo wa kujenga amani katika nchi yetu. Hivyo, maneno yote yenye viashiria vya kuwachochea au kuwatia hasira Wananchi kama ilivyo katika ukurasa wa kwanza mpaka wa 14 wa Hotuba hiyo hayatakubalika.

Huu ni uamuzi wangu ambao umekwishatolewa. Sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani aendelee na Hotuba yake kwa maelekezo hayo. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwanza, ninaomba kuanzia leo kwa ridhaa yako, nikiombe Kiti kiache kutumia jina la Sugu, kitumie Joseph Mbilinyi, kwa sababu nimeona kuna *element* za ku-*abuse* matumizi ya hilo jina ambalo ni *Trade Name* yangu na nimetumia kwa muda mrefu**.**

SPIKA: Ninakubaliana na wewe. Kwanza, sikujua kama ni Sugu au Sugula. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, VIJANA UTAMADUNI NA MICHEZO: Mbeya wanajua.

SPIKA: Haya.

(Hapa Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo haikuwa recorded)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Jenista Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya, lakini pia atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Nkamia.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Mwongozo kuhusu nini?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, hivi punde kabla Msemaji wa Kambi ya Upinzani hajaanza kuwasilisha, umetoa maelekezo kufuatia suala la kiutaratibu ambalo nililiomba asubuhi, na kimsingi umeelekeza kwamba yale mambo yote yanayohusiana na masuala ya mauaji ya Mwangosi liondolewe kwa sababu ni suala ambalo lipo Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, lakini nilichoshangaa ni kwamba yale yote ambayo umeelekeza yaondolewe, hayakuondolewa na wewe umeliacha liendelee. Sasa nimeshindwa kuelewa ni jambo gani ambalo umelitolea maelekezo ambalo limeshindwa kufuatwa hapa Bungeni?

Kwa hiyo, nataka unipe mwongozo wako, hivi Kiti kikitoa maelekezo na Mbunge anaendelea kukaidi maelekezo, Kiti kinachukua hatua gani? Maana tukiliacha hivi, kila mtu atanyanyuka tu na kuamua vyovyote hata kama Kiti kimetoa maelekezo.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako katika hili.

SPIKA: Naomba kaeni. Miongozo haiwezi kuwa miwili. Ninachosema ni kwamba, hotuba yake haikuwa *recorded completely,* kwa sababu ndiyo maagizo yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jenista Mhagama tuendelee!

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema ili niweze kuchangia katika mada hii katika siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kusema, naomba kwa mujibu wa kanuni, niseme kwamba inawezekana yale nitakayoyazungumza yatakuwa na maslahi yangu binafsi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Kamati ambayo inasimamia shughuli za Wizara hii na Kamati ambayo imekuwa ikiishauri sana Serikali kuhusu masuala yote muhimu yanayohusiana na Wizara hii. Maslahi yangu niliyonayo hapo siyo ya kifedha, lakini ni maslahi ya maendeleo ya wananchi wa Tanzania na nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba naipongeza Wizara hii, kwa kazi kubwa inayofanya, na mambo yote haya yanayosemwa, Taarifa ya Kamati ilipowekwa leo Mezani na kusomwa na Kamati yangu, imeanza kwa kuelezea maeneo ambayo Serikali kupitia Wizara imeyazingatia na imefanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpatie. Ni kweli kabisa yapo maeneo ambayo sisi kama Wabunge tunatakiwa kushauri. Nami niseme kwamba sioni kama busara inanituma, kipindi hiki ambacho tunao vijana takribani milioni 16 katika nchi yetu ya Tanzania, tunaacha kuchukua nafasi muhimu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuishauri Serikali na kuungana mkono na juhudi za Wizara katika kutatua tatizo la vijana hao milioni 16 na tukajiingiza na kuzungumzia masuala ambayo hayaendi kuleta ukombozi kwa asilimia hiyo ya vijana walioko katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, yameelezwa hapa kwamba Wizara hii haijali masuala yoyote yanayohusiana na vijana, haishughulikii suala la Baraza la Vijana, haishughulikii suala la Benki ya Vijana na halishughulikii suala la kuwawezesha vijana.

Mheshimiwa Spika na Bunge hili, naomba niwaambie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu, baada ya Kamati kukaa na Wizara, kwanza Wizara imetuletea mpangokazi, mpango wa kwenda kuwakomboa vijana hawa milioni 16 wa Tanzania.

Tayari mpango huo Serikali imeuandaa na umeshaletwa ndani ya Kamati kwa niaba ya Bunge hili na Wabunge ambao hawafahamu wawasiliane na Wajumbe wa Kamati na wale ambao hawakupata nafasi ya kushiriki mijadala hiyo, nadhani wakija kwenye Kamati yetu watayafahamu hayo na baada ya Kamati yetu kupokea mpango huo kabambe wa kuwakomboa vijana wa Tanzania, ilipita na kuitazama bajeti ya Wizara na kuona imejipanga vipi katika hilo.

Mheshimiwa Spika, t•Tulichokuja kugundua ni kwamba Serikali kwa mwaka huu wa fedha imetenga Shilingi bilioni tatu kwenda kuanzisha harakati za kutatua kero ya ajira kwa vijana wa nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunachokishauri na mimi kama Mbunge wa Jimbo la Peramiho mwenye vijana ambao wapo ndani ya hao milioni 16 ninasema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaishauri Serikali yangu sikivu kabisa ya Chama cha Mapinduzi kwamba milioni tatu hizo zilizotengwa na Serikali kwenda kutatua kero ya ajira kwa vijana hazitoshi, ziongezwe ili harakati hizi zikianza ziwe na mafanikio makubwa.

Hiyo ndiyo hoja ya msingi hapa na siyo kuzungumzia maeneo ambayo hayaendi kuleta tija wala kutatua matatizo ya vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu wakati inafanya mjadala na mimi kama Mbunge, tulipitia bajeti ya Kilimo na tulijiuliza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti ya kilimo tumegundua kwamba kuna mradi mkubwa wa *SAGCOT* ambao utakuwa na Shilingi bilioni 17 ambayo ni fedha ya ndani ya Tanzania. Lakini mradi huo wa *SAGCOT* utakwenda kusapotiwa pia na fedha za nje kutoka kwa wenzetu wa Marekani. Kuna mradi wa Afrika Mashariki wa kilimo na wenyewe una fedha zake.

Tulichoishauri Serikali na ninachotaka kuishauri Serikali na kuonyesha kwamba Serikali yetu inajali masuala haya tunayoyazungumza, Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi, tumekubaliana Wizara hii sasa na Wizara ya Kilimo katika miradi mikubwa kama hii, itambue fursa muafaka zilizopo ili kuwasaidia vijana kwenye miradi hii ya kitaifa kupitia Wizara yetu na kwa kupitia Shilingi bilioni tatu zilizotengwa na fedha nyingine tunazoziongeza, basi vijana wa Tanzania katika makundi tuliyonayo, wapo vijana wasomi wamemaliza *SUA* na katika Vyuo Vikuu vingine, wapo vijana ambao wana elimu za ufundi stadi na wapo vijana wengine wanaweza kufanya hata shughuli za vibarua.

Mheshimiwa Spika, Miradi mikubwa hii iliyopangwa na Serikali, Wizara hii imejipanga katika mpango kabambe kwenda kushirikiana na Wizara kutatua tatizo la ajira. Sasa mtu anaposema Serikali haijali, anataka Serikali ijali kwa kubeba kitu gani kichwani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yakifanyika, ndiyo mambo tunayoyasema, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inatekeleza ilani yake na yakisimamiwa vizuri yataondoa matatizo haya ya vijana kwa ngazi zote kupitia vijana wasomi, vijana wa ngazi ya kati na vijana wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba Wizara hii haijaanzisha harakati za kuwa na benki ya vijana. Ninaipongeza Wizara katika Bajeti ya mwaka huu, imeshatenga fedha za mchakato wa kuanzisha benki ya vijana kama ilivyoahidi.

Ninaomba nguvu hiyo ya Serikali katika kuanzisha benki ya vijana katika nchi yetu ya Tanzania isiishie hapo na iweze kuendelea mbele.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, tunaomba nguvu iliyoanzishwa na Wizara kwa mfano, baada ya Bunge la bajeti ya mwaka 2012, tuliiagiza Wizara kukaa na vyombo vyote vinavyohusiana na tasnia ya sanaa katika nchi yetu ya Tanzania ili waweze kuangalia ni namna gani wanaweza kutatua matatizo ya tasnia hii? Hatua zimechukuliwa; hatua zimeshachukuliwa!

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba hatua hazijachukuliwa, tayari wote sisi ni mashahidi kwa wale watu ambao wananunua kazi za wasanii, kazi zote za wasanii sasa hivi zimeshaanza kuwekewa stika kuonyesha mali ya kazi za wasanii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, upo upungufu, nakubali katika sheria ile, sheria bado haijaweka bayana namna ya kuwalinda wasanii wa ndani kwa kazi zao ukilinganisha na wasanii wa nje. Haya ni mambo ambayo tunaiomba Serikali yetu kwa usikivu ule ule wa kuanzisha stika, basi usikivu ule ule wa kubadilisha sheria nao ufanyike. Sasa kama mambo mengine yameshaanzishwa, kwa nini tusiwapongeze na tukayasubiri hayo mengine ambayo tunataka kufanya mabadiliko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba pale ambapo kazi imefanyika, ni budi Wabunge wa Bunge hili wawe na ujasiri wa kuyasema mazuri na kushauri upungufu uliobakia. Naiomba Wizara pale ambapo pamebaki na hasa katika sheria zinazowalinda wasanii, kazi hiyo ifanyike. Siyo kweli kwamba Serikali hii sikivu haijasikia kabisa kilio cha wasanii.

Kwa hiyo, naomba sana Serikali mfahamu hilo na muweze kuona namna gani tunaweza kujipanga na kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, naendelea katika suala la *TBC*. Hakuna nchi yoyote duniani na katika ulimwengu huu haimiliki chombo cha habari. Hakuna kabisa! Nchi zote zinamiliki vyombo vyake vya habari vya Kiserikali.

Mimi nilidhani sisi Wabunge leo tungesema kwa kazi kubwa inayofanywa na *TBC* kuonesha matukio na shughuli tu kwanza za hapa Bungeni, tungeungana mkono kabisa ili *TBC* waongezewe fedha katika bajeti yao. Haya yanayotokea Bungeni kila siku Watanzania wanahabarishwa na *TBC*. Mambo yote yanayoendelea ndani ya Bunge hili, nikiacha tu yale mengine ya nje, ni *TBC* ndiyo wanaofanya kazi hii kubwa hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chombo hiki ni cha Serikali, uendeshaji wa chombo cha Serikali utatofautiana kwa asilimia 100 na chombo kingine ambacho siyo cha Serikali. Leo naiomba Serikali...

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, hii ni kengele yangu ya kwanza.

WABUNGE: Ya pili hiyo!

SPIKA: Ni kengele ya pili.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

SPIKA: Namwita Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Nkamia, halafu atafuatia Mheshimiwa Philipa Mturano.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza naomba niseme kwamba mimi pia ni mwanahabari kwa kusomea na kufanya kazi kabla sijawa

Bungeni. Wanahabari wenzangu pamoja na vijana wanajua jinsi ninavyowatetea.

Mheshimiwa Spika, lakini nitakayoyasema sina maana kwamba, naunga mkono vitendo vya unyanyasaji ambavyo wanafanyiwa waandishi wenzangu wa habari. Mimi pia ninavipiga marufuku na ndiyo maana tunasema Serikali iharakishe mchakato wa sheria ya kulinda na kutoa uhuru wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu wangu wa somo la *News Writing*, Mwalimu Dogoli, ambaye ni mzuri sana kwa somo hilo alinifundisha kwamba siyo kila kitu ni habari. Ni lazima upime habari utakayotoa: Je, ina maslahi kwa Taifa? Je, italeta athari gani kwa Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama viongozi, tunao uhuru kwa sababu tumepewa uhuru wa kupata habari na kuwasiliana na wananchi. Je, sisi viongozi ambao waasisi na wazee wetu wanaotaka kutuachia madaraka, tunautumiaje uhuru huu wa kutoa habari kwa wananchi?

Niwaambie vijana wenzangu, Taifa hili ni zaidi ya CCM, CHADEMA, *CUF* na *TLP*. Sisi ndiyo tunatakiwa tuongoze, tuoneshe mfano wa *how to be a good political leaders*. Vijana wenzangu tuoneshe mfano kwamba tunaweza kuongoza. Tusijenge Taifa la visasi na chuki; tutashindwa kuliongoza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda niweke wazi kwamba tusioneshe ujana, tuoneshe uongozi wetu tukiwa vijana. Tuoneshe kwamba tuna uwezo wa kuendelea kulitumikia Taifa hili katika kukuza uchumi wa nchi yetu wakati tukiwa na amani na utulivu. Nilikuwa napenda nisisitize hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini waandishi wa habari wana matatizo yao mengi, wanalalamikia maslahi yao na wengi wanafanya kazi nzuri, ingawa bado kuna wale wachache ambao hawafuati *ethics* za uandishi wa habari. Chonde

chonde, leo hii tuko katika hali ngumu, tuna maadui nje, tusi-*create* maadui wa ndani *unnecessarily*. Taifa hili linatutegemea vijana wenzangu wa pande zote, tuoneshe tuna uwezo wa kuongoza. Tusitumie uhuru wa kutoa habari vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kupongeza Wizara kwa kuongeza Sh. 3,100,000,000/= katika mfuko wa vijana. Nami naungana na taarifa ya Kamati kwamba bado fedha hizi ni ndogo. Vijana wengi wanahitaji kuwezeshwa, wanahitaji kukabiliana na tatizo la uchumi linalowakabili vijana wa mjini na wale wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, pia wakati napitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, bado kuna tatizo, zipo fedha kidogo sana kwenye bajeti ya maendeleo, Shilingi milioni 600 ni ndogo. Nimeona Mheshimiwa Waziri ameweka katika maeneo mengine, lakini kwenye ukarabati wa vituo vya vijana, hakuna fedha kabisa.

Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali yangu, kadri siku zinavyokwenda tuendelee kuongeza fedha za kutosha katika bajeti ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukiwa na fedha za kutosha kwenye bajeti ya maendeleo na mfuko wa vijana, tutakuwa na uwezo wa kuwekeza kwa vijana ambao wanajihusisha na shughuli mbalimbali. Kama ambavyo tunaona sasa hivi, vijana wameamka, wanajihusisha kwenye sekta ya kilimo, lakini kama hatutakuwa na fedha za kutosha, bado hatutaweza kumaliza tatizo la ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba kuna malalamiko kwenye Halmashauri zetu kwamba, hizi fedha hazifiki huko. Naomba nitolee mfano wa nyumbani kwetu Bunda, tangu mwaka 2005 ni Shilingi milioni 10 tu ambazo zimekwenda. Kule tuna vikundi zaidi ya 90 ambavyo vina wanachama zaidi ya 400, lakini vilivyofaidika ni vikundi viwili tu kwa Shilingi milioni tano tano.

Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie jambo hilo kwa mapana yake.

Mheshimiwa Spika, nimesoma kwenye hotuba ya Waziri ambapo amesema baada ya kilio kirefu, sasa Serikali iko kwenye mchakato wa kuleta sheria ya kusimamia vyombo vya habari. Hili ni jambo jema, lakini nilitegemea mambo haya yangekwenda sambamba.

Mheshimiwa Spika, unapoleta sheria ya kusimamia vyombo vya habari, ingekwenda sambamba na sheria ya kulinda uhuru wa kupata habari kwa vyombo vya habari. Sasa hapa Mheshimiwa Waziri amesema baada ya kumaliza mchakato huu, ndiyo uanze mchakato mwingine. Mimi naona mambo haya yanakwenda sambamba.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nilikuwa napenda kuzungumzia kilio cha wasanii. Naungana na nimpongeze Ndugu na Dada yangu Jaydee, tumetoka wote Wilaya moja, kwa kazi nzuri. Huyu amekuwa ni *role model* kwa wasanii wengi wa kike. Natambua ana mchango mkubwa katika kuwasaidia wasanii, lakini pia mbali na matatizo mengi ambayo *Clouds* imesemwa, Ruge naye pia ana mchango katika kukuza sekta hii ya muziki.

Mheshimiwa Spika, ninachowaomba wakongwe hawa ni kwamba, wote wanajenga nyumba moja, hivyo hawana haja ya kugombea fito. Kwa hiyo, *Clouds FM* na Lady Jaydee lazima wakae waone ni jinsi gani watawasaidia wasanii kuwa pamoja. Haya malumbano hayana hoja, hayana msingi wala maslahi kwa wasanii. Nilikuwa naomba kwamba, ipo haja ya wao kukutana.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Nchimbi aliwakutanisha Sugu na Ruge, wakamaliza yale matatizo, ingawa hata hilo wameshindwa kulipongeza, kwa kiasi hicho hicho naomba Mheshimiwa Waziri awakutanishe Lady Jaydee na Ruge, kwani hawa wote wana mchango kwa Taifa hili.

Narudia kwa kusema kwamba, natambua sana mchango wa Lady Jaydee na ni rafiki yangu mkubwa, kwani amekuwa akiniletea maoni mbalimbali kuhusiana na matatizo ya wasanii, lakini wote tunawategemea.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya wasanii hawa kukutana ili waone ni jinsi gani ambavyo wanaweza kusaidiana na sisi viongozi vijana na wasanii wenzao humu ndani kama Mheshimiwa Vick Kamata na Mheshimiwa Mbilinyi (Sugu) ili kuona namna ambavyo tunaweza tukasaidia vijana wenzetu ambao wako kwenye hii *industry* ya muziki. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumzia hapa suala la mapato kwamba Wizara imekusanya Shilingi milioni 800. Lakini kama Wizara ikifanyia kazi na kusimamia wizi wa kazi za wasanii, ninaamini katika mwaka ujao wa fedha Waziri atatwambia wamekusanya Shilingi bilioni kadhaa kupitia kazi za wasanii. Wasanii watafaidika, lakini na Serikali itapata mapato.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kwamba, vijana wa Taifa hili, bila kujali itikadi zetu, Taifa linatutegemea. Tusitumie uhuru vibaya. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo iliyo mbele yetu. Kwanza, niwape pole Waandishi wenzangu wa habari waliopata matatizo katika kipindi cha mwaka huu, lakini watambue kwamba uandishi wa habari ni *semi soldier*.

Mheshimiwa Spika, pili, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nimshukuru sana Ndugu yangu Dioniz Malinzi, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuendesha *BMT* na sasa hivi tunaona mafanikio yake.

Mheshimiwa Spika, nianze na huu Muswada wa Sheria ya Vyombo vya Habari ambao Mheshimiwa Waziri ameahidi

kwamba atauleta katika Bunge hili mwaka huu. Muswada huu utakapokuwa sheria, utakuwa umesaidia sana waandishi wa habari kupata haki zao. Lakini nitoe angalizo kwa kupingana na mwenzangu aliyekaa punde hivi kuhusu ile sheria ya *right to information*.

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na Muswada huu unaokuja sasa, lakini huo mlioupendekeza kwamba, tuwe na *right to information* ni lazima Serikali iwe makini sana kwenye hili. Sheria hiyo inasumbua sana India, Afrika Kusini na hata kwa wakubwa huko. Kwa hiyo, ni lazima Serikali ifanye tathmini ya kutosha kabla ya kuja na huo Muswada ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, huo Muswada umekuwa ukishinikizwa sana na baadhi ya *NGOs* ambazo zinadai kwamba na zenyewe zinatetea haki za waandishi wa Habari. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali iwe makini juu ya hilo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa sheria utatusaidia sana waandishi wa habari ku-*set standard* ya uandishi wa habari. Tuna tatizo kubwa la *standard* ya uandishi wa habari katika nchi yetu. Waandishi wengi wa habari hawana malipo stahiki katika vyombo vya habari vya Serikali, na hata huko kwa vyombo vya habari binafsi ndiyo kubaya zaidi. Ni hao hao wanaoandika kwamba Serikali inashindwa kutafuta ajira kwa Watanzania, wakati wao wenyewe hawajapata ajira huko wanakofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukienda Dar es Salaam pale kwenye *Press Conference* unakuta waandishi zaidi ya 70, kwenye *Press Conference* moja. Baadhi yao ndiyo hao tunaowaita waandishi kanjanja kwa sababu hatuna *standards* za uandishi wa habari katika Taifa letu. Ninaamini hilo litasaidia sana. Sheria hii itawasaidia waandishi wa habari kuwa na *governing body* yao kama ilivyo hivi sasa kwa wahasibu na wanataaluma wengine.

Mheshimiwa Spika, leo kuna baadhi ya watu wanajifanya kama ndio *governing bodies* za waandishi wa

habari. Mfano *MCT* na Jukwaa la Wahariri. Hizi ni *NGOs*, lakini haziko pale kwa ajili ya kutetea maslahi ya waandishi wa habari, ziko pale kwa ajili ya *interests* zao. Tukiwa na sheria hii itatusaidia sana kama Taifa kujua nini mustakabali wa waandishi wa habari na heshima yao itabaki pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maafisa Habari kwenye Wizara zetu za Serikali hii, wanafanya kazi gani? Ni watu wamepata kazi, ama kazi imepata watu? Hawafanyi kazi, na wako chini ya Idara ya Habari, Maelezo; lakini kazi faifanywi. Leo unasikia Mheshimiwa Waziri kasema hili, kesho Katibu Mkuu kasema hili, hawa Waandishi wa Habari ambao ni *spokespersons* wa hizi Wizara wanafanya kazi gani? Hata ukiangalia kwenye bajeti za Wizara zote, zinatengwa fedha pale kwa ajili ya Idara ya Habari na Mawasiliano, lakini hawafanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, nije Idara ya Habari Maelezo. Kila mwaka Idara ya Habari Maelezo inatoa *Press Cards.* Kila mwaka! Hivi hatuwezi ku-*set standard* tukawa tunatoa hizi *Press Cards* kila baada ya miaka mitatu? Itasaidia zaidi kujenga heshima ya Waandishi wa Habari katika nchi yetu. Kutoa hizi kadi kila mwaka, imefikia hatua hata katika Bunge hili baadhi ya Waandishi wa Habari wanapoteza vitambulisho na inawalazimu wahariri wao ndio waje ndani ya Bunge kuje kuandika habari, kazi ambayo siyo yao.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye michezo. Kwa kweli makato kwenye uwanja wa Taifa ni makubwa mno, tunawanyonya wachezaji wa mpira wa nchi yetu! Mheshimiwa Naibu Waziri Makala anacheza mpira sana, naomba mtusaidie kwa hili. Mfano mdogo tu, juzi katika mchezo ule wa Simba na Yanga ambapo Simba walifungwa kwa taabu magoli mawili, zilipatikana Shilingi milioni 500, lakini vilabu vya Simba na Yanga, vimepata Shilingi milioni 246, Shilingi milioni 254 zimekwenda wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana hawa hii ndiyo ajira yao. Kesho na kesho kutwa wakistaafu mpira, wanategemea hiki wanachokitapata kiwasaidie maisha yao, isije kuwa kama

yale ya akina Jela Mtagwa. Ndiyo maana nilianza mwanzoni kwa kumpongeza Dionizi Malinzi kwa kazi nzuri anayoifanya. Hebu naombeni tusaidie vijana wetu wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kodi ya makocha wa kigeni wanaofanya kazi hapa nchini. Alikuja Maxio Maximo, Serikali ilikuwa inamlipa mshahara na Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba analipa mshahara kwa ajili ya makocha wale. Amekuja King Paulsen, vivyo hivyo; lakini juzi juzi imejitokeza kwamba hawa makocha hawakulipa kodi, ikawa aibu kubwa kwao.

Ningeomba Mheshimiwa Waziri anisaidie, ni nani alikuwa anatakiwa kukata ile kodi? Kwa sababu ninavyofahamu, inawezekana kabisa mishahara ya makocha wale ilikuwa inapitia Hazina. Sasa inakuwaje leo hawa makocha hawajalipa kodi wakati fedha ilikuwa inapitia Hazina? Tunajidhalilisha sisi kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, nime-*declare interest* kwamba mimi ni Mwandishi wa Habari, lakini nimalizie tu kwa kuzungumzia habari ya *TBC*. Nimefanya kazi pale kwa muda mrefu kidogo. Hali ya maisha ya wafanyakazi wa *TBC* ni mbaya. Fedha inayotolewa na Serikali kuendesha lile shirika ni kidogo. Umeme unaotumika *TBC* kwa mwezi ni zaidi ya Shilingi milioni 100.

Naiomba Serikali iliangalie jambo hili. Taasisi hii ni chombo cha umma, *all over the World* kama alivyosema Mheshimiwa Jenista Mhagama. *BBC* ni Shirika la Umma la Uingereza, *Voice of America, ABC* Marekani; Urusi iko hivyo hivyo, *RAI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba, hebu tuangalie Shirika hili la Habari la Umma, lipo kwenye hali mbaya sana. Vitendea kazi ni vibovu, matangazo yanakatikakatika; nilikuwa namshangaa mtani wangu hapo, rafiki yangu Mheshimiwa Sugu kwamba, *TBC* huwa wanakata matangazo labda wanapozungumza wapinzani; siyo kweli! Mheshimiwa Rais alikuwa anahutubia Arusha matangazo

yakakatika, yule siyo mpinzani. Kwa hiyo, tunapozungumza lazima tufanye *research*, tuwe na *data,* siyo tunazungumza tu kwa sababu tunaweza kuzungumza. Hapana! Kuna kuzungumza na kupiga kelele. Hivi ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, tufanye *research*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana Serikali iitazame *TBC* kwa jicho la huruma. Ni kweli wanakusanya mapato, mapato yao yale yahatoshi na hata hayo mapato wanayokusanya yanakwenda Hazina.

Naombeni sana, kama nilivyosema, mimi nimefanya kazi pale *about ten years*, hali ya pale ni mbaya sana. Kuna jengo pale alizindua Mheshimiwa Mzee Alli Hassan Mwinyi, amekaa miaka 10 madarakani, amestaafu; amekuja Mheshimiwa Mkapa, amestaafu; Mheshimiwa Kikwete pia inawezekana akastaafu. Hebu jamani saidieni lile jengo pale. Mnaweza kabisa kuihamisha *TBC* kutoka kule ilipo ikaja Mikocheni kule mkawapa viwanja vile wakafanya *investment* waka-*generate funds* kama Serikali inashindwa kuwapa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, Mwanza pale wana uwanja mkubwa sana. Matokeo yake watakuja kunyang'anywa kile kiwanja. Ile mitambo ambayo zamani walikuwa wanaitumia sasa imekufa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Phillipa Mturano atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Tauhida Calos Nyimbo na Mheshimiwa Margaret Mkanga wajiandae.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu. Wiki mbili zilizopita nilimwuliza swali Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhusu pato linalopatikana pale Uwanja wa Taifa kwa mwaka ni kiasi gani? Kwamba

tangu mwaka 2007 uwanja ule umeanza kutumika mpaka sasa tumepata kiasi gani? Mheshimiwa Waziri akajibu kwamba tumepata Shilling bilioni moja tu.

Mheshimiwa Spika, kwa ushahidi ambao umeonekana sasa hivi tu kwa mapato ambayo yamepatikana jana na kwamba hawa wachezaji wenyewe wamepata Sh. 200,000,000/= tu hizo nyingine sijui zimekwenda sehemu gani, ni wazi kabisa kwamba siyo Shilingi bilioni moja kwa muda wa miaka yote mitano tangu Uwanja wa Taifa umeanza kutumika. Hii pengine ni mwendelezo ule ule wa kubeba zile fedha kwenye viroba zinapelekwa bila *escort* ya Polisi zikifika njiani zinaporwa, hakuna mtu wa kuuliza.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani fedha za Watanzania, fedha nyingi namna hiyo zikabebwa bila ya kuwa na *escort* ya Polisi halafu zinafika njiani mnasema kwamba zimeporwa. Haiwezekani! Huu ni ufisadi uliokithiri!

Narudia tena kwa mara nyingine, *CAG* aende akafanye ukaguzi *TFF* tujue mapato halisi ambayo yanatokana na mechi zinazochezwa katika Uwanja wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilizungumza nikasema kwamba, nimeona hata kwenye vyombo vya habari, Mheshimiwa Waziri akasema kwamba hafanyi kazi na magazeti; ni Waziri mwenye dhamana na vyombo hivyo vya habari, akasema kwamba yeye hafanyi kazi na vyombo vya habari. Lakini ni Afisa wake katika Wizara yake ambaye alikuwa analalamika jinsi fedha zinavyobebwa hovyo na kwamba amelalamika lakini Wizara haikuchukua hatua yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lugha ni kielelezo cha Taifa lolote lile, na ni wajibu wa kila Taifa kuheshimu lugha yake kama kitambulisho chake. Nirudie kutoa masikitiko yangu kama ambavyo nimeshasema siku za nyuma kwamba nasikitika sana kuona kwamba Kiswahili chetu sisi hatukizungumzi inavyostahili kama vile wengine wanavyozungumza lugha zao hata wanapokuwa nje ya Mataifa yao.

Kwa kumbukumbu yangu mimi, imekuwa mara ya pili Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Watu wa China anakuja Tanzania, pamoja na kwamba anafahamu Kiingereza vizuri, pengine na lugha nyingine, lakini alihutubia kwa kutumia lugha ya Kichina bila kujali kwamba anaowahutubia ni Watanzania ambao hawafahamu Kichina, lakini alionyesha namna gani anaenzi utamaduni na anatambua utamaduni wa nchi yake.

Naomba sana Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo mlifanyie kazi hili ili na sisi lugha yetu iweze kufahamika Kimataifa. Tusionee haya, ndiyo lugha yetu na ndiyo inatutambulisha huko nje tunapokwenda.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu Michezo Mashuleni. Mmerudisha Michezo Mashuleni, tunashukuru. Lakini hii Michezo ya UMISHUMTA imekuwa na matatizo. Fedha inayopelekwa kule ni ndogo, sasa wanaanza kuchangishana mpaka walimu ili kuwezesha suala hili. Kwa kweli tunaomba kama hiki kitu kimeanzishwa wakati hatujakuwa na uwezo, tukiache kwanza tuendelee na mengine ambayo tuna uwezo nayo. Tunatambua uwezo wetu pengine hauruhusu, basi tuliache kuliko kuanza tena kuwaumiza wazazi kuchangisha fedha hizo kwa watoto na walimu kukaa wanaombaomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije upande wa wasanii. Tulizungumza suala la Jela Mtagwa, sina taarifa sahihi kama Serikali imeshachukua hatua yoyote kuanza kumpatia matibabu. Lakini pia tuliambiwa kwamba siyo lazima na siyo jukumu la Serikali kuwatibia hawa wasanii isipokuwa pale wanapopeleka maombi maalum.

Mimi nadhani kwa kutambua mchango wa Jela Mtagwa kwenye stempu zetu miaka iliyopita, ameitangaza Tanzania Kimataifa, tunastahili kabisa kumpatia matibabu bila hata kujali kupelekewa maombi. Kwa sababu tumezungumza sana Wabunge wiki mbili zilizopita na leo tunazungumza, hayo ni maombi tosha, hamna haja ya maombi mengine. Tunaomba huyu mtu ahudumiwe,

ikishindikana, basi sehemu ya mapato ya ile stempu ambazo zilitumika picha zake, apatiwe ili aweze kujitibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo huyo tu, tunaye *Mzee Small,* sasa hivi yuko anasota, ni mgonjwa, hana msaada wowote. Sasa sijui tunasubiri waje waondoke ndiyo tutoe salamu za rambirambi! Sielewi! Lakini hawa watu wamekuwa muhimu sana, wamekuwa wakitangaza Taifa letu, pia tunaburudika, tunapata mafundisho kutoka kwenye maneno yao wanayozungumza wakati wanapofanya maigizo, tunaomba sana Serikali iwaangalie hawa.

Mheshimiwa Spika, mtu kama *Mzee Small* ni mzee na ni masikini, hakuna mtu wa kumlilia, hakuna mtu wa kumsemea, ni sisi. Tunaomba Serikali isikie kilio hiki, imtetee *Mzee Small* hata kama anafanya michezo labda kwa udhamini wa Kampuni fulani, lakini bado Serikali ndiyo msimamizi wa watu hawa, ijue wasanii wake wanaishi vipi. Tumeona wasanii wengi wakifa wakiwa katika hali ngumu sana za maisha. Ilikuwa ni aibu kubwa Mzee Kipara ameshafariki na alifariki katika hali ngumu bila kupata msaada wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bibi Kidude amefariki hivi juzi, alikuwa katika hali ngumu sana, lakini baada ya kufa alipata mazishi ya heshima. Basi heshima hii kama tungempatia akiwa bado ni mgonjwa, tukamtibu pengine tungekuwa naye hadi sasa.

Kwa hiyo, tunaomba Serikali iwaangalie wasanii. Ninakumbuka miaka ya nyuma wakati Mheshimiwa Mstaafu Rais Benjamin Mkapa anagombea Urais alikuwepo Mzee mmoja ambaye sasa hivi amefariki, alikuwa anaitwa Mzee Jongo. Huyu mzee ndiye aliyeanzisha ile *slogan* amesema kwamba alikuwa anapita kwenye Kampeni akimnadi Mzee Mkapa anasema kwamba "Mchague huyu kijana ni mwadilifu, bado ni mdogo, anaweza kazi, huyu kijana anaitwa Benjamin, mtoto wa William, mjukuu wa Nkapa." Watu walikuwa wanacheka, wanafurahia na wakamchagua kweli. Sasa watu kama hao tuwakumbuke, tujue mchango

wao kwamba ni mzuri, wanatusaidia kwenye shughuli zetu ambazo tunazozihitaji, tukishapata tunawasahau. Haipendezi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu mavazi ya wasanii. Tumepiga kelele sana, Wizara tunaomba mtusikilize. Wasanii hawa wa bendi za muziki wa kike, zile nguo wanazovalishwa zinatia aibu. Tumeshasema sana, tuongee lugha gani jamani tueleweke? Wanatudhalilisha sisi wanawake wenzao. Tunashukuru sasa hivi Wizara inaongozwa na mwanamke mwenzetu, naomba ulione hilo ndugu yangu. Tunaaibika, tunadhalilika kwa nguo zile. Hata kama hawataki kubadilika, tunaomba mwongee na wamiliki wa bendi hizo, mwaeleze hali halisi kwamba wanatakiwa wavae mavazi yenye nidhamu. Tunajua wakati mwingine wanatoka jasho sana hawatakiwi kuvaa nguo ngumu, lakini haizuii kusitiri maeneo nyeti. Tunaomba sana Serikali mliangalie hilo. Tunaadhirika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hii timu ya wanawake inaitwa Mburahati *Queens* waliwahi kuja hata Bungeni kipindi fulani wakajitangaza hapa tukawaona. Timu hii inahitaji huduma. Wale wasichana wa ile timu wanacheza mpira mzuri, siku moja walicheza na timu ya wanaume wakawashinda. Hii ni timu ya kuendelezwa. Mheshimiwa Waziri ni mwanamke, timu hiyo ya wanawake iko Kinondoni. Tunaomba uitembelee, muisaidie, muipatie vifaa, muwape moyo, hata ikibidi muwape ziara waende wakatembelee sehemu nyingine waone wenzao wanafanya vipi ili tuwe na ushindani ambao ni mkubwa sana hatimaye tuweze kulitangaza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, leo kwa kuwa nimepata nafasi hii, basi nitamtaka tena Mheshimiwa Waziri anapohitimisha anieleze kwamba ule Uwanja wa Taifa uko Temeke, mechi zinazofanyika pale ni nyingi. Mechi hizo zinapofanyika pale, zinahusisha uwepo wa biashara nyingi, uuzwaji wa *T-shirt*, ubuyu, mahindi, biskuti, pipi na kadhalika, panakuwa pachafu sana. Mechi ikiisha watu wanaondoka, uchafu unabaki umezagaa. Ni Manispaa ya Temeke tunaofanya

usafi. Tunaomba Manispaa ya Temeke tupewe mgao japo kidogo, maana sisi ndio tunaosafisha pale. Mheshimiwa Waziri aliniambia kwamba ni hiyo asilimia ngapi sijui inakwenda huko Hazina, inasaidia Watanzania wote kama kawaida. Nakubali, lakini Mheshimiwa wewe unafahamu pale mechi inapokuwepo, kama juzi ilipokuwepo, pale ni pachafu mno! Miundombinu mingi inaharibika, ni Manispaa ya Temeke inayokuja kutengeneza. Naomba tupate mgao japo kidogo wa kufanyia usafi maeneo hayo baada ya kumalizika mechi hizo.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa tulisema kwamba waajiriwe, wengine waende JKT. Wanafunzi wamekwenda huko, lakini mimi nikija kwenye Wizara yako tunaomba basi uombe vijana wengine waweze kwenda JKT, hata wale ambao sio wanafunzi na pindi wanapojiunga na...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mturano. Namwita Mheshimiwa Martha Mlata, atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Galos na Mheshimiwa Margaret Mkanga ajiandae.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa, kwa sababu muda ni mdogo, naomba niseme jambo moja. Mheshimiwa Rais wangu ametuhumiwa kutotumia Kiswahili wakati Rais wa China alipokuwepo. Lakini ninavyofahamu, siyo kosa lake. Rais wa China alikuja na mtafsiri anayejua Kiingereza kwenda Kichina. Kwa hiyo, ninachoomba labda Wizara itusaidie kuwapeleka Watanzania wakajifunze Kichina ili Mchina anapokuja, basi tuongee Kiswahili na Kichina.

Mheshimiwa Spika, naomba pia ni-*declare interest* kwamba mimi ni msanii wa muziki wa Injili, lakini naomba niseme jambo moja. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu, nilipoingia Bungeni mwaka 2005 nilipitia *Hansard* za nyuma, sikuwahi kukuta suala la wasanii limeingizwa ndani ya Bunge.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa ni msanii wa kwanza kuingiza suala la kutetea masuala ya wasanii ndani ya Bunge. Hivyo ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kuona kwamba sasa tumekuwa na kikundi ambacho kinaweza kitatetea wasanii ndani ya Bunge. Lakini niwaase tu wasanii wenzangu tulioko ndani ya Bunge tuwe na subira kwa sababu tulikotoka ni mbali tunakokwenda bado ni mbali, tunahitaji twende kwa staha. Unapotaka kumwomba baba akusaidie ukamwombe kwa heshima na nidhamu ili aweze kukusikiliza na kukupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuanza kuzungumzia Mfuko wa Kuwawezesha Vijana. Natamka hivyo kwa sababu naelewa kundi kubwa la vijana ambalo ni la wasanii, Mfuko huu Wizara imeomba fedha Shilingi bilioni 10, lakini imepewa Shilingi bilioni tatu. Kama kweli Serikali au Wizara ina nia ya kusaidia kundi hili, hizo fedha bado hazitoshi. Nasema hivyo kwa sababu kama wasanii wao hawana dhamana yoyote, dhamana ni wao na vipaji vyao na kazi zao. Ukienda kwenye Mabenki mengine utaambiwa ulete nyumba. Msanii hawezi kupeleka nyumba. Mfuko huu ungekuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa vijana hususan ninawazungumzia wasanii.

Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yako wekeni mkakati ili wasanii waweze kukopesheka. Wameandaa kazi zao, zimekaa *studio,* anataka kufanya video, anataka kukomboa kazi yake, lakini hana fedha. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, mmesema kuna mtandao mmeuanzisha wa ndani kwa ndani, nyinyi mnaweza mkagundua Martha Mlata ameuza kanda ngapi, ameuza *CD* ngapi, ana *album* ngapi kupitia *COSOTA* ili niweze kukopesheka, hiyo ndiyo iwe dhamana ya msanii. Nilikuwa naomba sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bado kuna mradi wa *sticker* nashukuru limezungumziwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Tunapofika kwenye kuungana kwenye kitu kimoja ni lazima tuseme Mradi wa *Sticker* mimi nilikuwa wa kwanza kuzungumza Mradi wa *Sticker*, lakini lilipofika hapa likaporwa. Mmepeleka, mmeliandaa mnavyojua wenyewe, matokeo

yake mmeleta hapa kwa faida ya Serikali, wala sio kwa faida ya msanii, kwa sababu *TRA* anapokwenda kukusanya yale mapato una uhakika gani kwamba msanii ameweza kufaidika na *Sticker* ile? Kumetokea matatizo sasa hivi, wasambazaji wanakataa kuchukua kazi za wasanii mpaka wapeleke *sticker*.

Mheshimiwa Spika, naomba mradi ule usitenganishwe, apelekewe *COSOTA,* ataelewana na wasanii ni namna gani *sticker* zile ziweze kutumika kwa ajili ya kumkomboa msanii na wala siyo kwa ajili ya kukusanya kipato kwa ajili ya *TRA*. Tuliongea kwamba *sticker* kwa ajili ya kumsaidia msanii siyo kwa ajili ya kipato, kwa ajili ya *TRA*, ninaomba sana suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine la wizi wa kazi za sanaa kwenye milio ya simu. Ninasikitika sana kwa sababu utaratibu ule bado mpaka sasa hivi haufahamiki. Naomba *TCRA* ikabidhiwe jukumu hilo la kusimamia na kukusanya na kuhakikisha mikataba yote ya kazi za wasanii kwenye milio ya simu na yale Makampuni ambayo yanawaibia wasanii; wasanii bado wanahangaika, unafanya kazi kubwa, mtu anachukua nyimbo zako anaziuza, wewe msanii unabaki huna kitu. Mimi nakutegemea sana pamoja na Serikali yangu, ninaamini hili mtalisimamia. Sitegemei mwaka 2014 tuje tulizungumzie hili. Tuiteni sisi wasanii tutawasaidia na tutawaeleza, msiende kukaa mezani peke yenu, kwa sababu nyinyi hayawahusu, tuulizeni sisi tunaoumia na tunaonyanyasika kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba suala la chombo cha *studio* ambacho kimezungumziwa hapa. Wakati huo Wizara mlikuwa hamjajipanga vizuri. Mheshimiwa Rais hakufanya makosa kupeleka kile chombo kwenye kundi lingine la wasanii. Ni kama mimi Mbunge ambaye naweza nikaombwa, chombo chochote nikapeleka, siwezi kukinyang'anya. Kiendacho kwa Mganga hakirudi. Ninachotaka kuiomba Wizara yako, iandae utaratibu wa kutafuta chombo kingine kwa ajili ya kazi za wasanii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kuna suala la wizi wa kazi za wasanii. Hilo bado halijazungumziwa. Niliwahi kushauri hapa, *studio* zote zinazorekodi kazi za wasanii ni kweli kwamba zinatambulika *BASATA?* Zimesajiliwa kule?

Mheshimiwa Spika, naomba *studio* zote, maana yake ziko *studio* nyingine bubu, kule ndiko tutakakoweza kubanwa zile kazi, maana ukiweka *sticker* bado mtu atanyonya zile nyimbo, ataziweka kwenye *laptop* yake, atampa na mwenzake, atampa na mwingine na wala hutakaa ujue. Lakini *compact* itakuwa ni moja. Zile kazi zitakwenda kwa watu hata zaidi ya kumi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba utaratibu huo uangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nishauri kuhusu vazi la Taifa. Hapa tuna makabila mia moja. Hivi vazi la Taifa hilo linalotafutwa ni la namna gani? Nilikuwa naomba, hakuna kushindanisha watu. Kitafutwe Kitengo, jopo la watu, wakae, walete mavazi ya makabila yote, tuje tuangalie kila Kanda vazi gani linatoka; watu wapewe ruhusa wavae yawe ni mavazi ya Taifa ili kutafuta vazi moja, wapi utalipata na makabila yote mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nizungumze kuhusu ajira za Waandishi wa Habari. Ukweli ni kwamba, Waandishi wa Habari katika vyombo binafsi wameajiriwa kule. Sielewi Wizara kama mnafahamu ni Waandishi wa Habari wangapi wameajiriwa, ni akina nani wanafanya wapi na ndiyo maana unakuta wakati mwingine hata habari nyingine zinatoka kwenye magazeti mnaanza kumtafuta ni mwandishi gani?

Mheshimiwa Spika, naomba vyombo vya habari vya binafsi vitoe orodha na utaratibu wa kuwaajiri Waandishi wa Habari, haki zao na hatima yao hata pale watakapostaafu, maana yake wanafanya kazi wakati mwingine kama kuganga njaa kwa sababu Wizara bado haijafuatilia na kujua ni namna gani wanatendewa na ni namna gani wanapata maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TBC* imekuwa ikionyesha habari ambazo hazionekana vizuri. Ni kweli tumeingia katika mfumo mpya, hatuwezi kurudi nyuma ni lazima tusonge mbele lakini hivi kweli mwaka huu nasikia hamjaitengea kabisa *TBC* fedha. Mimi sielewi labda Waziri atuambie ana mikakati gani ya kuboresha Shirika letu la Utangazaji ili Watanzania waweze kupata habari zilizosahihi kwa sababu fedha ambazo zimewekwa ni kidogo sana. Hivyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana suala hili alizingatie.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kuna Waraka wa Wizara ya Fedha imesambaza ambao umerekebisha Fungu la Habari. Naomba muusome Waraka huo. *(Makofi)*

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Tauhida Galos Nyimbo, Mheshimiwa Mkanga na Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis wajiandae.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Waziri na Naibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyopita tulizungumza mambo mengi na kati yake ilikuwa ni kulinda haki za kazi za wasanii. Tumeona wakifanya kazi, tumeona wakiyatendea kazi na tumeona na hatua zilizochukuliwa. Wanasema taratibu ndiyo mwendo, tunaamini tutafika ambapo tunapatarajia. Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaamini kwamba hamkuwekwa hapo kwa bahati mbaya, mmewekwa hapo na Chama cha Mapinduzi maana aliyewateueni ni Rais wa Chama cha Mapinduzi. Vijana wa Tanzania matumaini yao yote yapo ndani ya Chama cha

Mapinduzi. Ndiyo maana kila siku wanakipa ushindi kwa sababu wanaimani na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

SPIKA: Huyo aliyekaa jirani yako tunaomba asipige makofi maana inaingilia mchango wako. Hebu endelea tusipoteze muda wako.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Tanzania ambao ni asilimia 60 ya Watanzania matumaini yao, akili zao, mitazamo yao yote iko ndani ya CCM na waliopo hapo Waziri na Naibu Waziri wanatokana na Chama cha Mapinduzi. Tunaimani na tunajua kwamba kazi inaendelea na itafanyika.

Mheshimiwa Spika, wasanii leo mliobahatika kuja hapa, mjue yale mengine mnayoona ni sanaa, wanaowateteeni ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi. Ule mwingine ni usanii tena usanii mtupu. Nadhani mnaelewa, ukimkuta mwigizaji mzuri, Mbunge mwenzangu siku moja alichangia, ukimkuta analia na wewe utalia. Kwa hiyo, msije mkalia, ile ni sanaa, hebu ulizeni posho iko wapi? *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wa Tanzania katika suala la ajira, wanahitaji zaidi elimu na elimu wanayoihitaji ielekee kwenye vitendo zaidi. Serikali yetu niiombe, iwekeze kwenye masuala mazima ya elimu kwa vitendo. Vijana wengi wanapomaliza kusoma hawana pa kuelekea, vijana wengi hawana ajira, wanaojikusanya na kuamua kufanya sanaa, Serikali yenu iko pamoja na nanyi na inawasaidia na Wabunge wa CCM kila siku wanalia na wanasema shida zenu na zinatatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wa Tanzania katika suala la ajira Serikali ishughulikie suala la elimu. Nadhani tukiwapa elimu ya uchumi, wakihamasishwa katika suala la michezo, iwe elimu ya uhakika, waelimishwe kujua nini wajibu wao

katika Taifa lao. Vijana matumaini yao yapo kwetu sisi viongozi tuliomo humu. Tunataka vijana waendelee kushughulikiwa kama wanavyoshughulikiwa. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wanahitaji suala zima la sanaa, suala zima la michezo. Suala la sanaa katika nchi yetu, Mheshimiwa Waziri, kweli kuna masuala hayatufurahishi. Unakuta *bar,* pembeni yake kuna shule, kuna vijana wadogo ambao wanasoma mpaka usiku labda darasa la saba au *form four* lakini tunataka Waziri unapokuja hapa utupe majibu, muziki katika *bar* ambazo haziruhusiwi kupiga muziki mpaka usiku, mwisho saa ngapi na Serikali itachukua hatua gani kwa zile *bar* ambazo ziko karibu na shule kuhusu suala la muziki? Niungane na mwenzangu aliyesema kwamba inafika wakati wanawake vijana tunajikuta tunadhalilika, tunakuomba Waziri ukiwa mwanamke mwenzetu, ukiwa dada yetu, ukiwa mama yetu ulichukulie hatua tena za haraka. Hatupendi kuona mambo kama yale yanatokea ndani ya nchi ya Tanzania ambayo ni nchi ya kistaarabu na kiungwana.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kaka zetu, ndugu zetu na baba zetu muache kutuajiri kwa kutaka sisi tujidhalilishe. Tunataka ajira zenu, ngoma na muziki tutacheza lakini muache kutufanya sisi kwenda pale kwa sababu ya fedha zenu mnazotulipa bila ya mavazi yasiyokuwa rasmi. Nakuomba mama yangu Mheshimiwa Waziri katika Wizara hii, katika majukumu utakayoondokanayo hapa, hili lipe kipaumbele. Imekuwa sasa si tamaduni kwetu, imekuwa si haiba nzuri ya Kitanzania, imekuwa ni tishio, unaona tabu kumwambia ndugu yako twende mara moja tukanunue chakula au kitu fulani. Aibu ndani ya *bar*, imekuwa hujui hii *bar* iliyoruhusiwa kupiga usiku, hii inaruhusiwa kupiga mchana, ukienda pale masuala yanayofanyika si mazuri.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala zima la michezo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, suala la *TFF*, si mtaalam sana wa michezo lakini hayo ninayoyasikia kutoka

Zanzibar, naomba niyazungumze. Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, suala la *TFF* tunaomba lifikiriwe kwa kina, mkae chini na Zanzibar ili kudumisha muungano wetu tulionao. Haya matatizo yaliyomo ndani ya *TFF,* yaondoke maana matatizo yapo, hakuna sehemu ambayo haina matatizo. Matatizo yaliyopo, wanalalamikia vitu kama mkataba, wanalalamikia ajira kwa *TFF* kama ni suala la Muungano, hakuna aliyeajiriwa kutoka Zanzibar. Tunaomba Mheshimiwa Waziri mkae chini na Wizara ya Zanzibar inayohusika na michezo, mtizame na muipe vipaumbele, tunataka *TFF* ifanye kazi kimuungano ili tuzidi kuimarisha Muungano tulionao katika suala zima la michezo.

Mheshimiwa Spika, kidogo nigusie suala la habari. Nitoe pole kwa waandishi wa habari waliopata matatizo. Pamoja na suala zima nililolizungumza bajeti iliyokwisha, Mheshimiwa Waziri niliomba kwamba habari zitolewe kwa utaratibu. Ninarudia kwa sababu halikufanyika. Leo unasikiliza taarifa ya habari, ukifungua habari ya mwanzo inatoka ya Mheshimiwa fulani yuko mahali fulani, hatutaki. Tunataka kwanza tuone hotuba ya Mheshimiwa Rais, tunataka kwanza tuone kazi za Mheshimiwa Rais. Hili liko kwenye uwezo wenu, nalizungumza mnanisikia. Tunataka wenye vyombo vya habari wafuate tunavyotaka sisi viongozi wa Chama cha Mapinduzi kwa maslahi ya wananchi wa chama na wananchi Watanzania. Tunataka tuone ikitoka ya Rais, tunataka ije ya Waziri Mkuu, baada ya Waziri Mkuu zije za Mawaziri, kama kuna na Manaibu Waziri waje halafu ndiyo zije habari zingine. Tumechoka kuona habari zinavyokuja msetomseto, hatuzitaki.

Mheshimiwa Waziri, unanisikia na Naibu Waziri unanisikia tunaomba hili mlifanyie kazi, tumechoka mtu muda huna unataka kusikiliza habari kwanza unaletewa habari hata umuhimu haina halafu baadaye ndio unashtukizia Rais anaongea. Sisi tunataka tusikilize ripoti za nchi hii kwanza, tukishawaona hao wengine ndiyo tuwaache waendelee. Maana unakuta vituko kwenye taarifa habari mpaka unacheka, maana huwa vituko vya kwelikweli kwamba fulani wako kwenye mkutano anachokizungumza hakijui,

anazungumza hotuba za Bungeni kwamba bajeti, bajeti; si unawawakilishi wako kwenye bajeti humu si wanazungumza au wanatoka hawakai Bungeni. Sasa unakwenda kuzungumza na wananchi badala ya kuzungumza na Wabunge...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU SPIKA: Namwita sasa Mheshimiwa Mkanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Khamis, Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya na Mheshimiwa Kamata anaweza kufikiwa.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo katika hotuba ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kupongeza kwa ujumla Serikali kwa upande wa michezo jinsi inavyojitahidi angalau kuongeza aina ya michezo ambayo nayo inapaswa kuwa na hadhi yake kwa kujaribu kutuletea makocha kutoka nje na kuhimiza tu kwamba wananchi tusishikilie tu *football* lakini na michezo mingine tuyaendeleze. Hilo nalishukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naanza na lugha ya Kiswahili. Mimi tangu tukubaliane hapa kupitisha Azimio la Kamisheni ya Kiswahili kuwa nchini kwetu, nilitegemea kwamba angalau katika hotuba hii nitapata fununu na maelekezo kidogo kwamba Kiswahili kitaelekeaelekea kuenziwa zaidi ndani ya nchi yetu kuliko ilivyo sasa. Kwa nini nasema hivyo? Ninasema hivyo kwa sababu naona bado pamoja na kwamba BAKITA wamejitahidi sana kuandaa misamiati na kutunga hata Kamusi mpya lakini bado lile wazo la kusema Kiswahili kiwe

lugha ya kufundishia kwa *level* fulani ya elimu, naona kama haipo kabisa.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mwalimu, ndiyo kilikuwa kibarua changu tena kwa miaka mingi, bado naendelea kuamini kwamba mtoto katika ngazi yoyote ile ukimfundisha kwa lugha anayoielewa zaidi, anafanya vizuri kimasomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naloomba, sio kwamba Kiingereza kitupwe, mimi nashauri Kiswahili kitumike kwa ngazi zote za elimu nchini hapa kwa sababu misamiati ya kutosha sasa upo kwa kila somo na Kiingereza kiwe ni kipindi au lugha ya lazima kuisoma tangu mwanzo mpaka mwisho ili tuje tuwapate wataalam wa masomo mengine watakaokwenda nje na kufanya mambo mengine. Ndicho nachopenda kushauri kwa vile naona nchi nyingine Kiswahili wanakithamini sana na wanaenda harakaharaka kuliko sisi wenyewe. Hii Kamisheni ilikuwa fursa nzuri ya sisi kujitanua kwa kuendelea kukiimarisha.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na *debate* kubwa, Kiswahili hakifai, hakina misamiati wa masomo lakini jamani hebu tuanze, mimi siamini kwamba mpaka sasa hivi Kiswahili hakina misamiati ya kutosha, mbona naisikia? Hasa tukisikiliza vile vipindi vyao vile, jifunze Kiswahili, mbona nasikia maneno magenimageni hata ya biolojia, kemia na masomo mengine? Kwa hiyo, ulikuwa ni ushauri wangu kwamba hii Kamisheni tuliyoikubali iwepo ndani ya nchi yetu na wenzetu wametuamini jamani hebu tuifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza BAKITA wana somo la ukalimani. Wanafundisha Wakalimani na kwa mwaka huu wa fedha imesemekana kwamba watajikita kuongeza maarifa kwa Walimu wa Kiswahili. Labda hiyo itatusaidia sasa kuandaa Walimu wa Kiswahili wazuri zaidi kuweza kufundisha watoto kwa hilo ninalolifikiria kwamba linaweza likatusogeza mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya michezo. Nimeshasema, napongeza Serikali kwa kuanzisha michezo mingi, lakini hapa napenda kuzungumzia michezo ya watu wenye ulemavu. Kwa miaka ya hivi karibuni, wanaokwenda kwenye michezo hii ya watu wenye ulemavu ambayo inaitwa *Para Olympic,* walikuwa wanashinda vizuri tu. Utakuta timu za wazima wanatoka kapa lakini hawa wanakuja na medali zao nyingi tu. Kwa hiyo, mimi ningeomba wangeendelezwa kuhimizwa hawa. Kinachotokea ni kwamba wanapojiandaa kwenye kambi za michezo hiyo mbalimbali, usaidizi unakuwa mdogo sana. Vifaa vyao hawa ni maalum kwa michezo yao hivyohivyo ilivyo maalum, wanaipata kwa shida. Kambi zao zile hazina usaidizi wa kutosheleza, kwa mfano vyakula vinavyohitajika lakini wanaendelea hivyohivyo na chama chao walichounda cha *Para Olympic* na hatimaye wanaleta sifa ya nchi kwa sababu huwa wanaleta ushindi wa kutosha tu.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nakiomba kwa hawa; wengi wanatoka shuleni lakini wakishamaliza elimu yao kwa mfano darasa la saba au la kumi na mbili; hivi Serikali inaendeleaje kuwaendeleza hawa? Kwa sababu kama ni kusaidiwa, hawa ndiyo wanapaswa kusaidiwa kabisa kwamba katika michezo wanayoiweza iwe ndiyo mahali ambapo wanaweza kujitegemea kupata kipato. Wenye ulemavu mnajua wana shida, wana matatizo. Kama watu wazima wana matatizo, watu wenye ulemavu wana matatizo mara tano ya hayo matatizo. Kwa hiyo, wanapomaliza masomo yao, hizi timu ziendelezwe kusudi waweze kujitegemea. Kuna yule mkimbiaji wa Afrika ya Kusini pamoja na kwamba sasa hivi ana matatizo ya kesi na nini; yule baba mpaka leo anachuma fedha kutokana na kukimbia hana miguu sijui amewekewa vitu gani lakini anajimudu na ni tajiri wa kutosha. Kwa hiyo, hawa waendelezwe ndiyo ombi langu. Sio tu wakishaleta medali, wakimaliza shule wanatupwa pembeni halafu wala hawajaliwi wala kufuatiliwa kwamba wako wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru *TBC* inafanya kazi nzuri na nimeona hapa kilio na nini wameongezewaongezewa;

hazitoshi lakini mwanzo mzuri. Ni mategemeo yangu kila mwaka tutaendelea kuwaongezea pesa za bajeti ili kweli shirika hili liwe mbele zaidi kuliko hata ya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, *TBC* ndiyo hawa wanatuelemisha, tunapata habari na nini; ninaomba pawe na kitengo maalum cha lugha ya alama ndani ya *TBC*. Wenye ulemavu viziwi hawalewi wanaona tu vituvitu kwenye *TV* humo. Mbona nchi nyingine wanaweza? Tukitafuta watu wawili watatu, *specialist* wa haya mambo, inaweza ikasaidia, basi angalau hata taasisi yetu ya umma hii ionyeshe mfano kama taasisi zingine zinaona ni shida. Hawaelewi lakini taarifa tunazopewa ni muhimu na hili ndilo Shirika la Umma. Basi lichukue nafasi hiyo ya kuhudumia wote kabisa katika ujumla wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia limeshasemwa kuhusu vazi la taifa. Mimi tangu niingie humu Bungeni nasikia habari ya vazi ya taifa kila siku. Hivi ni lini sasa habari ya vazi la Taifa itakamilika. Inapendeza tunapowaona wenzetu wa Nigeria, sijui wa wapi; wanatoka kila mahali na mavazi yao yale maalum na yanasaidia kujitambulisha kwamba huyu mtu ukiona hivyo unajua ni Mnaigeria. Sasa kwa sisi Watanzania kwanza tujitambulishe na lugha yetu na mavazi ambayo tutakutwa tumeamua. Mwingine amesema ni vigumu, lakini mimi niliona mashindano yalishafanyika, mchakato huu ulishakuwa mrefu mno, unamalizika lini? Tufike mahali tumalize ili tuelewe kwamba hiki kinakuwa namna gani.

Mheshimiwa Spika, mimi sikuwa na mengi, *Para Olympics* tafadhali wawezeshwe, wale Walimu wanaowafundisha na angalau wapewe hata faraja pale wanaporudi wamekwishashinda.

Mheshimiwa Spika, la pili *TBC* kuwa na kitengo cha lugha ya alama. Hayo mengine nimefanya kuchombezeachombezea kuyaingizia kwa sababu Wizara yenyewe ina mambo mengi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga hoja mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya, Mheshimiwa Vicky Kamata na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na mimi naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa salama na kuwa hai na kudiriki kuchangia hotuba hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi moja kwa moja naenda kwenye timu ya Taifa *(Taifa Stars),* timu ya mpira wa miguu ya Tanzania. Timu ya Taifa ya Tanzania ni ya Watanzania wote, ni timu ya Muungano ya Zanzibar na Tanganyika yote. Nafahamu vyema kuwa wanaochaguliwa kwenye timu ya Taifa wanachaguliwa kwa mujibu wa vipaji walivyo navyo, uchezaji wao mzuri, vipaji vizuri ndiyo vinawapeleka kuchezea timu ya Taifa na taratibu zote zinazotumika lakini haziwatendei haki Wazanzibar kutokana na kuwa ile timu ni timu ya Taifa, Wazanzibar hawapati haki vizuri katika kuchaguliwa wachezaji wa timu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu zifuatazo, kocha wa Timu ya Taifa ya Tanzania anaangalia *Vodacom,* Ligi Kuu ya Bara peke yake ambamo ndimo wanamochaguliwa wachezaji wa timu ya Taifa, Ligi ya Zanzibar haiangalii. Sasa wachezaji wanaopata nafasi kuchezea Timu ya Taifa ya Tanzania, ni wale ambao wako Bara wanachezea vilabu kama Simba, Yanga na vilabu vikubwa vingine lakini wale wanaocheza Ligi Kuu ya Zanzibar hawaonekani kwa hiyo hawatendewi haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linasababisha matatizo ndani ya ligi yetu ya Tanzania utakuta kocha wa timu ya Taifa ya Tanzania ameletwa kwa mujibu wa Tanzania nzima lakini kocha huyuhuyu ndiye anayechaguliwa kufundisha timu ya upande mmoja wa

Kilimanjaro Stars. Sasa huyu kocha akifundisha timu hii ya Tanzania Bara inakuwa kama timu ya nyumbani kwake. Kwa hiyo, mara nyingi atapendelea wachezaji ambao anahisi ni wa nyumbani kwake wale wa *Zanzibar Heroes* ambao wako Zanzibar hawaonekani kabisa. Kwa hiyo, jambo hili liangaliwe kwa upana na liangaliwe vizuri namna gani tutaboresha mchezo wetu wa mpira kwa kushirikisha wachezaji wote. Zanzibar kuna wachezaji wazuri vilevile na wana uwezo wa kuchezea timu ya Taifa lakini kutokana na hizi taratibu zinazotumika hawapati nafasi, tunawaonea.

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapa sasa nakuja kwenye uwanja wa Taifa Dar es Salaam ingawaje Wabunge wengine waliosimama hapa wamesifu sana ukusanyaji wa mapato na shilingi milioni 500 zimekusanywa lakini pamoja na hilo mimi nimeshiriki mchezo wa tarehe 18 kati ya Simba na Yanga, kuna ubovu mkubwa unaosababisha mianya ya kupotea mapato hayo. Kama zimekusanywa shilingi milioni 500 basi shilingi milioni 100, shilingi milioni 200 zimekwenda mifukoni mwa watu wengine, utaratibu huu siyo mzuri. Nimefika pale saa nane za mchana lakini hakuna gari lolote linalouza tiketi kwani tiketi zimekwisha zote zilizobakia ni za ulanguzi watu wanapitisha kuuza kwa bei ambayo siyo ya sheria. Tiketi ya shilingi 5000 pale ilikuwa inauzwa shilingi 10,000.

WABUNGE FULANI: Eeeh.

MHE.YUSUPH HAJI KHAMIS: Ya shilingi 7000 inauzwa shilingi 15,000, zimepanda kama hivyo, hakuna gari yoyote inayouza tiketi lakini watu wanauza tiketi kiulanguzi pasipo aibu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziliuzwa tiketi mpaka zile za mikononi zikaisha ikawa mbinu za kuingia ikawa wanakusanywa vijana kama watano mpaka sita wanapelekwa mlangoni, fedha watu wanaingiza mfukoni. Sasa nikajiuliza sasa kama hawa wanajaribu kujitetea kuwa wameuza *level seat* ya kiwanja kilivyo hawa wanaoingia kwa makundi wanakwenda kukaa wapi?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo siyo zuri, vijana mamia kwa mamia walikuwa wanakiuka uzio ule, wanatumbukia ndani na hakuna anayerejeshwa hata mmoja wote wamekwenda uwanjani. Kwa hiyo, pale *TFF* uwezo wake wa kukusanya mapato ni mdogo na mapato siyo kwamba yalikuwa ya kukusanya yalikuwa ni ya kuzoa. Sasa Chama cha Mpira Tanzania kinashindwa kuzoa yale mapato ili kuendeleza michezo Tanzania, sijui watapata wapi fedha wakati mwingine, watakuwa wanalalamika tu kwa sababu siku hiyo ilikuwa za kuzoa, watu waliokuwa nje wengi tiketi hawana, walioko ndani chungu nzima, watu wanauza tiketi kwa maslahi yao. Kwa hiyo, hili jambo Mheshimiwa Waziri ninataka aliangalie kwa upana wake, kwa sababu pamoja na kuendeleza michezo, kama watu wanafanya uzembe katika kukusanya fedha sijui wataendeleza vipi michezo.

Mheshimiwa Spika, sasa naenda kwenye utoaji wa vibali kwa vyombo vya habari. Simu za nyuma palifanyika kongamano kubwa sana katika kiwanja cha Taifa kuhusu kuichangia Redio Imani. Wananchi mbalimbali, viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa, viongozi wa Kitaifa wamekwenda pale kuichangia Redio Imani ili iwezeshwe na yenyewe irushe matangazo yake. Jambo hilo lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, *TV* Imani, samahani sana ulimi kidogo umepotea, ni *TV* Imani. Viongozi wa *TV* Imani wametekeleza majukumu yao yote, wamelipa chombo kinachoitwa *TCRA* lakini cha kushangaza mpaka leo *TV* ile bado haijaruhusiwa kurusha matangazo yake, sijui imekwama wapi. Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa unieleze kwa vizuri sana jambo gani lililosababisha *TV* Imani mpaka leo isirushe matangazo yake, ni jambo gani lililozuia. Kwa sababu huku ni kuchonganisha, waliochangia pale wananchi wengine ni maskini, wengine ni matajiri lakini wametoa haki zao kwa jambo maalumu walilokusudia. Sasa hivi zinakwenda fitina kuwa viongozi wamekula fedha zile, kwa hiyo tunaingiza mgogoro ndani ya wananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninataka uliweke safi suala hili ili wananchi wa Tanzania wale waliochangia na wale wanaopenda maendeleo ili wajue kuna sababu gani zilizochangia *TV* hii

mpaka leo bado haijaruhusiwa kurusha matangazo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapo sasa nakuja katika vyombo vya habari. Kwa kweli vyombo vya habari, Waandishi wa Habari, ni kioo cha jamii, wanatakiwa wawe kioo cha jamii waelimishe, wahofishe halafu pia wajenge mustakabali wa mbele ya Taifa hili, hiyo ndiyo kazi ya chombo cha habari lakini chombo cha habari kama si hivyo kikienda kinyume na maadili yake basi ni kulipeleka Taifa hili mahala pabaya kwa sababu wao vilevile ulinzi siyo ni kukamata bunduki tu na wao vilevile kalamu yao ni sehemu ya ulinzi, ni silaha ya kulilinda Taifa hili. Kwa hiyo, wanatakiwa wawe *fair*, wasipendelee huku wala huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo kidogo yanakuwa yana utatanishi. Zanzibar kule kulitokea mauaji ya Padri Mushi, vyombo vya habari vikatangaza vizuri, ikapatikana habari vizuri lakini wiki kama moja mbele akauwawa kinyama kabisa Sheikh Ali Khamis Mwakaje akapigwa visu akauwawa, vyombo vya habari vingine wakatangaza alikuwa mwizi wa muhogo, wanapotosha na ni Sheikh wa Ijumaa, anastahiki, ana heshima badala ya kutangaza vile neno lilivyo basi limeharibiwa kwa makusudi tu ili kupoteza heshima yake, hii ni hatari kwa vyombo vyetu vya habari vya Taifa. Wawe wa kweli katika kutangaza habari zao, wasitanagaze kwa utashi. Ukiangalia hapahapa Bungeni, anaweza kusimama Mbunge akatoa hoja safi, hoja ya kitaifa lakini habari zake usizisikie lakini akatokezea Mbunge ambaye anasimama tu hapa anaomba Mwongozo utaona waandishi wa habari *kukurukukuru* wanakuja, wanashughulika sijui tunakwenda wapi, wengine wanakosa haki kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mbunge atoke nje tu hapo akiwa maarufu na mkoba wake utamkuta kwenye magazeti kachukua mkoba, wale wanaochangia humu hoja safi, huzisikii hoja zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hawa Waandishi wa Habari kwa kiasi kikubwa bado na wao wana matatizo yao,

wanatakiwa kujirekebisha. Wafanye kazi yao kwa mujibu wa maadili yao yanavyowaruhusu lakini kama watafanya kazi zao kwa upendeleo basi Taifa hili watalifikisha pabaya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nimalizie kwa tukio moja. Juzi Arusha kulitokea ugaidi. Ugaidi ule uliotokea Arusha Waandishi wa Habari wameandika habari zao kwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante kengele yako ya pili hiyo.

Sasa ni Mheshimiwa Neema Mgaya, atafuatiwa na Vick Kamata na Mheshimiwa Cecilia Paresso atafikiwa pia.

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, mimi nitajikita zaidi kuzungumzia tatizo la ajira kwa vijana lakini pia kuishauri Serikali ni mikakati gani ya kufanya ili kuweza kutatua tatizo hili la vijana ukizingatia kuwa tatizo la vijana ni la kidunia na nchi nyingi zimekumbwa na tatizo hili la vijana. *Job report* inaonyesha kuwa tatizo la ajira sasa limefikia 8.7% mwezi Aprili mwaka huu na kwa kule Marekani tatizo hili limepungua kufikia 7.5% mwezi Aprili kutoka 7.6 Machi na kwa Tanzania sasa tatizo hili la ajira liko 10.7%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua mchango mkubwa unaofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kupambana na tatizo la ajira kwa vijana. Imeweka mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwatayarisha vijana ili kuweza kujiajiri wenyewe na vilevile kuwaajiri wenzao. Vilevile imeweka Idara ya Maendeleo ya Vijana na pia tumemsikia Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hotuba yake kwamba sasa kuna baadhi ya Mikoa mingi Tanzania

wameshapeleka Maafisa wa Vijana kwa ajili ya kusaidia vijana kwenye Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imetuwekea Mfuko wa Vijana ili uweze kusaidia maendeleo ya vijana. Mwaka wa bajeti uliopita ziliwekkwa shilingi milioni 100 lakini sasa hivi imetungozea mpaka shilingi bilioni tatu. Tunaishukuru Serikali lakini bado nasisitiza kuiambia Serikali kuwa Mfuko huu ni muhimu wasiufanyie mzaha kwa sababu unasaidia vijana walio wengi ukizingatia kuwa vijana Tanzania ni takribani 60%. Kwa kuboresha Mfuko huu utasaidia kuboresha *SACCOS* za vijana lakini vilevile utasaidia kukuza mitaji ya vijana waliounda vikundi vyao, wale wanaotoka vyuo vikuu lakini vilevile kuna vikundi vya vijana vinavyoshughulika na masuala ya kilimo kwenye Mikoa mingi ya Tanzania ukizingatia vijana wengi wa Tanzania wako Mikoani. Hivyo basi, ninaomba Serikali iuchukulie kwa makini na kwa umuhimu mkubwa Mfuko huu wa Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze katika kuishauri Serikali jinsi gani ya kuweza kutatua tatizo hili la vijana katika suala zima la ajira. Hivi sasa tumekuwa tukiwasahau sana vijana ambao wako Mikoani na asilimia kubwa ya Tanzania ni Mikoa, Majiji ni baadhi tu. Kule Mikoani kuna miradi mingi mikubwa ya kilimo, naishauri Serikali katika ile miradi mikubwa ya kilimo kuwe na *outgrowers,* Serikali iweke *program* ya *outgrowers* kwa vijana kwa sababu vijana watakuwa na uhakika wa masoko lakini vilevile uhakika wa *services.* Kwa hiyo, vijana wataendelea kukaa kwenye maeneo yao yale ya Mikoani na kufanya shughuli za kilimo. Kwa mfano kama kule Kirombero kwenye mashamba ya miwa, Njombe, pareto kuna chain na Iringa pia, kule Tabora kuna tumbaku, Kilimanjaro Kahawa, Kanda ya Ziwa kule kuna pamba, hivyo Serikli ikitengezeza hizi *program* za *outgrowers* kwa vijana kwenye miradi mikubwa ya kilimo vijana watakaa kule na kufanya shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia Serikali iendelee kusisitiza matumizi ya bidhaa zinazotoka ndani ya nchi yetu. Hii itasaidia kukuza uzalishaji na vilevile wale ambao

wanashughulika na shughuli za viwanda watapata moyo kwa sababu wanakuwa na uhakika wa soko na hivyo basi kukua kwa uzalishaji ajira nayo itakuwa, vijana wetu watapata ajira katika viwanda.

Mheshimiwa Spika, tuchukulie mfano mdogo tu tukiamua kuwa shule zote za sekondari, shule zote za msingi, Majeshi na hata CCM pia tukaamua kuvaa nguo zinazotengenezwa na pamba ya Tanzania, zinazotengenezwa hapahapa Tanzania, hii itatoa fursa kwa vijana wetu kupata kazi katika viwanda hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iendelee kupanua wigo wa kuajiri wakandarasi katika sekta mbalimbali, wakandarasi hao watoke humu Tanzania sababu vijana wetu wanaomaliza vyuo vikuu watapata fursa ya kupata kazi.

Mheshimiwa Spika, niiombe pia Serikali isaidie vijana katika suala zima la kuweza kukopesheka. Vijana wengi hawana uwezo wa kuweza kukopesheka kutokana na masharti magumu ya mikopo. Hivyo basi naishauri Serikali, kwa nini isitumie vitambulisho vya Taifa na vyeti vyao iwe kama dhamana ya wao kuweza kukopesheka kwa sababu vijana wako tayari kujiajiri na kijana mmoja anapoamua kujiajiri, ina maana atatoa fursa ya ajira kwa vijana wengine katika shughuli zake hizo ambazo ameamua kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kutoa uhuru kwa vyombo vya habari lakini vilevile niwakumbushe Waandishi wa Habari kuwa wao ni chombo muhimu sana na kama chombo hiki watakitumia vizuri baadaye Waandishi wa Habari wanaweza kuwa ni mhimili usio rasmi. Linapotokea tatizo Serikali inawaomba wao jamani tunaomba mtusaidie kama vile ilivyo kwa viongozi wa dini lakini kama watakuwa hawatumii vizuri *professional* yao katika kupeleka habari njema na za ukweli ambazo siyo za upotoshaji, hawatoweza kufikia heshima hiyo kama waliyonayo viongozi wa dini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niikumbushe Serikali zile 5% katika kila Halmashauri zinazotokana na mapato ya Halmashauri ziende kwa vijana kama ilivyokusudiwa. Hii ni sheria lakini tumeona kuwa Halmashauri nyingi zile 5% zinazotokana na mapato ambazo zinatakiwa ziende kwa vijana, vijana hawa hawapatiwi, siyo kusema Halmashauri imepata pesa ndogo, hapana, mapato yoyote yale lazima 5% itolewe ipelekwe kwa vijana ili iende kusaidia vijana huko kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nimalizie kwa kusema kwamba kuna baadhi ya vijana ambao wameamua kujiajiri kwenye fani ya muziki na filamu. Naiomba Serikali isaidie vijana hawa katika kulinda haki za kazi zao kwa sababu kama kijana ameshajitoa mhanga mwenyewe, amehangaika ameamua kuwa mwanamuziki, ana-*act* hizo filamu, mchango mkubwa wa Serikali hapo ni kuwasimamia katika kuhakikisha kuwa wanapata haki zao za msingi lakini vilevile ku-*deal* na wale ambao wanapora fani hizo za wasanii ambao wanafanya ujangili katika kazi hizo za wasanii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Vick Kamata, Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba wajiandae.

MHE. VICK P. KAMATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuanza kwa kusema kuwa ninaunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitaanza kuzungumzia jina la Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Mimi naona kuwa Wizara hii ni kubwa sana, inawaelemea hawa waliopo sasa.

Nisingependa kuongea sana, naomba nitoe ushauri na nitaomba ushauri wangu uzingatiwe. Naomba Vijana wakapelekwa kwenye Wizara ya Kazi na Ajira. Habari ikapelekwa Wizara ya Sayansi na Teknolojia kwa akina Mheshimiwa Mbarawa na Mheshimiwa January Makamba *then* ikabaki Michezo na Utamaduni kwenye hii Wizara na ikaweza kufanya kazi vizuri kabisa kwa ufanisi unaokidhi haja za Watanzania. Langu ni hilo katika ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, la pili, napenda nizungumzie pia kuhusu soka na niishauri Serikali ni kwa namna gani inaweza ikafanya soka la nchini kwetu likaweza kutuingizia pesa. Korea ya Kusini ilikuwa haitambuliki kabisa katika ulimwengu wa soka duniani mpaka mwaka 1999 iliposhinda na kupata nafasi ya kuandaa Kombe la Dunia mwaka 2002. Mara baada ya Kombe hilo la Dunia kuchezeshwa Korea ya Kusini, kilichofanyika ni kwamba Korea ya Kusini ilichagua vijana ambao wana-*talent* ya mpira, wakawapeleka kusoma nchi mbalimbali, mfano Spain, Italy na German. Vijana wale walipopelekwa kusoma, waliporudi walikuwa ni wazalendo kwelikweli na walihakikisha wanafanya kazi nzuri kuhakikisha kwamba wanainua soka ya nchini kwao na ndiyo maana mpaka leo Korea ya Kusini tunai-*salute* kwamba ni miongoni mwa nchi ambazo zinafanya vizuri sana katika soka.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuiomba Serikali, kwa nini sasa tusione kwamba ni muda muafaka na sisi kuchukua vijana wetu waliomaliza vyuo vikuu, *form six* tukawapeleka nchi kama Spain na Italy kusoma kule, wakirudi tuwe na vijana ambao ni wazalendo kwelikweli siyo waende kule wazamie, hapana, waende kule wasome wakati wale wanasoma Serikali inajipanga kujenga Chuo cha Makocha hapa nchini, watakaporudi wale vijana, wengine waje kuwa wakufunzi katika hicho Chuo Kikuu cha mpira Tanzania, wengine wafundishe hizi timu zetu ndogo na kubwa ili tuweze kuinua soka letu hapa nchini Tanzania. Ninaamini kabisa inawezekana, kama wenzetu waliweza sisi tunashindwa nini? Tunaweza kabisa, tukijipanga vizuri tunaweza, tena nashauri Chuo Kikuu cha Soka hicho kama

kitakubalika kijengwe Geita kwa sababu Geita kuna ardhi kubwa nzuri ambayo haijawa *polluted*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumze jambo ambalo nimeagizwa na wananchi wa Geita. Wananchi wa Geita wamenituma niiombe Wizara hii ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo isikilize kilio cha Wanageita, hatuna uwanja wa kisasa wa mpira. Hivi sasa vijana wanacheza mpira na kombe la Vick Kamata linaendelea kule lakini wanacheza katika viwanja ambavyo havina hata uzio, vumbi tupu, hakuna ile ladha kwamba kweli hawa vijana wanacheza. Naamini kabisa Serikali ikitujengea uwanja mzuri wa kisasa pale Geita, tutakuwa na uwezo wa kukusanya mapato yetu na kujiweka vizuri na sisi kama Mkoa mpya wa Geita. Naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, isikilize sana hiki kilio cha watu wa Geita, wanaomba uwanja mzuri wa kisasa na ninadhani tunastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki tatu zilizopita nilikuwa Geita, niliitwa na Shirikisho la Wasanii wa Geita. Huu ni umoja wa vijana wapatao kama mia tatu na kitu hivi nilizungumza nao, vijana hawa wapo katika kikundi na wanafanya sanaa vizuri kwelikweli, katika hili kundi la watu 300 kuna wanaoimba, kuna wanaoigiza, kuna wachoraji, fani zimekamilika kwa wale vijana 300 ambao wametengeneza umoja wao. Mbali na kwamba ni wanamichezo, wanasanaa, wanafanya pia shughuli zingine za kijamii, mengi nimeandika kwenye mchango wangu wa maandishi nimeuleta hapo nadhani utakuwa upo njiani au umeshawafikia, wameomba Serikali iwasaidie, iwape nyenzo za kufanyia kazi. Wale ni vijana ambao wanahitaji kusapotiwa, wameshajitoa tayari. Kwanza kile kitendo cha kuungana pamoja kinaonesha kwamba ni watu ambao wapo *committed* na wanasikilizana na watu wakiweza kukaa pamoja wanaweza kufanya jambo likafanikiwa sana. Kwa hiyo, mimi ninawapongeza kwanza hawa vijana wa Shirikisho la Wasanii Geita kwa kuweza kuungana pamoja na kuamua kuanza kufanya shughuli zao kwa pamoja namna hii. Kwa hiyo, naiomba

Wizara iwaangalie na iwasikilize maombi yao nimeyaleta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na kwamba wanafanya shughuli za sanaa kama nilivyosema pale mwanzo lakini pia wanajishughulisha na kazi za usafi. Wanaomba Serikali iwasaidie wapate vitendea kazi, wanafanya usafi kwenye hospitali, sokoni na sehemu nyingine mbalimbali. Mimi binafsi nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iwasaidie hawa vijana nyenzo za kutendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine katika hiki kikundi wanafuga kuku, walikuwa wanaomba *incubator* kama Serikali inaweza na ninaona hapa kuna pesa kidogo itakwenda kule, ninaomba hii pesa iwaangalie hawa wasanii waliojiunga 300 lakini pia isiwasahau na wale wengine ambao hawapo kwenye hili Shirikisho la Wasanii Geita.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kama ambavyo nimetumwa na vijana waliomaliza Vyuo Vikuu Geita, sijasema kwamba Chuo Kikuu kipo Geita lakini kuna vijana ambao wamesoma Vyuo Vikuu mbalimbali Tanzania sasa hawana kazi wapo pale Geita, wamenionesha vyeti vyao, wanazo sifa kabisa, lakini kwa kuwa tunajua kwamba ajira hakuna wanaomba sana watumie vyeti vyao waweze kukopesheka. Mimi nashindwa kuelewa hivi inakuwaje Serikali inashindwa kuongea na mabenki yakapunguza hizi riba? Hivi inawezekanaje unasema unataka kumsaidia kijana wakati unampa riba kuanzia asilimia 18 mpaka 24, huyu mtu hiki si ni kitanzi? Wewe unasema unamsaidia au unamwuua? Kwa sababu kama mtu atakopa aambiwe kwamba atalipa riba kwa asilimia 20 mpaka 24 wewe unamsaidia au unamwua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ione ni namna gani itawasaidia kwa sababu tayari tunajua tatizo la ajira lipo dunia nzima, sisi kama Tanzania tumejipangaje kuwasaidia hawa vijana wetu kuondokana na tatizo hili? Naiomba sana Wizara na Serikali iwasaidie vijana hawa

waliomaliza Vyuo Vikuu waliopo Geita ambao hawana kazi, wamenituma nije kuomba sana watumie vyeti vyao kupata mikopo yenye masharti nafuu ili waendelee na shughuli zao za Bodaboda, *Noah*, nashukuru Serikali imeruhusu, waendelee na shughuli zao ili wasifanye vurugu mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtu wa ajabu sana nisipoipongeza *Taifa Stars*. Naipongeza sana *Taifa Stars* kwa kazi nzuri ambayo inafanya. Pia pengine niwaambie wale ambao watakuwa hawana taarifa kwamba *Taifa Stars* sasa imebakiza mechi mbili tu ikishinda tunaingia na sisi kwenye Kombe la Dunia. Ni sifa kubwa sana. Je, Serikali mmejipangaje kuwasapoti hawa Taifa Stars kwa hizi mechi mbili zilizobaki washinde ili na sisi tuwe kidedea? *Yanga big up* siku zote ninaipa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali na Watanzania wote tuiombee *Taifa Stars* iweze kuingia kwenye mashindano ya Kombe la Dunia mwakani kwa sababu zimebaki mechi mbili tu. Kama huku kote wamepita vizuri, hizi mechi mbili jamani tukipita sisi Tanzania mbona tutakuwa juu sana! Hata kama tutaenda tukaonekana tumecheza, siombi kwamba tushindwe kufika hata robo fainali, lakini *at least* tuonekane na sisi Tanzania tumeingia *World Cup*. Mimi nafikiri ni heshima kubwa sana watakuwa wametupatia *Taifa Stars*. Ninawaomba Watanzania wote kupitia Bunge hili tuwaombee *Taifa Stars,* lakini zaidi niiombe Serikali ifanye inavyojua kuwapa moyo hawa hizi mechi mbili zilizobaki waweze kushinda ili Tanzania iingie kwenye ramani kwamba na sisi kumbe tunajua kulisakata kabumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijagongewa kengele, napenda sana na mimi nizungumzie mgogoro uliopo kati ya dada yangu kipenzi Lady Jaydee na Ruge Mutabaha. Mimi ninatambua kabisa Ruge ana mchango mkubwa sana kwa vijana kwa kutoa ajira. Watanzania wanajua mchango mkubwa wa Ruge Mutabaha na wasanii tunaowapenda tunawasikiliza kwenye nyimbo zetu masaa 24, ni wale ambao wametokana na *THT*. Kwa hiyo, Lady Jaydee mwenyewe pia

ametokana na hao sijui kama ilikuwa *THT* au sivyo, lakini nafahamu *Lady Jaydee* ni mwanamke shupavu, ni mwanamke ambaye ana moyo, anaweza akakasirishwa akaumizwa, lakini pia anaweza akakaa chini akasema kwamba hapa duniani tunapita, haya mambo huwa yanatokea, awe na moyo wa kusamehe. Nimwombe na kaka yangu Ruge mambo ya kupelekana Mahakamani, kwanza atampotezea muda huyu dada wa watu badala ya kufanya kazi yake nzuri, tunaipenda kazi yake, mambo ya kwenda tena Mahakamani, amlipe Mwanasheria, afanye hivi mwisho anafilisika, hatutaki kumwona Lady Jaydee anakuwa maskini. Tunaomba Ruge na Lady Jaydee wakae, Serikali iwasaidie wamalize mgogoro wao, wafanye kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante, muda wako umekwisha.

MHE. VICK P. KAMATA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: *Okay*, sasa nimwite Mheshimiwa Cecilia Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kutoa mchango wangu kwa kuelezea suala la uhuru wa kutoa maoni na kujieleza. Tunatambua umuhimu wa kutoa maoni na kujieleza kama ni haki mojawapo ya msingi ya binadamu, kama ambavyo Azimio la Afrika kuhusu Kanuni...

SPIKA: Labda uhame kabisa mstari huo.

(Hapa Mheshimiwa Mbunge alihamia katika kipaza sauti kingine)

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nianze kuchangia kwa kueleza suala la uhuru wa kutoa maoni na kujieleza, tunaelewa kwamba suala hili ni haki ya msingi ya mtu kuzungumza na kutoa maoni yake bila kikwazo chochote. Pale inapobidi kunakuwa na vikwazo basi vikwazo hivyo ni lazima viwe dhahiri na viweze kuwepo kwa uhalali bila usumbufu wowote. Azimio la Kanuni za Uhuru wa Kujieleza katika Afrika mwaka 2002, zinaeleza kuwa uhuru huu wa kutoa maoni ni haki ya msingi ya binadamu na ni lazima iheshimiwe na nchi zote wanachama lazima wazitilie mkazo. Haya yapo pia katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara ya 18 ikieleza uhuru huu wa kutoa maoni na kujieleza.

Mheshimiwa Spika, lakini kivitendo suala hili limekuwa halitekelezeki. Halipo kwa sababu hatuna sheria yoyote ambayo inatetea suala zima la kutoa maoni na kujieleza kwa Mtanzania yeyote. Hivyo, ni wakati sasa wa Serikali kuona umuhimu wa kuleta sheria hii ya kulinda haki ya wananchi katika kutoa maoni na katika kujieleza.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni haki ya kupata taarifa. Wananchi wengi hawafaidiki na haki hii ya kupata Taarifa kama ambavyo Katiba pia inaeleza katika Ibara ya 18. Nyenzo pekee inayotumika hapa nchini katika kupata habari, ni kupitia magazeti, televisheni na redio, lakini wananchi wengi waliopo vijijini hawana uwezo wa kununua vitu hivi. Wananchi hawana uwezo wa kununua televisheni wala uwezo wa kununua magazeti.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na Tanzania *Human Report* ya mwaka 2011 inaonesha ni asilimia tano tu ya Watanzania ambao wanapata huduma ya televisheni na ni asilimia moja tu ya Watanzania wanaoweza kupata huduma ya *internet*. Wananchi wengi wanakosa fursa hii lakini tunaelewa kwamba kupata habari ni haki ya msingi kabisa katika maendeleo na demokrasia lakini pia inawafanya wananchi waweze kuwa na uhakika wa habari wanazozipata ili mwisho wa siku waweze kuiwajibisha Serikali lakini na kuwawajibisha pia viongozi wake. Katika hotuba

ya Waziri ameonesha kwamba wanatarajia kuwa na Sheria ya Haki ya Kupata Habari ambapo wanasema utafiti unaendelea, ni lini? Lazima tuwe na *timeframe*, mnaweza mkatuambia sasa hivi kwamba utafiti unaendelea, mnataka kujifunza katika nchi mbalimbali lakini mpaka lini? Lazima mtuambie *timeframe* yake inakuwaje.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976. Sheria hii sasa imekuwa ni kama sheria kuu ya vyombo vya habari inayotawala Tanzania lakini sheria hii imepitwa sana na wakati, ni sheria ambayo ipo tangu enzi za ukoloni, ni sheria ambayo ilikuwa inatumika wakati wa mfumo wa chama kimoja, leo tupo katika mfumo wa vyama vingi, ni lazima tuwe na sheria ambayo itatoa fursa na inaweza kukubalika katika mfumo huu wa vyama vingi tulionao sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, sheria hii ina vikwazo mbalimbali na inampa Waziri mamlaka makubwa sana. Kwa hiyo, ni lazima mtuambie ni lini sheria hii itafanyiwa marekebisho? Mwaka 1992, Tume ya Nyalali ilishaeleza kufutwa kwa sheria zote mbaya ikiwemo hii, lakini sasa hivi ni zaidi ya miaka 20 hatuoni nia dhahiri ya Serikali hii kutaka kubadilisha sheria hii. Serikali ituambie ni lini mabadiliko haya ya sheria yatafanyika ili tuweze kuwa na uhuru huu wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Waandishi wa Habari. Waandishi wa Habari siyo maadui, Waandishi wa Habari ni ndugu zetu, wanafanya kazi kwa niaba ya taasisi za umma, kwa niaba ya taasisi binafsi, kwa niaba ya wananchi wote lakini Waandishi hawa wa Habari wamekuwa na changamoto nyingi. Waandishi wa Habari wanapopata ajira hasa katika sekta binafsi hawana mikataba ya ajira, mwisho wa siku hata akinyang'anywa haki yake anakuwa hana kitu ambacho kinaweza kumsaidia kuweza kudai haki zake kwa sababu hakuna mikataba ambayo inaeleweka. Ni muhimu sana sasa kwa Serikali kutambua na kutuambia wana mkakati gani wa kulinda Waandishi wa Habari Tanzania ili wafanye kazi zao katika mazingira rahisi bila

vikwazo vyovyote na unyanyasaji wote ambao wanapata Waandishi wa Habari mtuambie nini mkakati wa kuwalinda Waandishi wa Habari katika nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la kazi za wasanii nchini. Wasanii ni hazina ya nchi, tunapaswa kuthamini na kutambua kazi zao na kuheshimu mchango wao. Tunaona katika nchi mbalimbali zilizoendelea jinsi ambavyo wanawaenzi na kuthamini wasanii wao, kwa nini ishindikane kwa Tanzania? Ni lazima tufike mahali sasa tuone umuhimu wa wasanii hawa, tuwathamini na kujali kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuzungumzia suala la mfumo wa analojia kwenda digitali. Pamoja na umuhimu wa kuendana na teknolojia ambayo ipo katika dunia, lakini nimeona kwamba bado wananchi wengi hawajapatiwa elimu ya kutosha ya mfumo huu mpya wa digitali. Tumekimbilia kuzima mitambo katika Mikoa mbalimbali na inaendelea kwa awamu, lakini ni kiasi gani elimu imetolewa kwa wananchi ili waelewe nini kinatakiwa kufanywa sasa hivi katika huu mfumo mpya. Mwananchi leo anaingia gharama ya kununua king'amuzi lakini bado ataendelea kulipa malipo ya kila mwezi kulingana na *channel* anazotaka, huku ni kunyima uhuru wa kupata habari kwa wananchi, huku ni kukiuka Katiba ambayo tumejiwekea sisi wenyewe. Ni vema sasa bora wanunue tu king'amuzi lakini malipo ya mwisho wa mwezi yasiwepo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la mbio za mwenge. Kambi ya Upinzani imeeleza katika hotuba yake kwamba ni vema huu mwenge sasa ukae makumbusho, ni mpaka lini tutaukimbiza? Kuanzia mababu mpaka leo, kwa nini tusiuweke makumbusho, unatumia hela nyingi sana. Katika Wizara yako Waziri umeomba karibu shilingi milioni mia mbili hamsini na tisa katika shughuli hii, lakini huko kwenye Wilaya zetu wananchi wanachangishwa. Sisi tunaotoka Mkoa wa Arusha wanaenda Hoteli za Kitalii wanachangisha hela, Wakuu wa Wilaya wanaratibu hizi shughuli, kama mwenge tumeutengea fedha huku kwa nini kule tena

wanachangishwa? Mpaka Walimu tunaambiwa wanaanza kuchangia shilingi elfu tatu, huu ni unyanyasaji na huu ni wizi! Kwa sababu mwisho wa siku hatujui hata haya matumizi ya hizi fedha za mwenge ambazo zinachangishwa katika Wilaya yanakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisikia mwenge unaenda katika Wilaya fulani shughuli za pale zinaweza zikasimama wiki mbili ama wiki tatu. DC atakimbia kuangalia miradi gani inaenda kupitiwa na mwenge, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Idara, shughuli zote zinasimama, hata huduma kwa wananchi zinasimama kwa sababu ya mwenge. Hatuwezi kuwa tu na utamaduni uliokuwepo huko nyuma na kuiga, nafikiri ni vema kuona sasa mwenge huu ukae kwenye makumbusho iwe kama ni sehemu ya Makumbusho ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la michezo. Wizara inajikita katika suala la mchezo wa mpira wa miguu tu, ni jambo jema lakini ni vema tuangalie na michezo mingine, tuiwekee mikakati. Katika hotuba ya Waziri ametuambia kwamba Rais amekubali kumlipia mshahara Kocha wa kigeni, hivi ni lini tutakuwa na mkakati wa kuwajengea uwezo Makocha Wazawa, tuache kutegemea makocha wa kigeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni sawa kuna umuhimu wake kwa wakati fulani, lakini Serikali ni lazima iwe na mkakati wa kuwajengea uwezo Makocha wazawa. Tunategemea fedha za bajeti kutoka kwa wafadhili lakini hata Makocha pia tunategemea kutoka nje, hii ni aibu kabisa kwa Serikali. Lazima tuondokane na mfumo huu, tuache suala la kuwa tegemezi kuanzia kwenye fedha mpaka watu, ni aibu sana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kuchangia suala la vijana. Vijana nchini wamekosa matumaini kabisa. Tunahitaji kurejesha matumaini kwa vijana wetu, vijana ndiyo Taifa la leo. Vijana wana mchango katika Taifa hili, ni lazima waangaliwe, ni lazima Serikali iwe na mkakati wa uhakika wa kusaidia vijana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ipo Dar es Salaam, Wizara haina vitengo vya Vijana katika Halmashauri zetu, vijana wengi wapo Wilayani, ni lazima kuwe na vitengo vinavyoshughulikia masuala ya vijana. Mfano, kijana aliyeko Karatu haiwezekani kama ana shida aende Wizarani Dar es Salaam, kwanza hata hiyo hela hana. Ni vema kukawa na kitengo ili kuwe na mawasiliano ya Wizara na kwenye Halmashauri kuwe na vitengo vya namna hiyo angalau itaweza kuwasaidia vijana kupata taarifa mbalimbali lakini na kushauriwa katika mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba na Mheshimiwa Amina Abdallah Amour ajiandae.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, niseme naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja lakini naomba kwanza mambo yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, hela zilizotengwa kwa Mfuko wa Vijana hazitoshi, hizi hela shilingi bilioni tatu hazitoshi kabisa. Naomba Waziri uwasiliane na Waziri wa Fedha, muongeze hela za kutosha na katika hela hizo, uniambie hela zitakazokwenda kwa vijana wa Tarime ni shilingi ngapi ili nikiondoka niende niwaambie vijana wa Tarime wanapelekewa shilingi ngapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili naomba kuongelea suala la Waandishi wa Habari. Mimi naomba kuwaasa Watanzania kwamba tunaoajiri Waandishi wa Habari kwa kweli hatuwatendei haki lakini vilevile Waandishi wa Habari wajue wanachokiandika ni nini, waepuke uchochozi ambao hauna tija katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi leo nitaomba nijiekeleze zaidi katika lugha ya Kiswahili na Fasihi ya Kiswahili.

Nafahamu kabisa kwamba lugha ya Kiswahili ndiyo imetuunganisha na kutufanya sisi Watanzania tuitwe Watanzania, kwa sababu ukienda katika nchi mbalimbali zaidi ya kumtambua Mwalimu Nyerere na viongozi wengine wa Kitaifa, wanafahamu Kiswahili. Sasa ni aibu kwa kweli kama hatuna mkakati madhubuti wa kukuza lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, tuna vyombo mbalimbali vya kukuza lugha ya Kiswahili, naomba kuvinukuu kwa ridhaa yako. Tuna TUKI ambayo sasa hivi tunaita TATAKI yaani Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, BAKITA, UKUTA, TAKIRUKI, CHAKA - Chama cha Kiswahili Afrika na UWAVITA. Utakuta hivi vyama vinakabiliwa na matatizo mbalimbali na hakuna chombo mahsusi cha kuwaunganisha watumishi katika vyombo hivi. Kwa mfano, TUKI utakikuta kiko Idara ya Kiswahili au Taasisi ya Uchunguzi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, BAKITA inajitegemea yenyewe, iko chini ya Wizara hii, UKUTA ni chama ambacho kinakuza ushairi wa Kiswahili Tanzania, lakini sasa hivi hakidhaminiwa wala hakipewi hela hata kidogo, TAKIRUKI ni Taasisi ya Kukuza Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar, CHAKA ni Chama cha Kiswahili Afrika na UWAVITA ni Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania. Utakuta kwamba Waandishi wengi hasa wa fasihi ambao ndiyo wasanii, acha wale wanaorukaruka kama Mheshimiwa Sugu na kuimba nyimbo za mitaani mnasema ni wasanii, wale wanaoandika ndiyo wasanii hasa, hao watu hawathaminiwi na hawapewi *royalties* zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tuangalie Taifa kama Taifa, tunawaenzije waandishi wa vitabu hasa waandishi wa vitabu vya fasihi, acha wale waandishi wa vitabu vya taaluma kama Nyambali Nyangwine alivyoviandika hivyo, hivyo kwa sababu vya taaluma lazima vinunuliwe lakini vitabu vya fasihi, kwa kweli kuviuza ni kazi ngumu sana. Tuwe na mkakati, Mheshimiwa Waziri tuangalie mkakati wa kukuza na kuanzisha Shirika la Uchapishaji la Taifa ambalo litakuwa na kazi kubwa ya kuhakiki na kuchapisha Miswada ya waandishi chipukizi, hao ndiyo wasanii asilia lakini hawa ambao wanakwenda wanaruka, wanafokafoka

mnasema ni wasanii siyo kweli. Wasanii asilia ni wale wanaoandika vitabu na katika nchi zozote zile tunajivunia wasanii wanaoweza kuandika vitabu, hao wanaojiita wasanii wanaigiza tu. Kwa hiyo, naomba hilo tulizingatie. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hilo litafanikiwa kama BAKITA itakuwa ndiyo inaangalia mashirika mengine yote ambayo yanahusika lakini vilevile BAKITA itafanikisha tu kama tutaiwezesha kwa kuwapa hela ya kutosha na iwe ni ruzuku kutoka Serikalini na wakati fulani hata tunapopeleka Miswada mbalimbali kwa sababu ya kupatiwa ithibati tuweze kuichangia. BAKITA ifanye kazi ya kusanifisha Kiswahili maana Kiswahili sasa hivi unajua ili kikue na kiendelee zaidi tunakitegemea kitoe maneno kutoka katika jamii inayokizunguka hasa wale vijana wa mitaani ndiyo wanaokuza Kiswahili lakini ukisema kwamba Kiswahili siyo sanifu, Kiswahili hiki hakijafuata sarufi ya Kiswahili, lugha haiwezi kukua, lugha inakuwa pale ambapo inazalisha maneno kutoka mitaani. Kwa hiyo, tuangalie namna gani maneno yakiibuliwa kutoka mitaani, ya waimbaji wanaoimba kutoka huko mitaani na wengine basi tuweze kuyasanifisha na yaweze kutumika kama Kiswahili sanifu, hapo Kiswahili kitakuwa.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika niongelee sera ya lugha. Katika nchi yetu ya Tanzania hatuna sera ya lugha. Ni aibu kuingia katika karne ya 21 na sasa hivi tunaingia katika utandawazi na wakati mwingine tunasema utandawizi, hatuna lugha shindani ambayo inaweza ikashindana kimataifa. Hapo tunajiuliza kwamba sijui tunatumia fikira zipi?

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu kwa ridhaa yako, kuna mtu mmoja alisema kwamba, kwa kweli ni aibu katika nchi kama Tanzania kuingia katika utandawazi tukiwa na lugha ambayo watu wengine wanaithamini na kuiona kwamba ni bidhaa adimu katika nchi yetu lakini sisi tunaidharau. Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba semina zote za viongozi, semina zote tunazotakiwa kufanya hata

hapa Bungeni kama tunafanya semina tutumie lugha ya Kiswahili kwanza, hapo tutakuza lugha yetu ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile sera ya lugha ya Kiswahili katika nchi yetu inakidhalilisha sana Kiswahili na inapandisha hadhi lugha ya Kiingereza. Tufahamu kwamba kuna aina mbili katika lugha. Kuna lugha ya kwako ambayo ni ya kujielewa na lugha ya mawasiliano ambayo ni lugha ya kujijua. Kiswahili ni lugha ya kwako yaani lugha ya kujielewa. Ndiyo maana tunapofanya sala zetu kwa sisi hapa tunaomba kwa wazee, waganga, wahenga na Mungu. Hatuwezi tukapata sala moja kwa moja kutoka kwa Mungu tunapitia katika hizo sehemu. Sasa Mungu anaweza akaelewa zaidi na akatuelewa tukimwomba kwa Kiswahili lakini tukimwomba kwa Kiingereza wale wazee hawataweza kuelewa. Kwa hiyo, hebu tuangalie namna gani tutumie lugha yetu ya Kiswahili ili tuweze kuwasiliana na Mungu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine tutumie lugha gani kutolea elimu. Unajua ni uamuzi wa dhahiri, kupanga ni kuchagua na elimu yetu haiwezi ikakua wala ikaendelea kama tutaendelea kutumia lugha ya mawasiliano. Hakuna Mtanzania yeyote anayekatazwa kutumia lugha yoyote anayopenda. Atumie Kichina, atumie Kifaransa, atumie Kiingereza ili aweze kuwasiliana na mataifa mengine lakini kwa kweli tunataka Serikali itamke hadharani kwamba sasa hivi ni muda muafaka wa kutumia lugha ya Kiswahili na kama itashindikana basi tutumie lugha ya Kiswahili kuanzia darasa la kwanza mpaka Chuo Kikuu kama somo la lazima na hali kadhalika somo letu la uraia huwezi kulifundisha kwa lugha ya Kiingereza, huo ni utumwa wa kimawazo. Kwa hiyo, nawaombeni kwa kweli tujitambue na tujielewe, tuthamini lugha yetu ya Kiswahili kama lugha ya bidhaa itakayoweza kutuwezesha na kuwapatia Watanzania wengi ajira.

Mheshimiwa Spika, narudia kusisitiza kwamba haya yote yatawezekana endapo Serikali kama Serikali itakuwa na Shirika la Uchapishaji wa Vitabu yenyewe. Tanzania tulikuwa na Shirika la Uchapishaji la Vitabu, *Tanzania*

Publishing House - TPH limeshabinafsishwa na kuuzwa. Kwa hiyo, sasa hivi hatuna shirika linalochapisha vitabu na sasa hivi tunategemea wafanyabiashara kama Nyangwine ndiyo wachapishe vitabu vya kutumika mashuleni. Kwa hiyo, naomba ili kuinua lugha ya Kiswahili tuwe na mkakati wa makusudi wa kuanzisha shirika la kuchapisha vitabu nchini kwetu. Hiyo itatuwezesha kufanya mambo yafuatayo, kwanza, ukalimani, mbili tafsiri na tatu tutaweza kuitumia lugha ya Kiswahili hasa katika maeneo kama ya utalii na sehemu nyinginezo na tutapata ajira kubwa sana kuwaajiri Watanzania wengi ambao wataweza kuwa wakalimani au wafasiri kwa wageni wanapokuja kutembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja ambalo limeongelewa kuhusu vazi la Taifa. Unajua katika nchi yetu, hilo jambo lisituhangaishe kichwa. Kwa mfano, Mheshimiwa Mwigulu Mchemba namwona kila siku anavaa skafu ya bendera ya Taifa. Tubuni vazi moja ambalo litakuwa na bendera ya taifa, hilo litatuwezesha kututambulisha wote popote pale tunakokwenda, mtu akiangalia ile bendera anajua kuwa ni Mtanzania lakini tukikaa kila siku tunaumiza vichwa kwamba vazi, vazi, vazi, tuna mambo mengi sana ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba mimi nimjibu dada yangu Cecilia Paresso pale aliposema kwamba Mwenge wa Uhuru hauna faida yoyote ile. Kwa kweli huu ni utumwa wa mawazo. Mwenge wa Uhuru una nafasi kubwa sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ndiyo unaotuunganisha na kutufanya tuonekane kama kitu kimoja. Sasa mnavyosema kwamba tuue Mwenge wa Uhuru nini kitatuunganisha? Dada yangu nikija kule Karatu kama hakuna Mwenge wa Uhuru wa kutuunganisha, nini kitatuunganisha? Mwenge wa Uhuru ndiyo unaotuunganisha. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba ni kweli Watanzania wote tena sisi Wabunge tuchangie sana Mwenge wa Uhuru. Kama Walimu wanachanga shilingi elfu tatu, sisi Wabunge

tuchange shilingi elfu kumi kwa sababu Mwenge wa Uhuru ndiyo unaotuunganisha.

WABUNGE FULANI: Aaah!

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Tukumbuke maneno aliyosema Mwalimu Nyerere kwamba Mwenge wa Uhuru utawashwa juu ya Mlima Kilimanjaro, utaondoa chuki na utaondoa na mambo mengine yote, pale palipo na chuki utaleta faraja. Sasa tukiondoa Mwenge wa Uhuru, chuki zitaendelea kuwepo, kila siku tutaendelea kutukanana. Wale wanaobeza Mwenge wa Uhuru, msanii mwenzangu Sugu, kwenye taarifa yako umebeza Mwenge wa Uhuru, mimi nakusihi sana na kusisitiza kwamba Mwenge wa Uhuru ni muhimu na ndiyo unaotuunganisha kokote kule ambapo watu wamekata tamaa, Mwenge wa Uhuru ukifika unawatia matumaini. Wale waliokata tamaa ya kutawala Mwenge wa Uhuru ukifika na wenyewe unaonyesha kwamba bado mtaendelea kutawaliwa katika nchi ya Tanzania. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaombeni jambo moja kwamba Mwenge wa Uhuru ni muhimu sana uwepo na tuushangilie. Nakuomba Mr. Sugu uutungie wimbo wa kuusifia Mwenge wa Uhuru na mimi nitaufadhili wimbo huo. Mimi najitolea kuuchapisha huo wimbo na kukutolea *CD* ili zikunufaishe lakini uusifie sana Mwenge wa Uhuru. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Amina Abdalla Amour, utakuwa msemaji wetu wa mwisho jioni ya leo.

MHE. AMINA ABDALLA AMOUR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyokuwepo mbele yetu. Mimi nitaanza kuzungumzia vyombo vya habari jinsi ambavyo vina nafasi kubwa katika kutunza amani ya nchi yetu na nitatoa mifano ya nchi mbili ambazo

zimekiuka misingi ya uandishi na matokeo yake. Nitaanza na Rwanda. Nchi ya Rwanda ilitumia vibaya vyombo vya habari na kuleta uchonganishi na ushawishi mkubwa kwa kuleta uchuki na kusababisha mauaji ya watu wa Rwanda na wengine wakakimbia makazi yao. Jambo la pili lilitolea hapo jirani Kenya katika uchaguzi wa mwaka 2007. Vyombo vya habari vilitumika vibaya na matokeo yake mauaji yakatokea na wengine wakahama nchi. Kenya ilifika kugeuka wao ndiyo Tume ya Uchaguzi, ikatoa matokeo ambayo siyo ya uchaguzi na hii ilisababisha machafuko makubwa, wengine wakakimbia makazi yao na wengine wakauawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi kuchukua nafasi hii adhimu kuviasa vyombo vya habari vya Tanzania visikubali kutumika vibaya kwani kutumika kwao vibaya ni kusababisha mauaji ya watu wengi na haya mauaji yakija hayachagui dini, hayachagui mwanamke, hayachagui mwanamume, sote tutauawa. Kwa hivyo, naviasa vyombo vya habari visikubali kutumika vibaya. Japokuwa vingine ni vya wanasiasa, mimi sina tatizo ikiwa kuanzia *page* 1-6 ya gazeti wakajipamba wao tu wanasiasa lakini wahakikishe wanafuata maadili ya waandishi wa habari. Anaweza *page* moja akaweka picha yake lakini aandike habari zilizokuwa nzuri. Anaweza pia *page* ya pili wakatia picha zao lakini waandike habari nzuri lakini wasithubutu hata siku moja kuvunja maadili ya uandishi wa habari. Namalizia jamani kwa kuomba Watanzania wote, kwa kuwa saa hizi tayari kuna viashiria na dalili ya kuvunjika amani, Watanzania wote tuiombee nchi yetu ya Tanzania amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nataka kuzungumza kuhusu lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ni nzuri sana na tunaweza kuiboresha lakini huu umri niliofikia mimi, hii leo nakaribia kunako miaka 60, hayo maneno ninayosikia Bungeni sijapata kuyasikia maisha yangu. Sijui Kiswahili kimetoka wapi hiki kilichosemwa humu Bungeni. Sijapata kusikia maisha yangu, mengine siwezi kuyasema. Nataka kutoa mfano. Juzi nilitoa mfano mdogo tu lakini leo sitoi mfano lakini kuna maneno yanayosemwa humu ni matusi kabisa kwa

Wazanzibar. Kwa hiyo, nakuombeni, tuboreshe Kiswahili, hiki Kiswahili tunachozungumza hapa siyo Kiswahili. Baadhi ni Kiswahili lakini haya maneno mengine ni ya matusi tena matusi makubwa mnayazungumza. *(Kicheko)*

WABUNGE FULANI: Sema!

MHE. AMINA ABDALLA AMOUR: Siwezi kusema, juzi nilisema siwezi kurudia tena. Mheshimiwa Waziri analifahamu nililomuambia juzi. Kuna mengine kuliko yale, basi ujue kwamba ni tusi kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nazungumzia kuhusu Wizara hii. Wizara hii bajeti ni ndogo mno. Naiomba Serikali iwazidishie japokuwa imeongeza kidogo lakini bado ni bajeti ndogo mno. Tunataka *TBC* isikike ulimwengu mzima. Kwa hivyo, naiomba Serikali iwaongezee bajeti Wizara hii ili tuweze kusikika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ni hayo tu, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, kuna dakika 10 unaweza kutoa mchango wako.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuwapa pole wale wote ambao walijeruhiwa wakati wakifanya shughuli zao, waandishi mbalimbali wa habari akiwemo Daudi Mwangosi ambaye alifariki, Abslom Kibanda, Mhariri aliyejeruhiwa, Ndugu Shaban Mtutu, Gazeti la Mtanzania, Ndugu Mnaku, Mhariri wa Majira, Said Kubenea zamani, Gazeti la Mwanahalisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nachukua nafasi hii kuwapa pole hawa wote ambao walipata majanga, hawa Waandishi wa Habari. Kwa kweli natoa pole sana.

Mheshimiwa Spika, watu wa Mkoa wa Lindi wanapenda sana michezo. Kwa hiyo, nianze na suala la michezo. Kwanza suala la kukarabati viwanja. Kiwanja cha Mkoa wa Lindi kinahitajiwa kukarabatiwa kwa sababu tangu mwaka 1950 wakati kikitumika kuchezea mipira ya Afrika Mashariki wakati ule walikuwa wanasema *Gossage*, mpaka leo kipo vilevile. Kiwanja hiki ndicho kilichozaa wanamichezo wengi wa Tanzania. Wachezaji wengi wa kitaifa walikuwa wametoka Lindi lakini kwa kupitia uwanja ule.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaomba uwanja wa Mkoa wa Lindi ukarabatiwe ili michezo iweze kuendelezwa. Kwa sababu moja ya ajira katika Mkoa wa Lindi ni michezo na kwa njia hiyo tuliweza kupata wachezaji mbalimbali katika Mkoa wa Lindi. Hapa ninayo majina ya wachezaji hawa na ningeomba vizazi vinavyofuata vilevile viweze kupenda michezo kama walivyopenda hawa. Tunaye Rashidi Inzi ambaye ni mchezaji maarufu sana alichezea Taifa, nafikiri wananchi mnamfahamu huyu. Tunaye mchezaji maarufu ambaye anaitwa Akwitende alitoka Lindi, nafikiri watu mnamfahamu huyu mchezaji mzuri sana. Tunaye Mheshimiwa Salumu Madadi, yeye sasa hivi ni Mshauri wa Makocha wote Tanzania *TFF*, yule anatoka Lindi. Tunaye Rashidi Chuma, mchezaji maarufu Tanzania na alichezea Taifa zamani, hawa wanatoka Lindi. Tunaye Mohamed Dini anatoka Lindi. Nikihesabu hapa tunaweza kupata wachezaji zaidi ya 10 wanatoka Lindi lakini uwanja ule ndiyo ulizaa matunda ya kuwapata wachezaji bora Tanzania na wamechezea kitaifa mpaka nchi za nje. Sasa tunaomba uwanja wa michezo Lindi uweze kukarabatiwa ili michezo hii iweze kuendelezwa katika Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la wafadhili. Mimi nawashukuru sana wafadhili ambao wanasaidia michezo mbalimbali hasa shuleni. Kwa mfano, *NMB, PPF, LAPF, TBL, Coca Cola, SDA. SDA hawa ni Sports Development Aid.* Hawa wamechangia sana michezo shuleni. Hivi sasa ni mbinu nzuri ya kuwezesha michezo iendelezwe kuanza kuchangia michezo shuleni. Hawa *SDA* au *Sports Development Aid* wanaendelezwa na kijana mmoja anaitwa

Mohamed Chigogolo. Hawa wameweza kutoa mipira kadhaa katika zetu, shule zote za Mkoa wa Lindi 462 wameweza kutoa magoli ya netiboli na magoli ya *footbal.* Sasa tunaomba na wengine vilevile waendeleze michezo katika maeneo mengine. Vilevile wameweza kuchangia mipira 5,400 lakini hawa wanakwazwa na vitu vyao kukwama bandarini. Kwa mfano, sasa hivi kuna kontena moja tangu mwaka jana mwezi wa tisa, kontena lile lina mipira 5,400 ya shule mbalimbali za msingi katika Mkoa wa Lindi lakini mpaka leo liko bandari halijatolewa. Tunaiomba Serikali iwasaidie ili kuweza kulitoa hili konteina. Kwa sababu mwaka jana kontena lilikuwa linatolewa kwa shilingi milioni 10 sasa hivi wameongeza kodi, ni shilingi milioni 16. Hawa vijana ni *NGO* tu. Hawawezi, hawana pesa. Tunaomba sana Serikali isaidie kutoa vifaa hivi bandarini ili viende shuleni kwa sababu ni muhimu sana kuanza michezo shuleni. Wanasema samaki mkunje angali mbichi. Kwa hiyo, tuanze michezo shuleni. Tunaomba Serikali itusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye suala la vijana hawa wanaopata mimba za utotoni. Tunafanya nini? Tunawasaidiaje watoto wanaopata mimba shuleni. Mimi wazo langu ni kwamba turudi zamani mtindo wa kuwa na *syllabus* ya michezo shuleni, *syllabus* ya ufundi mashuleni. Zamani kulikuwa na *syllabus* ambayo inakuwa na ufundi chuma, fundi seremala, fundi uashi, fundi michezo na fundi upishi. Sasa wakisoma mle kwenye ufundi mbalimbali, wakimaliza shule, wakienda nyumbani, kwa kweli watoto hawa wanakuwa mafundi tayari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeshauri kwamba turudi katika *syllabus* ya nyuma, tuangalie mfumo huu wa kuwa na ufundi mbalimbali katika shule za msingi ili hawa watoto wasome watakapotoka waweze kuwa mafundi. Sisi kwetu Lindi tunaomba sana suala hili mtusaidie kwa sababu tulikuwa nazo shule hizo za ufundi shuleni kwa kila Wilaya. Kwa mfano, Wilaya ya Kilwa kulikuwa na Singino, Njinjo na Kipatimo. Wilaya ya Liwale kulikuwa na Mbarikiwa na Chimbuko, shule za ufundi hizo. Wilaya ya Rwanga kulikuwa na Mkowe na Mbekenyera. Wilaya ya Nachingwea kulikuwa

na Kilimarondo, Mnero na Marambo. Wilaya ya Lindi Mjini kulikuwa na Mpilipili na Wilaya ya Lindi Vijijini kulikuwa na shule ya Mtama. Shule hizi za ufundi zilikuwa zinafundisha ufundi chuma, seremala, uashi, michezo na upishi. Hii itasaidia ajira ya vijana. Tunaomba hizi shule zifufuliwe ili kuwasaidia hawa vijana.

Mheshimiwa Spika, suala la vazi la Taifa. Ni kweli tunahitaji vazi la Taifa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapomalizia hotuba yake atuambie hili vazi la taifa limeishaje? Litaanzwa lini? Limekwendaje? Kwa sababu tulisikia wakati fulani walianza kulishughulikia, sasa limeishaje?

Mheshimiwa Spika, nije sasa kwenye suala la mchezo wa mpira wa miguu kwa wanawake *Twiga Star.*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana, muda umeisha.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa siku ya leo. Sina matangazo, kwa hiyo, naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.44 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 21 Mei, 2013)